ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Mhe. Pandu Ameir Kificho	-	SPIKA
1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi		- MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini		- MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary		-MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad		-MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban		-MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji		-MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed		-MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa

12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	-MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	-MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	-MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	-MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	-MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	-MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	-MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Omar Othman Makungu	- Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	-Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	- Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	-Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	-Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	-Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	- Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	- Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	- Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	- Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Salum Haji	- Jimbo la Kwahani
33.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	- Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asaa Othman Hamad	- Jimbo la Wete
35.Mhe. Asha Abdu Haji	- Nafasi za Wanawake
36.Mhe. Asha Bakari Makame	- Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Ashura Sharif Ali	- Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	- Nafasi za Wanawake

39.Mhe. Farida Amour Mohammed - Nafasi za Wanawake

40.Mhe. Fatma Mbarouk Said - Jimbo la Amani

41.Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Kwamtipura

42.Mhe. Hassan Hamad Omar - Jimbo la Kojani

43.Mhe. Hija Hassan Hija - Jimbo la Kiwani

44.Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Jimbo la Mji Mkongwe

45.Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Muyuni

46.Mhe. Kazija Khamis Kona - Nafasi za Wanawake

47.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa - Jimbo la Kikwajuni

48.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Jimbo la Kitope

49.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Jimbo la Mkwajuni

50.Mhe. Mgeni Hassan Juma - Nafasi za Wanawake

51.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma - Jimbo la Bumbwini

52.Mhe. Mohammed Haji Khalid - Jimbo la Mtambile

53.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi - Jimbo la Chambani

54.Mhe. Mohammed Said Mohammed - Jimbo la Mpendae

55. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak - Nafasi za Wanawake

56.Mhe. Mussa Ali Hassan - Jimbo la Koani

57. Mhe. Mussa Khamis Silima - Jimbo la Uzini

58.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

59.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Rahaleo

61.Mhe. Omar Ali Shehe - Jimbo la Chake-Chake

62.Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

63.Mhe. Rashid Seif Suleiman - Jimbo la Ziwani

64.Mhe. Raya Suleiman Hamad - Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Rufai Said Rufai - Jimbo la Tumbe

66.Mhe. Saleh Nassor Juma - Jimbo la Wawi

67.Mhe. Salim Abdalla Hamad - Jimbo la Mtambwe

68.Mhe. Salma Mohammed Ali - Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Salma Mussa Bilali - Nafasi za Wanawake

70.Mhe. Salmin Awadh Salmin - Jimbo la Magomeni

71.Mhe. Salum Amour Mtondoo - Jimbo la Bububu

72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha - Jimbo la Mwanakwerekwe

74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan - Jimbo la Dole

75.Mhe. Subeit Khamis Faki - Jimbo la Micheweni

76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis - Jimbo la Konde

77.Mhe. Ussi Jecha Simai - Jimbo la Chaani

78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake

79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim - KATIBU

Kikao cha Nane – Tarehe 01 April, 2011

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

KIAPO CHA UAMINIFU

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujamuapisha Mhe. Mwanasheria Mkuu katika Baraza Mkutano wa Kwanza, nilishauriwa kwamba tufanye utaratibu ili wakati wa kuapishwa nishuke chini iwe wepesi kwa anayechukua kiapo hatimaye kuweza kupeana mikono bila ya kupanda huku juu.

Kwa kuwa ushauri huo hauvunji taratibu zetu za kanuni naona tuuchukue na itakuwa ni wepesi kwa yule anayeapa kuweza kufanya kiapo hicho na kuonekana kwamba Spika, kweli ndiye anayeapisha kwa sababu hata zile picha haionekani kama Spika yupo anamuapisha Mhe. Mjumbe.

Tutaufuata taratibu huo, nitashuka chini na halafu kiapo kitaendelea.

Mhe. Othman Masoud Othman (Mwanashiria Mkuu wa Serikali): "*Mimi Othman Masoud Othman, naapa kwamba nitakuwa muaminifu kwa Zanzibar katika kazi zangu za uwakilishi na nitaitumikia kwa moyo wangu wote na kwamba nitazihifadhi, nitazilinda na kuzitetea kwa dhati Katiba ya Zanzibar na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nakuomba Mwenyezi Mungu unisaidie". (Makofi).*

(Mhe. Spika, alipanda juu na kukalia kiti chake)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwanza nichukue nafasi hii kukushukuruni kwa kushuhudia kiapo cha Mhe. Mwanasheria Mkuu kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Pia nichukue nafasi hii kumshukuru sana mwenzetu Mhe. Othman Makungu ambaye alikuwa Mwanasheria Mkuu wetu kwa kiasi cha miezi mitano hivi, tumefanya kazi naye vizuri, kwa mashirikiano makubwa mpaka jana alipopata uteuzi wa kuwa Jaji wa Mahakama Kuu.

Naomba nimkaribishe Mhe. Othman Masoud Othman Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwa na yeye ni Mjumbe katika Baraza hili kuanzia leo hii, baada ya

uteuzi uliofanywa rasmi jana na leo hii kuchukua kiapo kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi. Yeye kwa nafasi yake akiwa ni Mwanasheria Mkuu moja kwa moja anakuwa ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwanashiria Mkuu karibu sana kwa mashirikiano makubwa pamoja na waheshimiwa wajumbe na utaisaidia sana serikali kama vile inavyotegemewa. Wajumbe wamefarijika kuwa pamoja nasi hapa kwa kazi zako kama Mwanasheria mkuu wa serikali. karibu sana. Ahsanteni sana.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari: Mhe. Spika, kabla sijawasilisha Hati Mezani na mimi nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha siku hii ya leo kuamka salama kwa ajili ya mintaraf ya shughuli zetu za kitaifa.

Mhe. Spika, na mimi nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mwanasheria Mkuu ambaye ameapisha hivi punde.

Baada ya hayo Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha Hati Mezani ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi: Ahsante sana Mhe. Spika. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia uhai na uzima. Pia nimpongeze sana Mwanasheria Mkuu kwa kuchaguliwa kwa uwezo wake na Mwenyezi Mungu amjaalie kila la kheri.

Mhe. Spika, na mimi naomba kuwasilisha hati ya Kamati yangu ya Mawasiliano na Uchukuzi kwenye Meza. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala: Mhe. Spika, na mimi niungane na wenzangu waliotangulia kumshukuru Mwenyezi Mungu na pia kumponga Mwanasheria wetu Mkuu aliyeapishwa sasa hivi.

Baada ya hayo naomba kuwasilisha Mezani Hotuba ya kuwasilisha ripoti ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 100

Usalama wa Viongozi Katika Kusimamia na Kuzitekeleza Sheria za Serikali

Mhe. Ali Salum Haji - Aliuliza:-

Tarehe 17/02/2011 saa 2 usiku, Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa RASHID ALI JUMA alimwagiwa Tindi kali (*acid*) na mtu asiyejulikana. Kitendo alichofanyiwa Mkurugenzi huyo ni cha kulaaniwa na kupigwa vita.

Hata hivyo ni pigo pia kwa serikali kwani kimeonyesha kwamba viongozi wa serikalini wapo hatarini kufanyiwa vitendo viovu hususan wale wanaoonekana kusimamia na kuzitekeleza sheria za nchi kama ilivyokuwa kwa Mkurugenzi huyo.

(a) Je, serikali imejipanga vipi katika kuhakikisha usalama wa viongozi ili kuwakinga na matukio ya kuhujumiwa?

(b) Serikali inatoa kauli gani kwa wananchi dhidi ya vitendo viovu kama hivi?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 100 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza naomba nimpongeze sana Mhe. Mwakilishi katika maelezo yake na hasa alivyoonyeshwa kukasirishwa na kitendo hiki cha kumwagiwa tindi kali kiongozi wetu huyu au Mkurugenzi wa Manispaa.

(a) Mhe. Spika, napenda kumuhakikishia Mhe. Mjumbe kuwa serikali kwa nyakati tofuati imekuwa ikiwapatia ulinzi tena nathubutu kusema mkali sana, Viongozi wake wakuu na viongozi wengine kulingana na mazingira yanavyojitokeza na hali ya usalama ilivyo. Kwa hili serikali haina mzaha hata kidogo, tunatumia walinzi wenye sare na walinzi wasio na sare. Kwa vile mtu akikusudia ubaya hatujui ubaya huo ataufanya wakati gani na ataufanya pahali gani. Hawa wenzetu ndio walichukua *advantage* hii kwa kumshambulia kiongozi huyu wakatii akitoka Msikitini.

(b) Mhe. Spika, serikali ilikwishatoa tamko la kulani vikali tukio hilo kupitia vyombo vya Habari tarehe 18/02/2011, 19 na tarehe 20, mwaka 2011. tamko hilo nililitoa mwenyewe na hata magazetini mliona na kwenye vyombo vya habari vyengiine lilitoka.

Mhe. Spika, kupitia Baraza lako Tukufu serikali inawaomba Waheshimiwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi nao **KUKILAANI KITENDO HICHO NA VILE VYOTE VYA KUJICHUKULIA SHERIA MIKONONI.** Ahsante.

Nam. 126

Vijana Wanaojiunga na JKU na JKT

Mhe. Mbarouk Mussa Wadi (Mtando):(Kny: Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Aliuliza:-

Katika mipango yetu ya Kitaifa vijana wetu wote wanapomaliza skuli hutakiwa kuiunga na JKU na JKT kwa madhumuni ya kujiweka tayari kimaisha.

(a) Vijana wanaokwenda JKT Bara kwa mwezi hupata posho ya sabuni ya Shs. 70,000/=. Kwa nini vijana wetu wanapojiunga na JKU tunashindwa kuwapatia fedha ya sabuni.

(b) Je, baada ya vijana wetu kumaliza JKU na JKT serikali imewaandalia nini katika kuanza maisha mapya.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam, 126 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, vijana wetu wanapomaliza skuli hupelekwa Makambini kujifunza Mafunzo ya Amali ili wanapomaliza waweze kujitegemea kwa kujiajiri wenyewe. Ni kweli hivi sasa vijana hao hawapatiwi posho la sabuni lakini suala hilo ni zuri na tunalikubali. Lengo lake hasa ni kuwahamasisha vijana wajiunge na hizo kambi na pia waweze kujikimu kwa mahitaji madogo madogo.

Huko nyuma hali hiyo ilikuwepo lakini kadiri mambo yanavyokuwa magumu ya kiuchumi na ule mpango mzima wa JKU kidogo ulivurugika basi mambo yale yaliparaganyika.

Mhe. Spika, naomba niwahakikishie Wajumbe kwamba sasa tunajipanga upya kuweka mambo mazuri katika kambi zetu zote ya JKU na kuhakikisha kwamba vijana wanaokwenda wanapata mafunzo yale yaliyokusudiwa na wao waweze kujitegemea na hali zao zisiwe mbaya za omba omba. Ahsante.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kumuuliza Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri huoni kutokuwajiri hawa vijana ni kuongeza ujambazi?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, sheria iliyoanzisha JKU ya Nam. 6 mwaka 2003 ilikuwa na majukumu naomba niyataje kama matano:-

1) Kuwatunza vijana kulitumikia taifa lao.

2) Kuwafunza masuala ya uchumi, kilimo, viwanda vidogo vidogo, uvuvi na mafunzo ya amali.

3) Kuwafanya waweze kujiajiri pale wanapomaliza masomo yao na hata baada ya kumaliza mafunzo ya JKU. Sio kuwaajiri. Tutaajiri wangapi?

4) Tunawatayarisha waweze kuyakabili maisha, kule wanafunzwa ushoni, mbinu bora za kilimo, mbinu bora za uvuvi na mbinu mbali mbali.

5) Wanafunzo mambo ya kijeshi wawe wakakamavu ili kuweza kuhimili kishindo chochote cha ulinzi katika nchi yetu.

Hiyo ndio hasa misingi ya JKU. Itakapotokea nafasi za ajira za kudumu basi pale wanachukuliwa. Kwa wale ambao watabaki mle kuwafunza wengine. Ahsante.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mhe. Waziri utakubaliana kwamba hivi karibuni jeshi la wananchi wa Tanzania limeajiri vijana wa JKT wapatao elfu mbili. Lakini tulizoea kuona kwamba Jeshi hilo likiajiri huajiri na JKU. Mwaka huu wa fedha hatukuona hata mwananchi mmoja wa Zanzibar kuajiriwa. Je, huoni kwamba hilo ni kosa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, ni kweli kwamba JKT na Jeshi la Wananchi waliajiri vijana na pia hatukuwachwa nyuma sisi SMZ tulishirikishwa na wapo vijana wetu waliopata hizo ajira.

Tatizo tulilonalo na si hapa Zanzibar peke yake hata huko Bara vijana wengi huwa hawana sifa zinazotakiwa. Sifa zenyewe ni za msingi tu. Uwe umepasi darasa la 12, kwa bahati mbaya vijana wanachukuliwa wengi wanavyeti vya kufoji, baada ya kwenda *interview* mtu hata sentensi ya kiingereza moja hawezi kusema.

Siku hizi kwenye jeshi kuna mambo ya kwenda kitaalamu. Unafunzwa kupiga mzinga kwa degrees kwa kila kitu. Kwa hivyo angalau ujue mambo ya hesabu na mambo ya msingi. Kwa bahati mbaya sana vijana wetu wanafeli hizo *interview*. Tunawachukua wengi wanakwenda kwenye *interview* wanarudi. Sheria inasema wazi sasa kwa mtu yeyote kwenda JW basi ni lazima apitie JKT au JKU.

Nam. 118

Kutopatiwa Fedha Mradi wa Afya ya Akili

Mhe. Jaku Hashim Ayub - Aliuliza:-

Katika Bajeti ya mwaka wa fedha uliomalizika, Wizara ya Afya iliidhinishiwa na Baraza hili la Wawakilishi jumla ya Tshs. 95,000,000/= kwa ajili ya Mradi wa Afya ya Akili, lakini hapakuwa na hata senti moja iliyolipwa kwa Wizara ya Afya kwa ajili ya Mradi huo.

Je, Mhe. Waziri huoni kwamba kufanya hivyo kunadhofisha utoaji wa huduma ya wagonjwa wa akili hapa Zanzibar?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa kabla ya kujibu swali la Mwakilishi naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa na itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kutekeleza jukumu lake la kuwapatia wananchi wa Zanzibar tiba kwa lengo la kuimarisha na kutunza afya za wananchi wetu. Hata hivyo katika kutekeleza majukumu ya serikali Baraza lako Tukufu hupitisha Bajeti ya Serikali kwa Wizara na vifungu mbali mbali ikiwa ni pamoja na kifungu kwa ajili ya mradi wa afya ya akili.

Aidha katika mwaka wa Fedha 2009/2010 kifungu cha mradi wa afya ya akili kilitengewa shilingi milioni 107 na sio shilingi 95 milioni kama Mhe. Mwakilishi alivyoeleza.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo mafupi kwa heshima yako sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 118 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, mradi wa Afya ya Akili haukupatiwa fedha hizo kutoka mfuko Mkuu wa serikali. Hali hii imetokana na kujitokeza kwa mshiriki wa maendeleo yaani Development Partner kutoka falme za Kiarabu ambaye ametoa fedha kwa ajili ya matumizi ya mwaka 2009/2010. kwa mtazamo huo Wizara ya Afya imeona hakuna haja ya kutenga fedha kutoka katika mfuko Mkuu wa serikali, kwani msada uliopatikana unakidhi kutekeleza majukumu yaliyopangwa katika mwaka wa fedha 2009/2010.

Mhe. Spika, kufanya hivyo haina maana kwamba kunadhoofisha utoaji wa huduma ya wagonjwa wa akili bali ni kuzingatia matumizi bora ya fedha za serikali .

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri. Kwa kuwa Waziri wa Afya aliyepita aliahidi kutajengwa hospitali ya wagonjwa wa akili pale Wete kwa ajili ya Pemba na hospitali hiyo haikujengwa.

(a) Namuuliza Mhe. Waziri kutokutolewa kwa fedha hizo ndio kulikosababisha kutokujengwa tena hiyo hospitali?

(b) Ikiwa ni hivyo haoni kwamba ni kikwazo kwa Pemba kutokuwa na hospitali ya wagonjwa wa akili?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza nataka niseme kutokutolewa kwa fedha hizo sio kikwazo cha kutokujengwa hospitali ya wagonjwa wa akili Pemba. Ni matarajio yangu kwamba mahitaji ya fedha kwa hospitali ya wagonjwa wa akili Pemba ni makubwa zaidi kuliko fedha zilizopo hapa.

Hata hivyo napenda kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kama mipango ya Wizara ya Afya bado ipo pale pale kujenga hospitali ya wagonjwa wa akili, wizara yangu itashirikiana na Wizara ya Afya kuhakikisha kwamba hospitali hiyo inapatikana.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Nashukuru kwa kupata fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa ugonjwa wa akili unasababishwa kwanza na urithi na pia namna gani mtoto wakati anapozaliwa. Jengine kutokana na madawa ya kulevya hawa

wanapata ugonjwa huu kwa kujitakia. Ni adhabu gani wataipata baada ya kurejea akili zao kwa hawa wanaopata kwa madawa ya kulevya?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, mgonjwa ni mgonjwa awe anaumwa kwa maradhi yoyote yale *regardless* iwe kwa matumizi ya kulevya. Unapotoa dhamana ya kumtibu mgonjwa huyo na akapona. Si dhani kama tutafanya *justice* ya kusema kwamba unataka kumpa adhabu tena.

La msingi ninaloliona mimi ni kwamba wagonjwa wa akili ambao wametokana na kutumia madawa ya kulevya wanapopata hujambo, nadhani kuna haja kubwa ya jamii kuwajengea kisaikolojia ili wasiendelee kutumia tena madawa ya kulevya, badala ya kusema kwanza kuwaadhibu.

Nam. 62

Kuwasaidia Wavuvi Zana za Uvuvi

Mhe. Abdi Mosi Kombo – Aliuliza:-

Kwa kuwa hivi sasa serikali kupitia taasisi zake imeanza kuchukua hatua mbali mbali za kuzuia uvuvi wa kutumia nyavu zenye matundu madogo kwa kuzikamata nyavu za aina hiyo.

Je, wizara ina mpango gani wa kuwasaidia wavuvi wadogo wadogo hasa wa Matemwe, ambao wamekuwa wakitumia nyavu za aina hiyo na hawana uwezo wa kununua zana nyengine za uvuvi, ili waendelee kujitafutia mahitaji yao?

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 62. Kabla ya kujibu Mheshimiwa Mwakilishi swali hilo naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, serikali kupitia Taasisi yake ya Uvuvi ilianza kazi kubwa ya kutoa taaluma kwa wavuvi pamoja na kuanzisha maeneo ya hifadhi katika mwaka 1997. Aidha serikali baada ya kuona umuhimu wa kuwasaidia Wavuvi (zana na vifaa) ili waachane na uvuvi haramu, iliandaa mpango mzima wa utunzaji mazingira endelevu MACEMP katika mwaka 2005 wenye lengo la kuwasaidia wavuvi ili waendelee kujitafutia mahitaji yao.

Mhe. Spika, serikali pia ilipitia sheria ya Uvuvi ya Mwaka 1988 na kupitisha Sheria mpya Mwaka 2010, ambapo utekelezaji wake ulizingatia misaada tofauti

waliyopewa wavuvi na taaluma ya uhifadhi na uharibifu wa matumizi wa nyavu zenye macho madogo.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo mafupi naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kwamba wizara yangu tayari imeanza kutoa misaada tofauti kwa wavuvi wa Matemwe.

- Kuwapatia boti, *machine* na nyavu, wavuvi wa kijiji cha Kijini – Matemwe yenye thamani ya sh. 15 milioni.

- Matemwe Kilimajuu wamepatiwa Mradi wa Kuku na banda wenye thamani ya Sh. 18 milioni kwa lengo la kuzalisha mayai ili waweze kujinunulia wenyewe nyavu zenye macho yanayokubalika kisheria.

- Kijijini Matemwe wamepatiwa Mradi wa Mwani, banda la mwani pamoja na *'fibre boat'* na *machine* yake kwa jumla ya thamani ya sh. 26 milioni, kwa lengo la kuzalisha ili waweze kujinunulia wenyewe nyavu zenye macho yanayokubalika kisheria.

- Pia Kijini wamepatiwa Mradi wa Uvuvi wenye thamani ya sh. 10 Milioni.

- Pwani Mchangani wamepatiwa mradi wa boti ya utalii pamoja na mradi wa kuku kwa thamani ya sh. 28 milioni ili waweze kuzalisha na kununua nyavu zinazokubalika. .

Mhe. Spika, hata hivyo kwa kuzingatia wingi wa wavuvi wa Matemwe na Shehia zake ni kweli misaada iliyotolewa haijakidhi haja inayohitajika. Mhe. Spika, wizara yangu inaelewa hilo na pia yuko tayari kushirikiana na Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Matemwe Matemwe na Wawakilishi wengine wa Baraza lako tukufu kwa lengo la kuwaendeleza wavuvi katika nchi yetu.

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa ruhusa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri hivyo ni wavuvi wangapi wa Matemwe waliopatiwa nyavu halali.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, ni kwamba idadi anayoihitaji ipo wizarani na naomba muda ili nimletee takwimu halisi kwa maandishi.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri atakubaliana

na mimi kuwa hivi sasa katika ukanda wa Kiwengwa Kairo uvuvi haramu unaendelea kuharibu matumbawe. Je, Mhe. Waziri wizara yako imejipanga vipi kuondoa tatizo hilo kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, ni kweli kwamba nchi yetu haijaweza kuzuia uvuvi haramu kwa asilimia mia, hili tatizo kubwa na jukumu la kuzuia haliko wizarani kwangu peke yake, hilo ni jukumu la kila mwananchi na hasa Wajumbe wa Baraza lako tukufu. Katika maeneo yote ya Zanzibar kuna kamati za shehia ambazo kazi ya ukubwa ni kushirikiana kuona kuwa uvuvi haramu umedhibitiwa. Kwa hivyo, mimi wizara yangu itafanya kila jitihada lakini kwa jumla nahitaji nguvu na misaada ya Wajumbe wa Baraza lako tukufu Mhe. Mwakilishi akiwa ni mmoja wapo. Kwa hivyo, naomba tushirikiane kuona kwamba katika jimbo lake suala hili linakoma kama ambapo maeneo mengine yamepiga hatua kubwa.

Nam. 74

Wananchi Kuwezeshwa Katika Vita Dhidi ya Uvuvi Haramu

Mhe. Rufai Said Rufai – Aliuliza:-

Katika suala la uhifadhi wa mazingira ya pwani Serikali imekuwa ikifanya juhudi za makusudi kuzuia uvuvi haramu na kuwaelimisha wananchi wetu kuhusiana na umuhimu wa kuyatunza mazingira yetu.

(a) Mbali na taaluma na kuzuia uvuvi haramu. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wavuvi wadogo ili waweze kusaidiana na Serikali katika kupiga vita uvuvi haramu.

(b) Kwa nia ya uzuiaji wa uvuvi haramu. Je, Serikali haifikirii haja ya kuwawezesha kiuchumi wananchi hawa.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 74 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu naomba nimpongeze sana Mhe. Mwakilishi kwa kutambua juhudi za makusudi zinazochukuliwa na wizara yangu kuzuia uvuvi haramu na kuwaelimisha wananchi wetu kuhusiana na umuhimu wa kuyatunza mazingira ya pwani yetu. Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, naomba kutoa wito kupitia Baraza lako tukufu kwamba juhudi hizi hazipaswi kusimamiwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi tu, lakini inapaswa kuwa na juhudi ya kila

mwananchi wa Zanzibar chini ya usimamizi wa Wajumbe wa Baraza hili na Viongozi wengine wakiwemo Madiwani, Masheha na Viongozi wa Vyama na jamii kwa jumla. Kuna nchi zilizopuuza kuyatunza mazingira ya pwani zao, sasa zimekubwa na janga kubwa katika pwani na bahari zao. Baada ya maelezo hayo, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi.

(a) Mhe. Spika, mbali na taaluma za kuzuia uvuvi haramu, Serikali kupitia wizara yangu imefanya mambo mawili katika kuwasaidia wavuvi wadogo wadogo.

- Imeshajiisha kuunda Kamati za Uvuvi za vijiji na Shehia na kuziingiza katika Sheria ya Uvuvi ya mwaka 2010. Kamati hizo ni miongoni mwa Taasisi za Kijamii katika mikakati ya kuendeleza uvuvi endelevu.

- Katika kipindi hicho, wizara yangu imetoa misaada kwa jamii za wavuvi wadogo wadogo wenye jumla ya sh. 2.4 bilioni katika maeneo mbali mbali Unguja na 2.5 bilioni Pemba kupitia Miradi ya *MACEMP/TASAF*.

(b) Kwa nia ya uzuiaji wa uvuvi haramu, Serikali hii ya awamu ya saba inafikiria sana haja ya kuwawezesha kiuchumi wananchi hawa, na ndio Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Ali Moh'd Shein akaunda wizara maalum na kumteua Waziri mahiri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika ambapo tayari nimekwisha zungumza nae juu ya haja ya kushirikiana katika kuwawezesha wavuvi wetu kiuchumi.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, nashukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri jana katika swali mama ulipomjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Mtambile ulisema kwamba umewasaidia wavuvi wadogo wadogo boti na *machine* mbali mbali.

a) Je, huoni kwamba Jimbo langu la Tumbe kwa Pemba ndio jimbo mama la kuzalisha samaki na wavuvi hawa wadogo wadogo wapo kwa wingi, huoni kwamba sasa ni wakati wa kusaidia na wao zana kama hizo.

b) Ni wavuvi haramu wangapi ambao wizara yako imewakamata na kuwachukulia hatua.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, nakubaliana nae kwamba Jimbo la Tumbe ni miongoni mwa majimbo yanayochukuliwa na wizara yangu kwamba ni jimbo la kiuvuvi na kwa maana hiyo wizara ina mikakati madhubuti kuona kwamba wananchi wa Jimbo la Tumbe wameendelezwa kiuvuvi, hivi sasa wizara imo katika mchakato kuona kwamba Jimbo la Tumbe linajengewa soko moja kubwa sana katika soko la uvuvi hapa Zanzibar. Baada ya soko hilo ambalo litakuwa na huduma nyingi za kiuvuvi shughuli nyengine zinaandaliwa na wizara yangu kwa ajili ya Jimbo lake la Tumbe. Kwa hivyo, asiwe na wasi wasi awe karibu na wizara yangu na tushirikiane kuona kuwa wavuvi wake wameendelezwa kwa mujibu wa taratibu ambazo serikali hii ya awamu ya saba imeandaa.

Pia kuhusu wavuvi wangapi ambao wamekamatwa na kuchukuliwa hatua ni kwamba tangu sheria hii Nam. 7 ya mwaka 2010 iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi ni kwamba wavuvi 12 walikamatwa na kupelekwa Mahakamani katika Mahakama ya Mkoa wa Kusini Unguja na tayari wameshadhibiwa na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, nakushukuru sana kunipatia nafasi hii katika majibu yake mama Mhe. Waziri alisema kwamba wizara yake imetoa karibu shilingi bilioni 2.2 kwa ajili ya kuwasaidia wavuvi hawa. Je, wizara yake imefuatilia kuona kwamba wanapata maendeleo ya kuweza kukidhi mahitaji yao.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, ni kweli fedha iliyotoka ni nyingi na imetolewa na serikali kwa lengo la kuwaendeleza wavuvi na bado wizara yangu kwa kuungwa mkono na serikali hii ya awamu ya saba bado imo mbioni kuona kuwa fedha nyingi zaidi zinatoka kuwapelekea wananchi na wavuvi ili kuona wanavua katika kiwango ambacho kitatoa tija zaidi.

Kwa hivyo, fedha ambayo imetoka katika vikundi kwenye shehia zetu Unguja na Pemba zimekwenda kwa wavuvi na sisi katika wizara tumejiridhisha kwamba zinafanya kazi vizuri. Moja katika eneo ambalo tunaona kuwa fedha hii inafanya kazi vizuri ni kwamba takwimu zinaonesha kabla ya kutolewa fedha hizi upatikanaji wa samaki katika visiwa vyetu ulikuwa kwa mwaka ni wastani wa tani 16,000. Lakini hadi mwishoni mwaka 2010 basi uzalishaji wa samaki umefika tani 24,000 kwa mwaka.

Kwa hivyo, hii Mhe. Spika, ni ushahidi wa wazi kuona kwamba fedha ambayo imepelekwa kwa wananchi kwa kweli imefanya kazi vizuri na tunaamini kwamba kadri ambavyo tutakwenda basi tuna lengo kuwa tufike kiwango kikubwa zaidi.

Nam. 133

Idara ya Uvuvi

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) – Aliuliza:-

Hapo zamani kulikuwa na Mashirika mengi ya Serikali. Moja kati ya hayo ni Shirika la Uvuvi baadae likawa ni Idara ya Uvuvi.

(a) Je, idara hiyo bado ipo.

(b) Na kama ipo shughuli zake ni zipi.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 133 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli hapo zamani lilikuwepo Shirika la Uvuvi ambalo lilikuwa likijitegemea kama Mashirika mengine na pia ilikuwepo Idara ya Uvuvi. Shirika la Uvuvi baada ya kushindwa kujiendesha lilibinafsishwa na Serikali mnamo mwaka 2004. Idara ya Uvuvi bado ipo na ina jukumu la kusimamia mambo yote ya sekta ya uvuvi chini ya Sheria mpya ya Uvuvi Nam. 7 mwaka 2010, ambayo ni pamoja yake ni pamoja na:-

- Kuinua, kuendeleza na kudhibiti kwa madhumuni ya kusimamia shughuli zote za uvuvi wa kienyeji na viwanda.
- Kujenga uwezo kwa ajili ya usimamizi madhubuti kwa shughuli za uvuvi.
- Kuelimisha na kuinua kuelewa shughuli za uvuvi.
- Kushajiisha matumizi endelevu ya rasilimali za habari
- Kuongeza thamani ya mazao ya bahari na soko
- Kufanya utafiti wa kisayansi kwa ajili ya usimamizi mzuri wa shughuli za uvuvi.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando): Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niulize swali la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Kwanza nilikuwa nataka kujua kulikuwa kuna boti zile za uvuvi katika idara hii hivyo ziko wapi au kama zipo zinafanya kazi gani kwa sasa.

b) Kulikuwa kuna mtambo wa kuzalisha barafu za mapande makubwa na zile za chenge, nataka kujua shughuli zile kama zinaendelea au zimekufa.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, nilipokuwa najibu katika swali mama nilisema kwamba shirika hili lilishindwa kujiendesha na serikali mwaka 2004 ikaamua kulibinafsisha. Kwa hivyo, unapolibinafsisha shirika hubinafsishi jina tu, unabinasisha jina na mali yake. Kwa hivyo, kama kulikuwa na boti zilibinafsishwa, kama kulikuwa na mtambo wa barafu nao ulibinasishwa, lakini Mhe. Spika, yote kwa sababu yameshindwa kujiendesha boti zimekufa ukifika pale utaziona zimeharibika na mtambo nao pia haufanyi tena kazi.

Nam. 45

Wananchi Kuchangia Huduma za Afya

Mhe. Omar Ali Shehe - Aliuliza:-

Kufuatia Mapinduzi matukufu ya 1964, Serikali ilitangaza kutoa huduma bure za matibabu ya kwa wananchi wote. Ingawa hadi sasa tunaendelea kudumisha Mapinduzi hayo, Serikali katika miaka ya karibuni iliidhinisha mpango wa uchangiaji wa huduma za afya.

(a) Je, ni huduma zipi zinazotakiwa kuchangiwa na wananchi na ni huduma zipi zenye kuchangiwa na Serikali.

(b) Je, Serikali haioni kuwa kitendo cha kuchangia huduma za afya kwa wananchi wasio na uwezo ni kwenda kinyume na adhma ya Mapinduzi Matukufu ya 1964.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 45 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake naomba kwanza uniruhusu kutoa maelezo yafuatayo:

Mhe. Spika, mnamo miaka ya 90 gharama za uendeshaji wa huduma za afya zimekuwa zikiongezeka kwa kasi kubwa na haikulingana na fedha ambazo wizara imekuwa ikizipokea kutoka Serikalini. Zipo sababu kadhaa zilizopelekea kuongezeka kwa gharama hizo ambazo ni pamoja na:-

- Kuongezeka kwa idadi ya watu nchini ambapo hakukulingana na ukuaji wa uchumi wa nchi.
- Kupanda kwa bei za bidhaa na huduma za matibabu.
- Kuibuka kwa maradhi mapya na kuongezeka kwa maradhi ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza

Aidha, hali hii ya kukosekana fedha za kutosha za kuendesha huduma hizi kulipelekea kiwango cha utoaji wa huduma bora kudidimia siku hadi siku na baadhi ya huduma kushindakana kutolewa.

Mhe. Spika, ili kukabiliana na hali hiyo, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilipitisha Sera ya Kuchangia Huduma za Afya, ili kufanikisha upatikanaji wa huduma hizo.

(a) Huduma ambazo kwa sasa zinazotakiwa kuchangiwa ni zile zinazotolewa katika hospitali mbali mbali isipokuwa vituo vya Afya hivyo havipaswi kuchangia na huduma zenyewe ni:-

- Huduma za uchunguzi wa maradhi (huduma za maabara, *X-Ray, Ultrasound* na *CT – Scan*)
- Huduma za matatibabu meno na upasuaji mdogo na mkubwa.
- Pia katika baadhi ya hospitali – huduma kama vile masikio, pua, koo na macho pia huchangiwa.

Kwa upande wa Serikali, napenda kumjulisha Mhe. Mwakilishi na wananchi wote kwamba, Serikali haichangii huduma za afya bali ni wajibu wake kugharamia huduma hizo kwa wananchi wake wote.

(b) Mhe. Spika, Wizara ya Afya kupitia hospitali husika imeweka utaratibu maalum wa kuhakikisha wale wote wasio na uwezo hawakoseshwi huduma za afya. Aidha, itakumbuka kwamba nilieleza kwa ufasaha nilipokuwa nikijibu swali Nam. 37 (c) kwamba kutakuwa na utaratibu maalum wa misamaha kwa wale watakaobainika hawana uwezo.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa suala la kuchangia huduma za afya kwa sasa ni kitu cha kawaida katika hospitali zetu, kitu ambacho ni chanzo kikubwa cha rushwa.

a) Je, serikali iko tayari kutoa warka wenye kuelezea huduma ambazo wananchi wanapaswa kuchangia pamoja na viwango vyake.

b) Ili ionekane kuwa michango hiyo ya wananchi ni sehemu ya mapato ya serikali. Je, wizara iko tayari kusambaza risiti katika hospitali ili kila anayechangia apewe risiti.

c) Ni nini mpango wa serikali wa kuwasaidia wazee wasiojiweza katika kupata huduma ya matibabu bila ya kuchangia.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, katika sentensi yangu ya mwisho ya jibu (b) nimesema kwamba sisi tumo katika maandalizi ya kuhakikisha kwamba huduma za afya zinazolipiwa zianishwe, zitangazwe na pia watu wote wafahamu. Huduma zenyewe nilizosema ambazo zitachangiwa ni hizo nilizozitaja hapo juu hizo ndizo zitakazochangiwa. Mhe. Spika, mpaka dakika hii miongozo ilikuwa haijaandaliwa kwa hiyo sasa hivi tunaandaa miongozo hiyo ambayo itaanisha ni kiasi gani kinacholipwa, nani atalipa, nani atasamehewa wakiwemo hao wazee wasiojiweza na wale wote ambao watakuwa wanastahiki kwamba wasilipe pia nao hawatalipa.

Mhe. Spika, kuhusu suala la risiti tumeshakubaliana na Wizara ya Fedha watatuletea wafanyakazi kutoka kwao ambao wamesoma na wana taaluma na kutakuwa na *point* maalum ambapo watu wote watakwenda kulipia na kupewa risiti ambayo wataipeleka kunakotolewa huduma. Kwa hivyo, anayetoa huduma hatakuwa anapokea pesa isipokuwa anapokea risiti na anatimiza wajibu wake.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru sana kunipa fursa na mimi kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, pamoja na utaratibu huo wa kulipia ambao serikali inasema ni kuchangia, lakini je, kuna watu ambao wanakuja aidha wanapata matatizo ya ghafla kwa mfano ukiachana na mtu anayepata ajali lakini kwa mfano mtu amepata ngiri ya ghafla au matatizo mengine. Je, watu kama hao wizara yako ina mpango gani wa kuwasaidia ikawa hawachangii.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwanza serikali kusema kwamba kulipia ndio kuchangia ni vitu viwili tofauti naomba ufahamu hivyo. Unapolipia unalipa jumla ya kila kitu, lakini ukichangia unachangia baadhi ya sehemu ya kile ambacho kinachohudumiwa. Kwa mfano, ukenda ukizaa kwa bahati mbaya ukibidi kupasuliwa anatakiwa kuchangia shilingi elfu arubaini, lakini gharama ya upasuaji huu ni shilingi laki moja na hamsini. Kwa hivyo, kutoa shilingi elfu arubaini unachangia hulipii, na serikali inawajibika kuulipia wewe shilingi laki moja na elfu kumi kwa sababu huo ni wajibu wake kuhakikisha kwamba wewe unapata huduma au mke wako anapata huduma.

Mhe. Spika, kwa mfano yametokea maradhi ya ghafla au imetokea ajali, nafikiri hata Wizara ya Afya tunao wafanyakazi sisi ni binadamu mtu hawi anapapatika anakufa ukamwambia lete pesa, tunamuhudumia mengine yatafuata baadae.

Nam. 72

Kumalizika kwa Jengo la Kituo cha Afya Kojani

Mhe. Hassan Hamad Omar – Aliuliza:-

Tangu kujengwa kwa Kituo cha Afya kisiwani Kojani ni mwaka mmoja na nusu sasa halijakamilika. Kwa sasa huduma ya afya inatolewa katika nyumba iliyojengwa kwa msaada wa *TASAF* kwa ajili ya kuishi madaktari ambapo inasababisha msongamano wa wagonjwa kwa sababu sehemu hiyo ni finyu.

(a) Mhe. Waziri, jengo hilo la Kituo cha Afya kisiwani Kojani linatarajiwa kumalizika lini na kuanza kazi.

(b) Kwa sababu kituo hicho kina upungufu wa madaktari, wizara ina mpango gani wa kuongeza daktari ili kuondoa usumbufu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwanza naomba radhi kwa usumbufu uliojitokeza. Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 72 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba, ni muda mrefu sasa ujenzi wa Kituo cha Kojani haujamalizika. Mimi binafsi nilikwenda Pemba na kujionea mwenyewe hali halisi ilivyo. Msongamano wa wagonjwa katika sehemu inayotumika kwa hivi sasa (katika nyumba ya *staff*) kweli unakuwepo hasa nyakati za asubuhi.

Mhe. Spika, ujenzi wa Kituo cha Kojani ni mkubwa, kituo tumekijenga upya kwani kilichokuwapo kabla kilikuwa kichakavu mno na hakikuwa kikikidhi haja. Ilibidi mkandarasi aanze na kazi ya kubomoa (*demolishing*). Hiki ni kituo cha daraja la pili (*PHCU + 2nd line dispensary*) ni kituo ambacho kinatoa huduma karibu zote zinazotakiwa, zifanyike kwenye kituo mbali ya zile huduma za msingi. Kwa hivyo, meno, madawa na vyengine vyote vinakuwemo humo, na ujenzi wake ni kama ule wa Kengeja na Konde.

Kuchelewa kwa ujenzi huu kumetokana na sababu nyingi huko Pemba. Aidha, Kojani ni kisiwa na inabidi vifaa vyote kuvushwa kutoka ng'ambo ya pili, hii nayo ilipelekea kuchelewa kufika kwa vifaa vingi muhimu hasa ikizingatiwa kuwa mkandarasi alikuwa na kazi za ujenzi huo zaidi ya sehemu (*sites*) 23 zilizojumuisha pia ujenzi wa nyumba za '*staff*' sehemu mbali mbali za Pemba. Kuna baadhi ya wakati upatikanaji wa fedha pia ulichelewa kidogo, kutokana na akutokamilika kwa taratibu za mkandarasi zinazotakiwa kwenda sambamba na '*procedures'* zilizowekwa na Mfadhili *ADB.*

(a) Mhe. Spika, kwa sasa hali ya ujenzi huu unaendelea vizuri na uko katika awamu ya mwisho. Tumekualiana na Mkandarasi akabidhi kazi hiyo mwezi May, 2011. Vifaa vyote vya kutolea huduma vimeshafika na tumevihifadhi katika Bohari ya Madawa iliyopo Wete. Mara tu tutakapokabidhiwa tutaviingiza na hali ya huduma kituoni hapo itaanza kutolewa mwezi wa Juni, 2011.

(b) Kuhusu upungufu wa wafanyakazi kituoni hapo, wizara imeandaa mpango mahsusi kwa ajili ya kuimarisha huduma katika vituo hivi vya daraja la pili (*PHCU+*). Wizara itahakikisha kuna wafanyakazi na vitendea kazi vya kutosha. Taratibu za uajiri wa wafanyakazi wapya zinakamilishwa na baadhi yao watapelekwa Kojani. Nataka kumuahidi Mhe. Mwakilishi wa wananchi wa Kojani kwa ujumla wataona mabadiliko wakati wa ufunguzi rasmi wa kituo hicho.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa sababu Kojani ni kisiwa na ni kisiwa kinachoishi watu wengi, daktari anayetoa huduma ni mmoja na akimaliza muda wake wa kazi kwa siku si mkaazi wa kisiwani Kojani anaondoka. Kwa hivyo, yanatokea matatizo usiku na tunalazimika kuwavusha wagonjwa usiku na kukimbilia Hospitali ya Wete na Chake Chake jambo ambalo ni usumbufu mkubwa.

Je, Mhe. Naibu Waziri ni lini tutakuwa na daktari anayekaa pale kisiwani Kojani na kutoa huduma masaa 24.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwenye jibu (b) nimesema kwamba tukimaliza kituo kwa kuwa ni kituo cha daraja la pili kina idadi ya wafanyakazi wake wanaokubalika na kwa sasa hivi madhali nyumba ya kukaa watu ipo na kituo kitakuwa kimemalizika, basi kituo kitafanya kazi na nyumba itakaa wafanyakazi. Sasa hivi kwanza inashindikana wafanyakazi kukaa pale kwa sababu hiyo nyumba ya kufanyia kazi ndio kituo chenyewe. Kwa hivyo, sasa hatuwezi tukafanya kazi humo humo tukalala humo humo, tumechukua *option* ya kufanyia ile nyumba kazi halafu mtu anarudi anakwenda kulala kwake.

Bahati mbaya iliyoko Pemba wafanyakazi wengi wanafanya kazi kwa kufuatilia wagonjwa, na moja katika sehemu ambayo inafatilia wagonjwa kwa sababu hiyo ninayokwambia kwamba, nyumba ambayo ilikuwa anapaswa mfanyakazi kukaa ndio inayofanyiwa kazi na inabidi yule anayefanya kazi katika kituo kile atoke nje ya Kisiwa kile cha Kojani. Kwa hivyo, anakuja pale anafanya kazi na kurudi. Sasa tutakapomaliza kazi, kituo kikifunguliwa na nyumba ikiwa tupu wafanyakazi wataletwa kwa sababu tunajiandaa kwa hilo, watakpoletwa nyumba ya kulala ipo watalala pale na kituo kiko chini ya pua hivyo akifunua tu mdomo au mkono tayari kaingia kituoni unahudumiwa.

Nimepaangalia Kojani si pa kubwa hata hivyo, ingawa watu ni wengi. Kwa hivyo, nafikiri pale mambo yake yatakuwa *supper* kuliko sehemu nyengine yoyote katika visiwa vyetu viwili hivi.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa tena fursa ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu sababu moja ya kuchelewesha jengo alisema ni sababu ya mvua ambazo zilikuwa zinanyesha na kuwa nyingi na sababu nyengine ambazo amezieleza. Lakini kwa kuwa Kojani ni kisiwa na kama alivyozungumza Mhe. Mwakilishi watu wa kisiwani wanakuwa na shida ya kuvuka na kurudi na kwenda tena, kwa kuwa sasa hivi tunategemea mvua za masika tayari zinaanza na wakati wowote zitakuwa nyingi.

Je, wizara yake imejipanga vipi kusimamia mkandarasi ili isije ikatokea tena sababu ya mvua kabla ya kumalizika kujenga.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, suala la mvua si la Wizara ya Afya wala Mkandarasi, Mwenyezi Mungu anapanga na sisi tunapotea. Mkandarasi anajitahidi kwa kadiri ya uwezo wake na Kojani kama hivyo unavyosema sio tu wananchi kusafiri ni shida, kusafirisha vyombo ni shida zaidi. Mimi mwenyewe pale kusaifiri mpaka nimekwenda kule nimerudi nikajiuliza hivi

vitu vinasafirishwaje kama usafiri wenyewe ndio huu? Lakini mkandarasi anajitahidi na nimesema nyumba iko katika sehemu ya *finishing*. Nina imani mkandarasi tuliyenaye tunamuamini atajitahidi kwa kadiri itakavyowezekana, lakini tena mvua ikinyesha tumwachie Mungu itakapokwisha tutafanya kazi.

Nam. 12

Uanzishwaji wa Taasisi ya Usafirishaji Zanzibar

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa - Aliuliza:-

Mnamo miaka ya 2003/2004 Zanzibar ilifanya shughuli za usafirishaji wa abiria na mizigo kwa kushirikiana na Taasisi ya *T.C.F.B*. Baadae taasisi hii ikaonekana haisaidii Zanzibar katika shughuli hizo ipasavyo na kupelekea kuzuiliwa kufanya kazi. Kutokana na sababu hiyo, ilipendekezwa kuanzishwa taasisi kama hiyo kwa muda maalum hapa Zanzibar.

Je, Mhe. Waziri suala hili limefikia wapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 12 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia wizara yangu iliahidi kuanzisha chombo kitakachofanya kazi ambazo hapo awali zilikuwa zikifanywa na chombo cha *TCFB* baada ya taasisi hiyo kusitishwa kufanyakazi zake hapa Zanzibar mwaka 2003/2004.

Naomba kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa chombo hicho kimeundwa chini ya wizara yangu ambacho kinaitwa Mamlaka ya Kusimamia Usafiri wa Bahari Zanzibar (*Zanzibar Maritime Transport Authority*), ambacho kinasimamia masuala ya usalama baharini pamoja na udhibiti wa biashara ya usalama wa baharini. Mamlaka hii imeanzishwa kwa Sheria Nam. 3 ya mwaka 2009.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri lakini ni kweli kwamba tulikuwa na chombo hiki cha *TCFB* ambacho kwa sasa tunaweza kukiita kwamba ni *SUMATRA*, kilikuweko Zanzibar na kikifanya shughuli zake kwa sababu ya kuwasaidia wananchi wa Zanzibar. Baada ya kuonekana kwamba chombo hiki hakiwasaidii Wazanzibari, badala yake kinawasababishia hasara zaidi katika kufanya biashara zao, kwa sababu malengo makuu ya chombo hiki ilikuwa ni kusaidia wafanyabiashara wanaokwenda kununua bidhaa zao nje ili zile meli

zinazoleta mizigo ziwa-*charge charge* amabzo zinakuwa na maslahi kwao na wananchi kwa ujumla. Lakini ikaonekana kwamba, chombo hiki hakisimamii shughuli hiyo na wafanyabiashara wanalipa pesa nyingi kuliko taratibu zinavyoelekeza.

Sasa basi, Mhe. Spika, baada ya kwishakutolewa maelekezo kwamba chombo hiki kingine kiundwe kwa upande wa Zanzibar na kile kuondoshwa. Je, utaratibu gani wa sheria ambao utatumika katika kuhakikisha kwamba wafanyabiashara ambao watakuwa wanaleta biashara zao Zanzibar wanalipa kiwango sahihi cha *freight* na kuondokana na ule utaratibu ambao ulikuwa ukifanywa na ndugu zetu hawa wa *SUMATRA.*

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, chombo cha *TCFB* madhumuni yake makubwa ni kupokea malalamiko ya wafanyabiashara pale ambapo kodi waliyotozwa imekuwa ni kubwa kuliko matarajio au maelekezo husika. Mhe. Spika, chombo hiki kama alivyoeleza Mhe. Mwakilishi kilikuwa kinaleta utata na malalamiko na ndio yaliyopelekea chombo hiki kufutwa.

Baada ya kufutwa chombo hiki, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanzisha mamlaka mapya ya *Zanzibar Maritime Authority* ya sheria Nam. 3 ya mwaka 2009. chombo hiki ndicho kinachosimamia masuala ya usalama na biashara ya masuala ya baharini. Katika chombo hiki kuna kitengo maalum chenye kuhusiana na taratibu hizo za ushuru na mengineyo.

Nam. 105

Mitambo Inayotumiwa na Vyombo vya Habari vya Serikali (TVZ/STZ)

Mhe. Ali Salum Haji – Aliuliza:-

Kwa kuwa kuna azimio la Kimataifa linalovitaka vyombo vya habari kuachana na mitambo ya analogy na badala yake kutumia mitambo ya digital kabla ya 2012.

Na kwa kuwa mitambo inayotumiwa na vyombo vya habari vya serikali yaani *TVZ* na STZ bado vipo katika mfumo wa *analogy*. Pia mitambo hiyo ni chakavu na ya zamani kiasi ambacho hivi sasa baadhi ya vipuri vyake havipatikani tena. Na kwa kuwa Zanzibar huridhia maazimio yote ya kimataifa.

(a) Je, ni lini vyombo hivi vya serikali vitapatiwa mitambo ya *digital*.

(b) Na endapo ikafika 2012 mitambo ya *digital* ikwa haijapatikana, serikali haioni kuwa inakwenda kinyume na azimio la kimataifa ambalo imeridhia.

(c) Maktaba ya *TVZ* imejaa vipindi vizuri vya zamani vya kuelimisha, lakini vipindi hivyo vimerekodiwa katika kaseti za *emetic* na *bet amax*, na *super VHS* ambazo hivi sasa mashine za kuchezea kaseti hizo zimekufa. Je, lini wizara itanunua mashine hizo ili vipindi viendelee kuonekana na pia kuhamishiwa katika njia ya kisasa ya *DVD*.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 105 lenye vifungu (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Shirika la Kimataifa la Mawasiliano (*ITU*) limeagiza hadi mwaka 2015 kuwa televisheni zote ziachane na mitambo ya '*analogy'* na badala yake kutumia mitambo ya *digital*. Katika kulitekeleza hilo, baadhi ya televisheni katika ukanda wa Afrika Mashariki wamejiwekea malengo ya kuanza zoezi hilo mwaka 2012. Kuanza huko mapema kuna hasara zake na faida zake. Kwa mfano, kama linatokea tatizo lolote bila ya maingiliano huyu mwenye mawasiliano ya *digital* atakosa kinga kwani kipindi kilichowekwa na *ITU* bado hakijafikia.

Wakati nchi za Afrika Mashariki tulielekezwa kutumia *format* ya *DBB*, kuna nchi pamoja na vituo vya televisheni tayari vimeshawekeza katika mfumo huo. Ni hivi karibuni tu tayari mfumo mwengine mpya ulio bora ushazinduliwa ambao ni *DBB ITU*. TVZ ambayo tayari mitambo yako iko kiwandani imebidi kusitisha na kufanya mabadiliko haya.

(a) Zoezi hilo tayari limeshaanza na linaendelea. Limeanza kwa kuagiza mitambo pamoja na vifaa vya studio.

(b) Azimio la Kimataifa linatakiwa kutekelezwa ifikapo mwaka 2015 na sio mwaka 2012. ni matakwa binafsi ya baadhi ya nchi na tv katika ukanda wa Afrika Mashariki.

(c) Upo mpango mzima wa utaratibu wa uhamishaji wa vipindi vyote kuwekwa katika *'filke format'* huu ndio mpango wa kisasa wa kuhifadhi kumbukumbu zote katika *'Server System'* na badala ya kuwa na mkataba tunaweka *archive*. Katika mpango huu TVZ inapatiwa mafunzo kupitia *CFI*

(Canal France International) na yatakapokamilika, basi kumbukumbu zote zitahifadhiwa katika *archives* ifahamike kwamba twendako kaseti zinaondoka.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Spika, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, katika suala la (c) hapa kumetajwa juu ya kuwepo kwa vipindi vingi katika mifumo hii ya kizamani. Kuna taarifa Mhe. Spika, kwamba studio za TVZ zimekuwa zikishuhudia upotevu wa vifaa vyake vingi ikiwemo kaseti katika mazingira ambayo hayaeleweki.

Je, Mhe. Waziri anazo taarifa hizi? Kama anazo amechukua hatua gani ili kunusuru hifadhi ile ya taifa ambayo imejaa historia ya nchi yetu kutokana na vipindi vingi vilivyoanza tokea studio hizi zilipoanzishwa mwaka 1972.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, samahani naomba arejee kidogo hilo swali.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, nasema katika swali mama kifungu (c) kumeuliziwa juu ya vifaa mbali mbali hasa vipindi vya TVZ ambavyo vipo katika ile mifumo ya kizamani iliyotajwa pale. Ziko taarifa kwamba katika studio za TVZ kumekuwa na upotevu wa vifaa vile vya zamani vikiwemo mbali ya vyengine na vifaa hivi vyenye kanda na kaseti nyengine ambavyo vimejaa historia yetu.

Sasa namuuliza Mhe. Waziri kwamba anazo taarifa hizi? Kama anazo wizara inachukua hatua gani ili kunusuru hali hii ili visiendelee kupotea hasa ikizingatiwa hizi ni ***turathi*** za kitaifa kwa nchi yetu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwa kweli taarifa ninayo na nimeshatembelea katika jengo hilo na nimeona hali halisi. Ni kweli kwamba hali si shuwari, lakini pamoja na hayo kama nilivyoeleza awali kwamba, tuko katika hatua ya kuleta vifaa vipya na vile vile kulifanyia ukarabati lile jengo lenyewe na hususan katika ile *AC System* kwa kweli zote naweza kusema ni *right off*.

Kwa hivyo, nayo tuko katika hatua ya kuifanyia ukarabati ili kuhakikisha kwamba vifaa vinavyokuja vitakuwa *very sensitive*. Kwa hivyo, ni lazima tuvihifadhi kama nilivyotangulia awali kwamba, hakuna kaseti kutakuwa na vitu vyengine kabisa ambavyo vitakuwa *more sensitive* na vitahitaji utunzaji wa hali ya juu. Kwa hivyo, hiyo hatua iko mbioni Mheshimiwa naomba uwe na subira kidogo.

Mhe.Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, Mhe. Waziri anasema kwamba taarifa za upotevu wa baadhi ya vifaa na vipindi kwenye *archive* ya *TVZ* anayo. Na amekiri kwamba hali si shuwari. Je, anakusudia kutwambia kwamba, baadhi ya watendaji wake sio waaminifu na ndio ambao wanaiba vitu hivyo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nakubali kwamba kuna baadhi ya wafanyakazi sio waaminifu. Suala hilo nalifuatilia kwa karibu sana na wale wote ambao wamehusika kwa njia moja au nyengine na upotevu huo basi hatua itafuata.

Nam. 70

Matokeo ya Mtihani wa Darasa la Saba Mwaka 2011

Mhe. Hassan Hamad Omar - Aliuliza:-

Matokeo ya mitihani ya wanafunzi wa darasa la saba yaliyotolewa Februari 2011 yalikuwa ni mabaya sana hasa kwa Skuli za Vijijini ukiliganisha na Mijini. Kwa mfano, Skuli ya Jojo, Mchanga Mdogo katika Jimbo la Kojani, kati ya wanafunzi 88 alifaulu mmoja (1). Skuli ya Kojani kati ya 92 hakufaulu hata mmoja. Skuli ya Chwale kati ya 84 hakufaulu hata mmoja.

(a) Mhe. Waziri, wizara imechukua hatua gani za kutaka kujua sababu za msingi za matokeo hayo mabaya.

(b) Wizara imejipanga vipi katika kukabiliana na tatizo hilo, ukizingatia kwamba wengi wa wanafunzi hawa ndio wanaofeli Kidato cha Pili *(Form II)* na kubaki mitaani.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Nakushukuru Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 70 lenye vifungu (a) na (b) kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, kwanza naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Matokeo ya wanafunzi wa darasa la saba mwaka 2010 kuingia Kidato cha Kwanza mwaka 2011, yameonesha kuwa kati ya wanafunzi 23,269 waliofanya mitihani. Wanafunzi 18,908 walifaulu mtihani wao na kuchaguliwa kuingia Kidato cha Kwanza ikiwa ni sawa na asilimia 81.2 ya watahiniwa wote. Asilimia hio ya kufaulu ni nzuri.

Kwa skuli ya Mchanga Mdogo kati ya wanafunzi 166 waliofanya mtihani wa darasa la saba waliofaulu ni wanafunzi 122 sawa na asilimia 75.9 ya watahiniwa wote walifaulu na kuchaguliwa kuingia kidato cha kwanza. Katika Skuli ya Kojani kati ya wanafunzi 88 waliofanya mtihani wanafunzi 55 walifaulu sawa na asilimia 62.5 na walichaguliwa kuingia Kidato cha Kwanza.

Katika Skuli ya Chwale kati ya wanafunzi 86 waliofanya mtihani, wanafunzi 82 sawa na asilimia 95.3 walifaulu na kuchaguliwa kuingia kidato cha Tano. Hata hivyo, katika skuli hizo ni kweli kwamba wanafunzi waliopata alama za kuchaguliwa kuingia madarasa ya mchepuo ni ndogo sana, kwani ni Skuli ya Mchanga Mdogo tu ndio waliopata wanafunzi watatu na wala sio mmoja kama swali lilivyosema kujiunga katika darasa la mchepuo.

Wanafunzi kutochaguliwa kuingia katika madarasa ya mchepuo haimaanishi kuwa wamefeli. Pia hali ya kufaulu kwa wanafunzi wa skuli za vijijini haitofautiani sana na skuli za mjini. Skuli za Wilaya ya Micheweni zimekuwa zikifanya vizuri katika mitihani yao mara nyingi. Hata hivyo, ziko baadhi ya skuli chache ambazo matokeo yake ni ya kiwango cha chini ukilinganisha na skuli nyengine.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, matokeo ya darasa la saba hayakuwa mabaya kama inavyodhaniwa, kwani wanafunzi wengi wamechaguliwa kuingia kidato cha kwanza. Hata hivyo, kuna haja ya walimu na wanafunzi kutoridhika na matokeo hayo na kufanya bidii ili waweze kupata matokeo mazuri zaidi.

(b) Mhe. Spika, katika kuhakikisha kuwa matokeo ya mtihani wa darasa la saba yanakuwa mazuri zaidi na elimu ya msingi inaimarika, wizara imeimarisha mafunzo ya uwalimu kazini kupitia vituo vya walimu, inaendelea kuimarisha mazingira ya skuli na inakusudia kufanya mapitio ya muundo wa utumishi wa walimu. Aidha kupitia mradi mpya wa *"21st Century Basic Education"*, wizara itazipatia kompyuta na *internet* skuli zote za msingi na kuzitumia kama ni kifaa muhimu cha kufundishia.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na takwimu sahihi tena *latest* tulizozipata. Lakini mimi swali langu ni kwamba, pamoja na matokeo mazuri kama Mhe. Naibu Waziri alivyoeleza, lakini ukiangalia katika matokeo yalipotajwa katika mwaka

huu skuli kama vile ya Mitiulaya, Kizimbani, Jadida, skuli hizi zilitoa watoto wengi tu wa darasa la saba kuingia katika michepuo. Lakini skuli alizozitaja Mheshimiwa aliyeuliza swali na skuli yangu ya Uondwe haikutoa hata mtoto mmoja.

Hiki kigezo cha watoto skuli moja kutoa wengi wakaingia katika michepuo na skuli nyengine darasa la saba wakafanya mitihani wengi asitoke hata mmoja si kuonesha kuwa elimu katika skuli hizo imeanguka kweli? Tukiachilia mbali kutoka pale pale akaingia *Form I* pale pale. Kwa sababu toka zamani Mheshimiwa aliyekuwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali na nampongeza aliiweka hali hiyo ili watu wote wapate elimu mpaka madarasa ya kumi na mbili.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, wanafunzi kupasi michepuo kama nilivyosema katika jibu langu mama si kufeli kwa mwanafunzi, vile ni vipaji maalum vya wanafunzi. Hii Mhe. Spika, inapatikana kwa mashirikiano kati ya wazazi, kamati ya wazazi, walimu na wanafunzi. Skuli ambazo Mhe. Mwakilishi amezitaja ni kweli, lakini skuli hizi ukichunguza kwa undani kabisa unaona ni namna gani ya mashirikiano yao wanayofanya kati ya skuli, wanafunzi na wazazi. Wawakilishi wao na wabunge wanawasaidia sana skuli hizi kuhakikisha kama wanafanya vizuri. Ni kweli kwa mfano Skuli ya Mitiulaya imetoa watoto wa michepuo darasa zima wanafunzi 40. Lakini walifanya kazi ya ziada Mhe. Spika, walikuwa hawalali mchana wala usiku kuhakikisha kama wanapasisha wanafunzi wengi.

Mhe. Spika, natoa wito kwa Baraza lako tukufu tushirikiane Waheshimiwa Wawakilishi katika kuhakikisha wanafunzi wetu skuli ambazo tunazo katika majimbo yetu tunashirikiana kwa hali na mali wazee, wanafunzi na walimu kuhakikisha kama tunafanya vizuri.

Muongozo wa Spika

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, kanuni ya 48 na 49 naomba muongozo wako. Mhe. Spika, kanuni ya 48 fasili ya (1) inasema “Bila ya kuathiri masharti ya katiba au kanuni hizi mjumbe yeyote anaweza kupendekeza jambo lolote lijadiliwe katika Baraza kwa kutoa hoja, yaani kwa kutoa pendekezo lililokamilika na liwe limewekwa katika hali inayoweza kueleza uamuzi wa Baraza.

Kanuni ya 49 fasili ya (1) na ya (2) inasema “Isipokuwa kama kanuni hizi zitaruhusu vyenginevyo au kwa idhini ya Spika na kibali cha wajumbe wengi waliohudhuria. Hoja yoyote haitatolewa katika Baraza mpaka taarifa ya hoja

iwe imetolewa na kupokelewa angalau siku mbili kabla ya kikao ambapo hoja hiyo inakusudiwa kutolewa.

Fasili ya (2) inasema "Iwapo kwa mujibu wa kanuni hizi taarifa ya hoja inatakiwa kutolewa, basi taarifa hiyo itabidi itolewe kwa maandishi itiwe saini na mjumbe anayetoa na ipelekwe kwa Katibu ili aipokee kufuatana na masharti ya fasili ya (1) ya kanuni hii."

Muongozo ninaouomba kutoka kwako Mhe. Spika, ni kwamba iwapo hoja imetimiza masharti haya na imewasilishwa nini hatua inayofuata. Mhe. Spika, naliuliza hili kwa sababu nimewasilisha hoja tangu tarehe 23 lakini hadi hii leo sijapata maelekezo yoyote kutoka katika Afisi ya Baraza la Wawakilishi. Naomba muongozo wako Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe anachosema Mhe. Ismail Jussa Ladhu kinahusiana na hoja ambayo yeye aliituma kupitia kwa Katibu kama taratibu za kanuni zinavyohitaji. Hoja ilikuwa ni kubwa inahitaji kutafakari vizuri jambo ambalo limenichukua muda baada ya Katibu kuniwasilishia hoja ile kuitafakari hoja hiyo. Nilitegemea kwamba jibu la hoja hii angelipata jana, kwa bahati mbaya nilikuwa na dharura sikufika kwa sababu ya kuuguliwa, lakini leo nimejitahidi nifike na si muda mkubwa leo hii jibu hilo litapatikana.

Nataka nikiri kwamba imechukua muda mkubwa, lakini huwezi ukaenda haraka haraka kwenye mambo ambayo ni mazito na muhimu kuyatafakari, inabidi lazima ichukue muda katika kutafakari na kutoa wajibu sahihi. Huwezi tu ukavurumisha kwa sababu Mhe. Mjumbe ana nafasi yake kama mjumbe na ana haki zake katika Baraza hili, sasa jibu unalotoa lazima liwe na heshima ya Mhe. Mjumbe kama vile yeye alivyoleta kwa mujibu wa kanuni na kwa heshima zote.

Sasa kwa heshima kabisa Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwanza niombe radhi kwamba imechukua muda mkubwa, lakini pili utapata majibu ambayo ukiyaangalia nafikiri na wewe utazingatia na utaona umuhimu na uzito uliokuwepo kiasi cha kuchukua muda mrefu huo kupata majibu hayo. Nahakikisha kwamba majibu hayo yatatoka leo. Ahsante sana.

HOJA ZA KAMATI

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa

Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa: (Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi): Mhe. Spika, awali ya yote naomba nichukue fursa hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia

kukutana hapa kwa mara nyengine tena ili kujadili ripoti za Kamati za Baraza kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, pili naomba nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu, Muhtasari wa Ripoti ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa juu ya utekelezaji wa kazi za kawaida na kazi za maendeleo kuanzia Julai hadi Disemba, 2010.

Mhe. Spika, napenda kumpongeza kwa dhati Mhe. Dk. Ali Mohammed Shein kwa kuchaguliwa na wananchi wa Zanzibar kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Aidha, kamati inawapongeza kwa dhati viongozi mbali mbali waliochaguliwa na wananchi na wale walioteuliwa kushika nyadhifa mbali mbali Serikalini.

Mhe. Spika, kamati yetu kwa mwaka wa fedha wa 2010-2011 ilianza shughuli zake za kufuatilia utekelezaji wa kazi za kawaida na zile za maendeleo za ofisi zifuatazo za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar:

1. Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar.
2. Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, na
3. Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Kamati hii ilifanya kazi zake kwa muda wa wiki nne kwa utaratibu ufuatao:

i. Unguja kuanzia tarehe 31/01/2011 hadi 11/02/2011.
ii. Pemba kuanzia tarehe 28/02/2011 hadi 11/03/2011

Mhe. Spika, katika kufuatilia kazi hizo, Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi iliundwa na Wajumbe wafuatao:

1.	Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	-	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Ali Salum Haji	-	Mjumbe
4.	Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Mjumbe
5.	Mhe. Mohammed Haji Khalid	-	Mjumbe
6.	Mhe. Salma Mohammed Ali	-	Mjumbe
7.	Mhe. Ussi Jecha Simai	-	Mjumbe
8.	Ndg. Rahma Kombo Mgeni	-	Katibu
9.	Ndg. Ramadhan Kh. Masoud	-	Katibu

Mhe. Spika, muhtasari huu unakusudia kutoa sura ya utekelezaji wa Kazi za Kawaida na Maendeleo za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la

Mapinduzi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Zanzibar na kubainisha mafanikio kwa maana utekelezaji wa kazi hizo, changamoto, maoni, ushauri na maagizo ya kamati kwa ofisi hizo pamoja na Serikali kwa ujumla.

OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

Mhe. Spika, kamati yetu inaipongeza kwa dhati ofisi hii kwa kuweza kutekeleza mambo mbali mbali kama vile kusimamia na kuratibu shughuli zote za sera na mipango, kuyafanyia matengenezo majengo ya Ikulu Unguja na Pemba, kuratibu shughuli zote za kitaifa na kimataifa kupitia Ofisi ya Faragha ya Mhe. Rais, kuratibu na kusimamia vikao vya Baraza la Mapinduzi, kuendelea na usajili wa kadi za Mzanzibari na vitambulisho vyenginevyo, kuendelea kuimarisha Ulinzi na Usalama kupitia katika vikosi vilivyopo katika Idara Maalum na kuendeleza shughuli za usafi na maendeleo mjini na vijijini.

Mhe. Spika, hata hivyo, katika utekelezaji wa kazi zake Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

1. Uchakavu na ubovu wa majengo ya Ikulu ya Mkoani, uchakavu wa paa na ukosefu wa maji katika Ikulu ya Wete.

2. Uchakavu na ubovu wa Vyuo vya Mafunzo na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Chake na Wilaya ya Mjini.

3. Ufinyu wa majengo ya Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Wilaya na Ofisi ya Kadi za Utambulisho.

4. Kuwepo kwa mgongano wa sheria kati ya Manispaa na mamlaka ya Mji Mkongwe juu ya matumizi ya Bustani ya Jamhuri. Baadhi ya kanuni za Baraza la Manispaa kupitwa na wakati. Manispaa kukabiliwa na deni la ulipaji wa taa za barabarani.

5. Kikosi cha KMKM kinakabiliwa na uchakavu wa mashine mbali Mbale. Aidha, kina uhaba mkubwa wa vifaa vya kuzamia, lakini pia kinagharamika kwa kutumia lita 100 za mafuta kwa muda wa masaa 24 kuzihudumia boti zake. Kikosi kinamiliki chelezo kilichosita kufanya kazi kwa muda sasa.

6. Mazingira katika Vyuo vya Mafunzo hayaridhishi kwa wanachuo kuendelea kutumia mtondoo. Idadi ya rumande ni wengi ukilinganisha na wanachuo hali ambayo inapelekea kuitia hasara Serikali, malazi duni kwa wanachuo, lishe duni, ukosefu wa usafi na kukosekana kwa

kazi za amali mbali mbali kwa wanachuo. Pia ukosefu wa huduma muhimu ya maji hususan katika chuo cha Kengeja.

7. Kikosi cha JKU mabonde yake ya mpunga ya Kwa Pweza na Msaani yamekauka mno kwa jua na hayana visima vya maji ambavyo vingewezesha kuwepo kwa kilimo cha umwagiliaji na uzalishaji mkubwa wa mpunga. Pia wana ukosefu wa vitendea kazi vya kilimo mfano trekta kwa ajili ya kilimo.

8. Kikosi cha Zimamoto kina ukosefu wa Ofisi katika Kiwanja cha Ndege cha Chake Chake. Lakini pia kikosi hicho kina ofisi katika Wilaya ya Chake tu, walitafuta maeneo lakini bado hawajafanikiwa. Kikosi hichi kiliwapelekea Mamlaka ya Maji Pemba gharama za kuweka *stop cork* katika kila wilaya ili kurahisisha kazi zao lakini mpaka leo hakuna majibu.

Mhe. Spika, kutokana na changamoto hizo Kamati inatoa ushauri na maagizo yafuatayo kwa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na Serikali kwa ujumla:

1. Kamati inaiagiza Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuezeka paa jipya na kuchimba kisima kitakachowezesha kutoa huduma katika Ikulu hiyo ikiwemo ya kufufua bustani.

2. Kamati pia inaagiza Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kushirikiana na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kuifanyia matengenezo barabara iendayo Ikulu ya Chake Chake. Lakini vile vile Kamati inashauri kuna haja eneo la uzio wa Ikulu hiyo likawekewa sakafu ya vigae.

3. Kamati inaishauri serikali kuandaa mkakati wa kujenga majengo mapya ya kisasa ya Taasisi za Serikali yakiwemo ya Wakuu wa Mikoa, Wilaya na Vyuo vya Mafunzo ili kazi zitekelezwe kwa ufanisi.

4. Kamati inaiagiza Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuziimarisha nyumba za serikali za Mkokotoni na Bwefum. Lakini vile vile ni vyema ikaitisha zabuni kwa ajili ya matengenezo ya Ikulu ya Mkoani.
5. Kamati inaagiza jengo la Ofisi ya Wilaya ya Chake Chake kutotumika tena kutokana na uchakavu na ubovu wake.

6. Ni vyema kwa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuharakisha Sheria ya Marekebisho ya Tawala za Mikoa ili kuepusha

muingiliano wa kazi kati ya taasisi. Aidha, kuna haja kwa serikali kusaidia Baraza la Manispaa kulipa deni la taa za barabarani.

7. Kamati inaishauri serikali kukiimarisha kikosi cha KMKM kwa kukipatia vifaa vya uzamiaji, kukilipia deni inalodaiwa na bandari, kufikiria kutafuta njia ya kupunguza matumizi ya mafuta katika boti zake pamoja na kufufua chelazo kwa faida ya kikosi hicho na serikali kwa ujumla.

8. Kamati inaiomba Mahkama kuharakisha kesi kupunguza rumande katika Vyuo vya Mafunzo. Lakini pia wanachuo wanahitaji mazingira mazuri kwa kuwapatia huduma za kuridhisha kama vile maji, malazi, chakula, mafunzo ya amali na huduma za vyoo katika vyumba vyao.

9. Kuna haja kwa Wizara ya Kilito na Maliasili kukisaidia kikosi cha JKU kwa kukipatia msaada wa matrekta na kufikiria kukichimbia visima katika mabonde ya Kwa Pweza na Msaani kufanikisha kilito cha umwagiliaji.

10. Kikosi cha Zimamoto nacho kinahitaji kuimarishwa kwa kupatiwa ofisi katika Uwanja wa Ndege wa Chake Chake, kuwa na jengo jipya katika Ofisi ya Chake Chake pamoja na kuwa na majengo ya ofisi katika wilaya mbali mbali.

OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS

Mhe. Spika, kamati inathamini jitihada zilizochukuliwa na ofisi hii kwa kuweza kutekeleza majukumu mbali mbali kama vile kuweza kuendeleza mchakato wa kuanzisha *data base* kwa ajili ya watu wenye ulemavu, kuratibu mchakato wa kufanya tathmini ya athari za kimazingira na kijamii katika miradi tofauti, kutoa taaluma juu ya athari ya dawa za kulevya kwa jamii, kuendelea na kazi za uandaaji wa mkakati wa pili wa kupambana na ukimwi, kuendelea kusimamia na kuratibu sera na mipango ya ofisi.

Mhe. Spika, ofisi hii nayo katika utekelezaji wa kazi inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

1. Uhaba wa wafanyakazi katika Idara ya Ulemavu Pemba. Idara ya Ulemavu Zanzibar kukosa mashirikiano kutoka Idara ya Watu wenye Ulemavu Tanzania Bara katika suala la kuripoti kwa pamoja masuala yao katika vikao vya Umoja wa Mataifa. Vile vile idara hii haina uwezo wa kuwahudumia kimatibabu watu wenye ulemavu, sheria ya watu wenye ulemavu kuwawezesha kutumia miundombinu kwa

mazingira waliyonayo haitekelezwi, kwani majengo mengi yajengwayo hayazingatii sheria hiyo. Aidha, barabara zinazojengwa haziwawezeshi walemavu kuzitumia kwa mujibu wa mazingira yao.

2. Idara ya mazingira mfano Pemba kutoshirikishwa katika miradi inayopelekea kuchafua mazingira. Mfano uchimbaji wa kifusi unaofanywa na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa ajili ya ujenzi wa barabara. Idara hii pia haina vitendea kazi kupambana na uharibifu wa mazingira. Mfano Pemba kuna pikipiki moja tu kwa ajili ya kufanyia kazi hiyo.

3. Kuna ongezeko la maambukizi ya ukimwi kwa wanaojidunga sindano katika matumizi ya dawa za kulevya. Aidha, kuna uhaba wa elimu kwa wataalam wa tume katika baadhi ya kada. Pia kuna ukosefu wa kituo cha tiba na marekebisho ya tabia kwa watumiaji wa dawa za kulevya.

4. Vijana kutokuwa tayari kubadilika katika mapambano dhidi ya ukimwi.Unyanyapaa bado upo katika baadhi ya maeneo mfano Micheweni. Suala la kuzungumzia kondom kwa ajili ya matumizi linabaki kuwa nyeti kutokana na mila na dini. Tume ya Ukimwi ina ufinyu wa bajeti, inategemea zaidi washirika wa kimaendeleo.

Mhe. Spika, kamati kwa mara nyengine inatoa ushauri na maagizo yafuatayo kwa Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais pamoja na Serikali kwa ujumla.

1. Kamati inaishauri serikali kuongeza wafanyakazi katika Idara ya Watu Wenye Ulemavu, Pemba. Kamati inaona kuna haja kutekelezwa kwa sheria ya kuwawezesha walemavu kuwa na uwezo wa kuitumia miundombinu mbali mbali kwa mujibu wa mazingira yao. Serikali ni vyema ikawasaidia walemavu kwa kuwapatia viungo bandia. Idara ya Watu wenye Ulemavu ifikirie kutoa elimu ya moja kwa moja kwa jamii badala ya kutegemea vyombo vya habari pekee ambavyo baadhi ya watu hawana muda wa kuvisikiliza.

2. Kamati inazishauri Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, Idara ya Mazingira na Idara ya Ardhi Pemba kushirikiana katika miradi ambayo hupelekea kuharibu mazingira. Mfano, miradi ya barabara inayopelekea kuwepo kwa uchimbaji wa vifusi na uharibifu mazingira. Idara inahitaji kupatiwa vitendea kazi vya kutosha ili iweze kuratibu masuala ya kupambana na mazingira kwa ufanisi. Kamati inaagiza maeneo yaliyoharibiwa mazingira

kwa uchimbaji wa michanga na kifusi kujazwa taka. Mfano, Amani, Magogoni na Vitongoji. Kamati pia inaiomba serikali kuweka sheria ya kupiga marufuku matumizi ya misumeno ya moto ambayo kwa kiasi kikubwa imechangia uharibifu mkubwa wa mazingira.

3. Ni vyema kwa serikali kuharakisha ujenzi wa nyumba za kurekebisha tabia kuwawezesha vijana wanaoacha kuvuta unga kuzitumia nyumba hizo. Kuna haja kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kushirikiana na Tume ya Kupambana na Madawa ya Kulevya kuwawezesha vijana wanaomaliza muda wao katika nyumba za kurekebisha tabia *(Sober House)* kujiunga na vyuo vya amali, kuwapatia vifaa vya mafunzo mfano televisheni, kalamu, madaftari, kompyuta na vitabu ambavyo wanavyovitumia katika mafunzo yao ndani ya nyumba zao.

4. Kamati inashauri kwamba elimu ya ukimwi iendelee kutolewa kupunguza unyanyapaa hasa vijijini. Aidha, ni vyema kwa serikali kuchukua tahadhari kwa kuongeza fungu katika bajeti ya Tume ya Ukimwi ili iweze kufanya shughuli zake kwa ufanisi. Kwa kipindi kirefu Tume hii na baadhi ya Taasisi za Serikali zimekuwa zikitegemea zaidi fedha za washirika wa maendeleo ambao mitazamo yao kwa nchi zetu huwa haitabiriki.

OFISI YA MAKAMO WA PILI WA RAIS

Mhe. Spika, Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa vile vile inapongeza jitihada zinazochukuliwa na ofisi hii kwa kuweza kutekeleza mipango ya maendeleo na sera za ofisi, kuratibu na kufuatilia shughuli za *TASAF II* katika shehia zote za Zanzibar, kukamilisha rasimu ya Sera ya Taifa ya Kukabiliana na Maafa, kusimamia sherehe na maadhimisho ya kitaifa, kulifanyia matengenezo jengo la ofisi pamoja na nyumba ya Makamo wa Pili wa Rais, kusimamia utekelezaji wa utungaji wa sheria mbali mbali na kusimamia utekelezaji wa Kura ya Maoni na Uchaguzi wa mwaka 2010.

Mhe. Spika, mbali na utekelezaji wa majukumu yake ofisi bado inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

1. Idara ya Maafa haina usafiri, inagharamika kukodi ofisi Migombani. Idara hii imepatiwa kiwanja Tunguu. Hata hivyo, imefunguliwa kesi Mahkamani na mtu ambaye anadai ndie mmiliki halali wa kiwanja hicho.

2. Uchakavu wa vitendea kazi na jengo la Idara ya Upigaji Chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. Aidha, jengo hilo hujaa maji kila mvua kubwa zinaponyesha na kupelekea usumbufu mkubwa kwa wafanyakazi. Idara hii pia ina ukosefu wa vitendea kazi mbali mbali kama vile usafiri, kompyuta, mashine pamoja na maslahi duni kwa wafanyakazi.

3. Ofisi ya Baraza la Wawakilishi haina jenereta kwa ajili ya kusaidia pale umeme unapokatika. Kuwepo kwa *echo* inayotokana na mtambo wa sauti ndani ya ukumbi mkubwa wa Baraza. Miswada huchelewa kuwafikia Wajumbe wa Baraza kwa wakati uliopangwa. Fedha za kugharamia masomo kwa wafanyakazi hazipatikani kwa wakati. Kuna uhaba wa vitendea kazi mfano mashine ya *binding* kuliwezesha Baraza kutengeneza vitabu vilivyokamilika. Jengo la Ofisi ya Baraza la Wawakilishi Pemba haliridhishi kutokana na uchakavu wake, lakini pia mkandarasi ingawa alikwisha kamilishiwa malipo yake ameshindwa kumalizia ukarabati wa jengo katika ofisi hii. Aidha, Ofisi ya Baraza la Wawakilishi kwa Unguja na Pemba haina usafiri kwa ajili ya Wajumbe wa Baraza.

4. Tume ya Uchaguzi ina ukosefu wa usafiri na maslahi duni kwa wafanyakazi. Aidha, Tume inashindwa kuwadhamini kimasomo wafanyakazi wake ambao hulazimika kujisomesha wenyewe. Tume inagharamika kukodi jengo ingawa imo katika mchakato wa kutafuta eneo la ujenzi wa ofisi yake mpya.

5. Miradi mingi ya *TASAF* huanza kwa muelekeo mzuri lakini baadae huzorota kutokana na sababu mbali mbali kama vile wanavikundi kutoelewana kwa sababu mbali mbali na baadhi ya viongozi wa jimbo kutokushirikiana na waratibu wa miradi lakini pia kutowasimamia wananchi wao.

Mhe. Spika, kamati kutokana na changamoto hizi inatoa ushauri na maagizo kwa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais na Serikali kwa ujumla kama ifuatavyo:

1. Mazingira ya Kiwanda cha Uchapaji kwa ujumla hayaridhishi, hivyo kamati inaishauri Serikali kukamilisha kiwanda hicho kwa kukipatia jengo jipya, vitendea kazi vya kisasa, *stationery* za kutosha, usafiri na maslahi mazuri kwa wafanyakazi kwa lengo la kuimarisha kiwanda hicho. Aidha, kiwanda kitakapowezeshwa kifikirie kushindana kibiashara ili kuongeza mapato ya serikali.

2. Suala la maafa linaweza kutokea wakati wowote na pahala popote. Hali ya dunia sasa inajidhihirisha wazi visiwa navyo hukumbwa na maafa ya aina mbali mbali. Zanzibar katika kipindi hichi nayo imekumbwa na maafa ya upepo ulioathiri maeneo mengi. Hivyo, kamati inaishauri Serikali kuweka Mfuko wa Maafa ambao utatumika wakati maafa yanapotokea. Kamati inaiagiza Idara ya Maafa Makao Makuu kuwapatia vifaa vya maafa vya akiba Idara ya Maafa Pemba kwa lengo la kusaidia pale maafa yanapoweza kutokea.

3. Kamati inaiomba Serikali kuharakisha upatikanaji wa jenereta kwa ajili ya Ofisi ya Baraza pamoja na marekebisho ya *echo* ndani ya Ukumbi wa Baraza. Kamati vile vile inaiagiza Serikali kufuata Kanuni za Baraza kuhakikisha kwamba Miswada ya Sheria inawafikia Wajumbe wa Baraza kwa wakati. Kamati pia inalishauri Baraza kuharakisha Sheria ya Mfuko wa Baraza kuliwezesha Baraza kufanya kazi zake kwa ufanisi. Vile vile kamati inaiomba Serikali ilipatie Baraza mashine ya *binding* kwa ajili ya kuondoa tatizo la utengenezaji wa vitabu. Kamati inaliagiza Baraza la Wawakilishi Pemba kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kukamilisha ukarabati wa jengo la ofisi. Aidha, kuna umuhimu kufanyiwa matengenezo sehemu ya jengo la ofisi lililochakaa pamoja na matengenezo katika nyumba ya Spika.

4. Kuna umuhimu mkubwa kwa viongozi wa majimbo kushirikiana na waratibu wa miradi ya TASAF katika kusimamia na kutekeleza miradi hiyo.

   Aidha, kamati inaishauri idara inayohusiana na masuala ya TASAF kutekeleza TASAF III katika miradi ambayo inahitaji kukamilishwa.

5. Kamati imebaini kwamba watu wengi hawaelewi dhana ya elimu ya uraia, wengi wao wanadhani kwamba elimu ya uraia ni kupiga kura tu, wakati ukweli ni kwamba elimu ya uraia inajumuisha vipengele vingi, kama vile maadili ya kazi, umuhimu wa ulipaji kodi na kadhalika. Hivyo ni vyema kwa serikali kupanga mkakati wa kutoa elimu hii kwa wananchi ili kuijenga jamii yetu katika maadili mazuri.

6. Kamati imebaini kwamba taasisi za serikali kwa Unguja na Pemba hazina mfumo wa bajeti wa aina moja. Kwa mfano, kuna

Afisi Kuu Pemba hutengewa bajeti kama vile ni idara moja, lakini afisi nyengine ina idara zake mbali huwa na bajeti mbali na zile za Unguja. Hivyo, kamati inaishauri serikali kuweka mfumo wa bajeti wa aina moja kwa taasisi zake.

HITIMISHO

Mhe. Spika, napenda sana kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza, kwa kunisikiliza kwa makini na utulivu. Pia napenda kukushukuru kwa mara nyengine tena wewe Mhe. Spika, kwa kuniruhusu kuwasilisha Muhutasari wa Ripoti ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, juu ya utekelezaji wa kazi za kawaida na kazi za maendeleo kuanzia Julai/Disemba 2010.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

TAARIFA

Mhe. Spika: Nakushukuru Mhe. Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

Waheshimiwa Wajumbe, kabla hatujaendelea nataka nishauriane na nyinyi kwamba shughuli zetu tulizojipangia kwenye mkutano huu wa tatu, kimsingi zilikuwa zimalizike leo siku ya Ijumaa. Lakini kwa sababu ambazo hatukuweza kuepukana nazo na kutokana na mkatiko mkatiko wa umeme wa mara kwa mara, basi imefanya shughuli zetu leo zisimalizike na kimsingi kazi iliyobaki inahitaji siku mbili. *(Makofi).*

Waheshimiwa Wajumbe, msinivunjie viti, sina bajeti. Sasa kutokana na hali tuliyonayo na kwa sababu serikali ilikuwa imejipangia shughuli nyengine kwa kuelewa kwamba shughuli zetu zingemalizika leo. Nataka niwaombe Waheshimiwa Wajumbe, kwamba shughuli iliyobaki hii ambayo ilivyo ichukuwe siku mbili mpaka siku ya Jumanne, basi tufanye jitihada imalizike siku ya Jumatatu. Hii najua haitopigiwa makofi, kwa sababu itabidi tujifinye kidogo. Kitu ambacho nakusudia tukifanye ni kwamba leo Ijumaa ni siku fupi inabidi tuondoke saa 6, ni muda wa saa moja kutoka hivi sasa. Lakini itabidi iwe tunaongeza muda pengine kuanzia jioni leo na Jumatatu kwa kipindi cha asubuhi na kipindi cha jioni, ili mradi shughuli zetu tumuombe Mhe. Makamo wa Pili wa Rais atufungie siku ya Jumatatu. Nikamwambia Katibu kama tunafanya kazi nzito za namna hii, kazi ambazo pengine ni za kufanya kwa siku mbili, na sasa tunataka kufanya kwa siku moja sasa tutakuwa tunafanya nini. Basi tumekubaliana kwamba kwa kuwa tutaongeza muda kwa hapa na pale,

jambo ambalo litachukuwa muda wa Waheshimiwa Wajumbe, basi malipo Katibu ambayo atalipa yatakuwa ni ya siku mbili mpaka siku ya Jumanne.

Nitakachowaomba Waheshimiwa Wajumbe ni kwamba tupange *point* zetu vizuri, tunakwenda moja kwa moja kwenye hoja na jambo lenyewe liliopo. Pengine tupunguze muda wa kusema. Lakini siku ya Jumatatu tumalize shughuli zetu, lakini Katibu na wewe ujitahidi na serikali bila shaka inasikia, kwamba malipo yatakuwa mpaka siku ya Jumanne lakini tutajibana shughuli zetu tuzifanye mpaka siku ya Jumatatu. Naomba sana Waheshimiwa Wajumbe tuliangalie sana hilo, kwa sababu baada ya hapo kuna shughuli nyengine nyingi za serikali ambazo zimekwisha kupangwa, ambazo kuzipangua kwake nazo zina uzito na ugumu wake. Hii yote inatokana na kwamba shughuli zetu tulijipangia kuwa zinamalizika leo, kwa bahati mbaya haikuwezekana hivyo.

Waheshimiwa Wajumbe, nawaombeni radhi tukubali hivyo na tujibane kwa kiasi hicho, ili shughuli zetu zote ziende kwa sababu ya hali tuliyokuwa nayo na bila shaka kwa manufaa ya wananchi wetu pamoja na sisi Waheshimiwa Wajumbe. Nawashukuruni sana kwa kunisikiliza hivyo. *(Makofi)*.

Jambo ambalo linaonekana kama vile tunalikubali. Pale ambapo haja itafika ya kuongeza muda basi tutaomba utaratibu ufanyike ili tuongeze muda wa kumaliza shughuli zetu, ili ziweze kukamilika kwa jumla shughuli zetu zote kwa simu ya Jumatatu. Waheshimiwa Wajumbe nawashukuru sana. *(Makofi)*.

Waheshimiwa Wajumbe, nina wachangiaji wawili mpaka hivi sasa, tujitahidi kupunguza muda na tuweke *point* zetu vizuri, tuanze kumsikiliza Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na baadae Mhe. Abdalla Juma Abdalla.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii kuweza kuchangia kamati ya viongozi.

Mhe. Spika, kama ulivyosema kuwa twende kwenye *point,* lakini pamoja na hayo kuna *point* nyengine ambazo inabidi lazima tuweze kuwasaidia kamati ili huko mbele isije kutokezea tatizo kwenye serikali yetu.

Mhe. Spika, niwashukuru sana wana kamati kwa yale waliyoyaona na kwa uadilifu kabisa, na leo wametuletea hapa ili tuweze kuchangia. Mhe. Spika, mimi nianze moja kwa moja katika Baraza la Manispaa.

Mhe. Spika, kamati kuna mambo mengine wameyaeleza ambayo ni mazuri tu, na ni wajibu wa kamati kwamba lile ambalo wamelitolea ushauri kwa mujibu wa sheria na kanuni ni lazima liweze kutekelezwa. Lakini kuna jengine ambalo

kama kuna kamati nyengine imeona kuhusu suala lile la manispaa, vile vile kanuni nayo inamruhusu kuweza kulichangia ili kupatikane ufanisi.

Mhe. Spika, hivi sasa katika Baraza la Manispaa tuna wimbi kubwa sana la matatizo ya mikataba kubabaisha. Mhe. Spika, hali ambayo sasa hivi huwenda ikapelekea Baraza letu la Manispaa kuweza kushtakiwa, ni jambo la aibu sana.

Mhe. Spika, mimi napenda kuzungumzia kitu ambacho nina ushahidi nacho kabisa, sizungumzii kwa kukurupuka tu, nazungumza vitu ambavyo nilivyoviona na ninaweza kuviwasilisha ili kufanyiwa utaratibu kwa mujibu wa sheria na kanuni za Baraza.

Mhe. Spika, kuna Kampuni hii ya Zantel ambayo baada ya kupelekewa ule ulipaji wa kodi ile ya ma-*slogan* ya milioni 700, basi Zantel wakaona hapana mzigo huu tuutuwe na tutafute makampuni ambayo yatakuwa na uwezo wa kutubandikia ma-*slogan* yetu kwa mujibu wa utaratibu. Hiyo imepitishwa kwenye bodi yao na ikaamua kutafuta makampuni na makampuni yakapatikana. Kati ya hayo makampuni yaliyopatikana moja ni *East African Medium* ambayo ilikwenda manispaa na hii ni *registration* hapa Zanzibar. Imekwenda kule imelipa kodi vile vilivyotakiwa na ikapewa mikataba, ili kufungishana kwa sababu ya kuweza kufanyakazi zake hapa kuwa tayari ni ruhusa na imekubalika iweze kufanya.

Mhe. Spika, mkataba huo uliofungwa ni tarehe 23 April, 2009 kuwa mwekezaji huyu ameruhusika kufanya kazi zake katika kuweka ma-*slogan* ya matangazo ya Zantel. Sisi sote tunaelewa Zantel ni wabia wetu hapa. Sasa ikiwa leo tunanza kumpinda panda Mhe. Spika, tunampeleka wapi. Ni jambo la kusikitisha sana. Mwekezaji huyu wa *East African Medium* ameisaidia Serikali ya Zanzibar kujenga *canopy* lile la uwanja wa ndege kwa milioni 200 kwa bure, ni kuonesha jinsi gani alivyoipenda Zanzibar, ni mzungu huyo. Hivi sasa yuko katika matayarisho ya kutaka kuweka ulinzi kwenye maegesho kama vile wenzetu Dar es Salaam, yupo tayari kwa hilo na ni bure pia kwa pesa zetu serikali itie mapato tu. Yeye akishatengeneza basi anasema serikali ipate mapaato.

Mhe. Spika, mwekezaji huyu ana mpango wa kutaka kuweka *security light* kwa kutumia *solar system*. Inapunguza hata ile nguvu ya kutumia umeme huu wa kawaida, sasa kaona yeye kwa njia hiyo anaweza kufanya na kutuletea neema hiyo. Lakini la kusikitisha Mhe. Spika, tumefika pahala sasa hivi tunambugudhi, ni jambo la kusikitisha sana. Leo huyu mwekezaji akitoka na kupeleka ripoti nje, ushahidi upo, vyeti vyake hivi hapa na ma-*slogan* yake yote haya hapa. Tunakwenda kumdhalilisha kiasi hicho, ameshafunga mikataba.

Sasa la ajabu na la kuchekesha, mkataba huu imo saini ya bwana anaitwa, samahani namtaja jina kwa sababu ndio aliyesaini Mzee ambaye alikuwa pale ni *acting manager*, au *acting* mkurugenzi wakati ule. Lakini kuna mikataba mingine ambayo inasema kuna Rashid ambaye na yeye alisaini. Mkataba huu unaeleza kuna njia zile za Mlandege, lakini Mlandege kuna kampuni nyengine imepewa inaitwa Aston. Aston yule lakini hana mikataba na amepachika mabango yake ya Tigo.

Mhe. Spika, leo mwekezaji huyu kila siku wanakamatwa watu wake, tena anakamatwa na mikataba anayo, tumempa wenyewe kodi zote kalipa. Mhe. Spika, kuna kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ilifanya kazi yake kwa kidiplomasia, baada ya kupata malalamiko kutoka Zantel kwa kupitia mwekezaji wake, kamati ile iliwaita pande zote kwenye ukumbi wako chumba nambari mbili, haikwenda manispaa. Iliwaita na kuwasikiliza jamani kuna malalamiko kutoka Zantel kupitia kwa mwekezaji wake ambaye ni *East African Medium*, kutokana na kushushwa mabango yake na wakati anayo mikataba. Kamati ilisikiliza vizuri. Kamati hiyo maana yake ukimuacha mtu mdogo ana- *professor* ile *professional* yake, ilikaa ikasikiliza vizuri Mhe. Spika, ikatoa maamuzi ya kusema kuwa basi sawa, kitu cha kuheshimiwa hapa ni mikataba hakuna kitu chengine chochote. Ni mikataba ndio iliyokubalika kwa mujibu wa sheria ndio itakayosikilizwa.

Lakini Mhe. Spika, mule katika kuulizwa hoja wale wajumbe, walisema kwamba haa! Sisi tunafuata muongozi wa wakubwa wetu. Akianzia waziri na mkurugenzi ndio wanaotusumbua na kutubabaisha. Hapa Mhe. Spika, asilimia 10 ipo hapa, haiwezekani. Leo nchi yetu inaendeshwa namna hii, huyu ana mikataba yake na huyu ana mikataba yake kwa makusudio gani. Mhe. Spika, hapa kuna kitu, kuna mchezo mchafu unachezwa, kuna asilimia 10 ipo hapa, haiwezekani, viongozi wetu hapa wanakula, tuseme ukweli tusifiche. Ukificha mke ndugu huzai, hili tuseme ukweli. Viongozi wetu wanatufikisha pahala pabaya sana. Ni dhahiri mtu yeyote atolewe nje akija hapa akitizama atasema hii lazima asilimia 10 ipo. Haiwezekani kwamba mikataba hii huyu aandike vyeke na huyu aandike vyake.

Mhe. Spika, hivi sasa mwekezaji keshasimamishwa njia ile ya Mlandege, kasimamishwa kabisa asifanye kazi na wakati ana mkataba huu hapa. Watu wake wameshatiwa ndani mara ngapi, wametiwa ndani mara ya kwanza waziri kenda kuwatoa. Kapewa ile njia ya halmashauri kule kaambiwa na halmashauri huna sheria, potelea mbali kastahamili, kapewa kile alichopewa kakubali. Waziri anapewa *direction* wakachukuwe kule njia ya halmashauri, lakini baadae waziri yule yule anapinda baada ya kupata ushauri wake wa kufanya kazi, anasema mkataba futa. Futa mkataba kwa mdomo, futa mkataba kwa maandishi. Leo mkataba wake upo huu hapa. Mkataba na mwekezaji wetu

Zantel umeshafikia muda, tutamlipa nini huyu kazi tumeshakosa, kwa kumsumbua kinyume na taratibu. Barua zimesambazwa na Kamati ya Miundombinu na Ujenzi katika wizara zote husika kuonesha jinsi gani kamati ilivyokuwa imeweza kutoa mawazo yake kwa kupitia kwa hawa watu wa manispaa.

Mhe. Spika, kuna barua ambayo wewe mwenyewe utacheka, kwa sababu ni kitu kinyume na utaratibu, lakini barua hiyo imeandikwa. Kwa sababu tayari tumeshatoa ruhusa ya kuwepo. Kuna mtu muhusika mkuu mwenyewe ambaye ni mwanamke anayehusika na suala la *slogan*. Anaandika barua kuwaambia kuwa katika kuja kwako kuweka mabango, basi mabango ya Zantel usiweke. Barua hii hapa mimi ninayo na kama kuna utaratibu mimi naomba kuundwe tume, kwa sababu manispaa kuna mchezo mchafu. Kamati ya PAC nendeni, na mkienda kule wachukuweni na Polisi kama wenzetu wa Uganda. Kwa sababu kule kuna mambo ya uchafu, utakuta basi limeuzwa milioni 48 kinyume na utaratibu, hata Baraza la Manispaa halijauidhinisha. Mkurugenzi anaruhusika kuidhinisha *five million.*

Mhe. Spika, hili mimi naomba kwa makusudi tuunde tume ili kwenda kuangalia uchafu huu unaofanywa. Kuna nafasi za wazi kule zinazotakiwa watu wawekwe wenye uwezo wao, basi anakwenda kuwekwa mtu mwenye uwezo wa hali ya chini kabisa. Suala hili Mhe. Spika, ni kosa kubwa na limefanyika kule.

Kwa hivyo, kama nilivyokuambia Mhe. Spika, kwamba mchango wangu utakuwa ni kwa manispaa tu, siendi kwengine kokote. Kamati ile ya Miundombinu na Ujenzi imedharauliwa, imetoa barua ya kuonesha ni jinsi gani ilivyoona kwa ufanisi. Anafika mwanamama anasema kamati gani hiyo. Anadharau na kwenda kusema vyengine kwa waziri kuwa eti anatukanwa, anatukanwa na nani. Kuitwa na kuulizwa hoja. Maana yake hoja zikiwa nzito utageuza maneno na utasema ndio umetukanwa. Kwa sababu alichoulizwa huyo mama ni kwamba mmeshampa mkataba wa njia hii ya Mlandege, je, wewe ilikuwaje. Akajibu maana yake mimi nimeona ule mchezo mchafu wa Mkurugenzi sikwenda kushughulika na suala hili. Haya ndio katukanwa hivyo. Hoja imemshinda kujibu, lakini kinyume chake anakwenda kusema ametukanwa.

Mhe. Spika, hali mbaya manispaa, tukifanya mchezo Serikali ya Makamu ya Pili tunakuambia, hayupo hapa makamu. Lakini Mhe. Waziri tumeleta barua na nakala hii ya kuonesha hali halisi ya mchezo mchafu. Nakuomba Mhe. Waziri, mimi nakujua Mhe. Mohammed Aboud, kwa suala kama hilo huna mchezo nalo kabisa, historia yako ni nzuri tu, suala hili naamini utalifanyia kazi. Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, kwa jina jengine Makufuli na wewe

tumeleta barua kwako, tunaomba hatua zichukuliwe. Kwa sababu katika kikao kilichokaa Mkurugenzi wako wa Sera alikuja, lakini katibu wa wizara ya Mhe Waziri Dk. Mwinyihaji hakupita, kaidharau. Katuona sisi sio lolote sio chochote, kumbe hatujui na sisi tuna *master* na ma-*professor* na kadhalika. Mhe. Spika, nasikitika sana kamati yako imedharauliwa, katibu kapelekewa barua kakataa kabisa. Lakini angekuja katibu basi huu uongo ungefichika. Leo wanawahangaisha. Mwekezaji wetu anahangaika hajui la kufanya nini. Mheshimiwa asilimia 10 ipo hapa, ikiwa katibu anakula asilimia 10 iko hapa.

Mhe. Spika, nasema tunaelekea kwenye bajeti hii ndio itakayozuia bajeti, tutapambana nalo suala hili. Naweka tahadhari mapema kutokana na suala hili linalojionesha. Kwa hayo Mhe. Spika, kama nilivyosema kuwa leo sitokuwa na mchango mkubwa. Naomba kama kutakuwa na uwezekano kwa mujibu wa taratibu au kuleta hoja binafsi kwa suala hili basi niko tayari na niko njiani kulitengeneza suala hili. Kwa hayo machache. Mhe. Waziri piga vizuri kofi. Mhe. Spika, naunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili kutilia mkazo yale ambayo tayari kamati wameyabaini katika kazi zao. Kwanza nataka nichukuwe fursa hii kuipongeza kamati kwa kazi nzuri waliyoifanya na ni kawaida ya Baraza lako Mhe. Spika, kwa kupitia kamati hizi kufanya kazi nzuri sana. Naiomba sana serikali iendelee kulitumia Baraza la Wawakilishi kama kiyoo cha kujiangalia pale ambapo wanafanya makosa. Mawazo yanayotoka kwenye kamati kweli yanasaidia sana na tumeona hatua nyingi zimechukuliwa na serikali kutokana na mawazo ya kamati hizi.

Mhe. Spika, mimi nataka nianze kwenye Afisi ya Rais. Katika afisi hii natilia mkazo tu kuhusu ukarabati wa jengo la Ikulu ya Mkoani, ambayo kwa kweli ni muda mrefu sana lile jengo limesahauliwa na kwa nafasi yake lile jengo ni muhimu sana, hasa ukizingatia sasa hivi tuna viongozi wakuu watatu wa nchi, ikija ikitokea wote wako Pemba, afadhali Wete kunakalika, Chake Chake haijambo lakini Mkoani kwa kweli hali yake sio nzuri na sio vizuri viongozi kama wale kuwaweka pahala pamoja. Kwa hivyo, nilikuwa nafikiria jambo hili ni muhimu sana Afisi ya Rais ifanye juhudi kama ilivyofanya kwa Ikulu ya Mnazi Mmoja na Ikulu ya Wete basi wajitahidi na Ikulu ya Mkoani nayo iwe katika hali nzuri, sambamba na Ikulu ilioko kule Bwefumu haiko katika hali ya kuridhisha hata kidogo ni muhimu sana nayo ishughulikiwe.

Mhe. Spika, nataka pia nizungumzie kuhusu changamoto zinazoikabili KMKM. Mhe. Spika, KMKM ni kikosi muhimu sana kutokana na kazi zake, ni kikosi kilichokuwa na dhamana ya kuangalia mipaka ya nchi yetu. Lakini kinakabiliwa na changamoto kubwa hawana nyenzo za kufanyia kazi, KMKM

sasa hivi wamekaa kama vipofu hawaoni, hawana rada. Wana rada kule karibu na Mtambwe toka enzi ya Mjerumani mpaka leo, limeshaharibika kwa miaka. Wana kilio kikubwa wako pale lakini hawaoni kinachopita pale mbele yao.

Kwa hivyo, nilikuwa naomba pamoja na kuwa mradi huu ni mkubwa Mhe. Spika, lakini nahisi kwa umuhimu wake ni vyema serikali ikajipanga hata kama ni malengo ya muda mrefu, lakini siku moja KMKM wawe na rada ya kuona kwenye mipaka yetu ya bahari. Mhe. Spika, meli za uvuvi na nyengine za kiuharamia zinakuja mpaka karibu na kisiwa cha Pemba kule, lakini wapi hawaoni. Wanatuibia samaki wetu na wanafanya kila matendo ya balaa kule lakini KMKM hawaoni chochote, mpaka wapewe taarifa kule na wasamaria wema kwamba njooni huku kuna hiki na hiki. Sasa kwa kweli huo sio utendaji, hawana vifaa vya kuzamia.

Mhe. Spika, mimi nina wazo na wazungu wanasema, *'batter quality than quantity'*. Mhe. Spika, vikosi vya SMZ ni vingi, ni vingi na vyote vina changamoto. Nilikuwa nahisi serikali iandae mkakati wa kupunguza baadhi ya vikosi, lakini vile vitakavyobakia viwe na ufanisi.

Mhe. Spika, mara moja niliwahi kusema hapa kwamba Kikosi cha Valantia, mimi nahisi ni mzigo kwa serikali, ni mzigo kwa sababu kinatumia pesa nyingi kwa mwaka, lakini ukiangalia mapato yanayoingia kupitia kikosi kile hayapo ni hasara tupu. Sasa kwa nini serikali haifanyi maarifa ya kukiondoa kile kikosi, halafu ile kasma ya fedha inayoingia kile mwaka kule basi wakaangalia kuviimarisha vikosi vyengine. Nafikiri hiyo ni rai nzuri.

Mhe. Spika, pia kuna changamoto nyingi sana katika Kikosi cha Mafunzo hiki nacho ni tatizo. Wale wanaopelekwa kule, ama wakiwa rumande au wakiwa wafungwa au wanafunzi kama wanavyoitwa, kwa kweli mazingira yanaonesha kwamba hawafanyiwi hata haki za kibinadamu. Haiwezekani Mhe. Spika, watu kumi na nne wanye katika ndoo moja, wanaita mtondoo wenyewe kule na ndoo hiyo iko katika chumba hicho hicho ambacho urefu wake hakifiki hata futi 10 kwa 10, basi mikojo na mavi yako humo humo. Mhe. Waziri ananiambia nisiite mavi niite kinyesi, sawa ni kinyesi. Lakini kiko hapo hapo.

Mhe. Spika, mtu anakaa kule kuanzia saa 11:00 za jioni mpaka saa moja za asubuhi ni yeye na kinyesi chake. Mimi nafikiri ile ni kuvunja haki za binadamu. Halafu majengo yenyewe ni machakavu hayana hata hewa ya kutosha. Yaani mtu wa kawaida kama atakaa mule kwa usiku mmoja basi siku ya pili ama atapata mafua au atapata malaria, hali ni mbaya sana Mhe. Spika, na hiki ni kilio cha muda mrefu sana. Kila wakati wa bajeti na kila tukipata nafasi basi tunazungumzia habari ya uchakavu wa majengo na majengo

yasiyokidhi haja ya Vyuo vya Mafunzo. Kwa hivyo, naomba sana serikali walitilie maanani sana suala hili.

Kilimo chengine Mhe. Spika, sio vizuri hata kidogo kutokana na athari ambazo zinajitokeza kuweka rumande za watoto katika majengo yale ambayo wanakaa watu wazima. Hivi karibuni kamati yetu ilipata kutembelea pale Kiinua Mguu, walijitetea wenyewe wakatuambia aah! Tumewatenga watoto. Lakini pale walipotengwa ni sawa sawa na ziro, maana ni mule mule ndani hamna kizuizi. Kwa hivyo, mimi nilikuwa napendekeza serikali katika mipango yake ya baadae, basi itengeneze jengo ambalo watakuwa wakiwekwa watoto mbali sana na pahala ambapo watawekwa watu wazima. Kwa sababu mambo yanayofanyika Mhe. Spika, kwa kweli ndio yaliyomfanya Mhe. Zahra Ali Hamadi siku moja alie humu ndani.

Mhe. Spika, labda sasa niseme kidogo kuhusu Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais. Mhe. Spika, afisi hii kwa mujibu wa mpangilio wa kazi zake kwa kweli ina changamoto nyingi sana, mambo yake yote mazito na ni muhimu sana. Afisi hii imekabidhiwa udhibiti au uratibu wa mazingira. Mhe. Spika, tatizo la uchafuzi wa mazingira ni janga katika nchi yetu na kwa kweli linahitaji mkakati maalum wa kulidhibiti, vyenginevyo visiwa vyetu vyenye kila aina ya haiba ya rangi ya kijani basi itapotea. Mheshimiwa mikoko inakatwa ovyo.

Mhe. Spika, labda nipige mfano mimi mwenyewe binafsi. Kuna kipindi shughuli zangu zote zilikuwa ni za kule pwani. Sasa mazingira ambayo niliyazoea kwa siku hizo, baada ya miaka miwili au mitatu nilipojaribu kutembelea tena kule, kwa kweli nilitaka kutoka machozi. Msitu wa mkoko uliokuwepo wakati ule na kwa sasa hivi hakuna hata ujiti mmoja na sasa maji ya bahari yanapata fursa ya kuja juu, na kuchukua maeneo ambayo yanatumika kwa kilimo. Kwa kweli tatizo hili linatokezea sehemu nyingi.

Kwa mfano, Mhe. Spika hata hapa Mbweni tulipo hapa miaka ya 1980 kama ukitembelea kwenye fukwe, basi ulikuwa ukiona jinsi gani maji yanavyopanda juu na kula maeneo hata ya minazi, kwa sababu mikoko iliyokuwepo tayari watu wameshaitumia kwa shughuli nyengine.

Kwa hivyo, kama tusipoangalia sana suala hili siku moja wataalamu wa ardhi watakuja kutuambia eneo letu la visiwa sasa limepungua kwa asilimia kubwa, labda ndio ile tunayoisikia kwamba siku moja visiwa vitazama. Kwa maana hiyo, siku zote maji ya bahari yanachukua ardhi. Kutokana na hali hiyo, naiomba sana Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kupitia kwako Mhe. Spika, iliangalie suala hili kwa uzito mkubwa sana.

Vile vile kuna suala la ukataji wa misitu tukiacha mbali hii mikoko, pia kuna ukataji wa misitu Mhe. Spika, yaani misitu inakatwa ovyo sana na mingine ni mipango ya serikali labda hawakutanabahi, kwa sababu kule kwetu Pujini mvua haziadimiki. Lakini kuna mradi mmoja wa Serikali kupitia Kilimo ambao haukufanikiwa, walikuwa na *bulldozer* na kukata miti yote kule na kupelekea mvua kuhama Pujini.

Mhe. Spika, pia kuna hawa wakataji mbao kweli hawa pamoja na kwamba wanatafuta riziki ya kutia mdomoni, lakini wanatuweka katika hali mbaya sana. Kwa kweli wanatumia ile misumeno ya moto na ile haifai hata kidogo.

Kwa hivyo, naiomba sana serikali kupitia kwako Mhe. Spika, ijitahidi kupanga sheria ili tuweze kuidhibiti na wala sisemi isiwepo, kwa sababu wakati mwengine unaweza kuanguka mti barabarani kama haujakatwa kwa msumeno ule, basi pengine kutwa nzima gari hazipiti na ukiwepo muda wa nusu saa tu tayari kazi imemaliza. Kwa maana hiyo, idhibitiwe kiasi ambacho haitotuchafulia mazingira.

Mhe. Spika, janga jengine kubwa ambalo kamati wameliona na kila siku huwa tunalipigia kelele ni suala la Madawa ya Kulevya. Kwa kweli ni tatizo kubwa sana katika nchi yetu, kwa sababu linatupotezea rasilimali watu, nguvu kazi ya jamii inapotea kwa kiwango kikubwa na hili ni tatizo la dunia nzima hivi sasa.

Kutokana na udogo wa visiwa vyetu vya Zanzibar mimi najiuliza hizi dawa zinapita wapi na siku zote serikali inapiga kelele, siku zote dawa zinaletwa pamoja na vijana kuzitumia dawa hizo, kwa kujipiga sindano na kumeza madonge pamoja na mambo mengine na hali hii inasikitisha sana.

Mhe. Spika, kuna tetesi kwamba na wala sina hakika nazo, lakini wasambazaji wengine wanapita katika maeneo ya viwanja vyetu vya ndege na bahati mbaya sana, kwa sababu mzigo wa dawa za kulevya unaoweza kuingia kwenye *briefcase* ya kawaida huwa ni mkubwa sana.

Sasa mtu anaweza kupita nao pale na sijui *security* iko vipi pale mpaka inabidi watu wanapita pale. Kwa kweli watu wengine wanafikiria labda kuna baadhi ya watu nyeti wanawadhamini kuwapitisha, kama hivyo ni kweli basi ni hali mbaya sana na inakatisha tamaa.

Nadhani Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais ifanye utafiti wa kina kuhakikisha kwamba wafanyakazi wa viwanja vyetu vya ndege wako macho sana, kama ni kupita basi bora wapite huko kwenye mikoko, lakini sio kwenye viwanja vyetu vya ndege au bandarini, kwa sababu ni sehemu zenye udhibiti

wa serikali tena iko macho. Sasa kuona mambo haya yanapitishwa mle kwa kweli ni kukosa uzalendo.

Mhe. Spika, kwa kuwa sitaki nitumie muda mwingi sana pamoja na kwamba wapo wachangiaji na sisi ni wa kwanza ni wachokozi tu, lakini wengi watajitokeza. Kwa hivyo, nataka nimalizie hapa isipokuwa niendelee kuipongeza kamati kwa kazi nzuri walizozifanya. Ahsante Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, pale kwenye *Gallery* tumepata wageni, ambao wanakawaida ya kuja kutusalimia kama sikosei hii ni mara ya nne huwa tunapata ndugu zetu wanajeshi kutoka nchi mbali mbali. Wakiwemo kutoka Kenya, Uganda, Burundi, Mozambique, Rwanda, Namibia, Zambia, Zimbabwe na Tanzania, kwa kawaida hawa huwa wanahudhuria kwenye Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi pale Arusha na katika mafunzo yao hutembelea shughuli zetu kwenye Baraza la Wawakilishi, wakati mwengine hupata nafasi ya kuwahutubia.

Sasa leo bahati nzuri kwa mara nyengine tena wapo mbele yetu wamekuja kutusalia na kuona namna ya shughuli zetu zinavyokwenda, pengine hasa faida mpya ambayo wataipata tukiwemo katika Mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, kwa sababu mara zote huko nyuma walizokuwa ilikuwa hatupo kwenye Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Therefore, Our Guest Members for Defense Forces from the countries of Kenya, Uganda, Burundi, Mozambique, Rwanda, Namibia, Zambia, Zimbabwe and Tanzania, I have the pleasure once again to most welcome you for your visit to The House of Representatives and to see the members in this time we are having The Government of National Unity and you have seen here we are working together in calm atmosphere and we are working very well indeed.

I'm happy today once again to give you this opportunity to greet my Members of The House of Representatives and this delegation is being lead by Brigadier General E. E. Tiyunga. *(Makofi)*

So may I humbly request for whole delegation together to rise, so that they can greet the members please. (Makofi)

Thank you so much indeed you are most welcome. Thank you.

Waheshimiwa Wajumbe tunaendelea, naomba sana nimkaribishe Mhe. Salmin Awadh Salmin na baadaye Mhe. Hija Hassan Hija. *(Makofi)*

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia mawili, matatu.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, wageni wetu sasa wanatuaga baada ya kufarajika kuona shughuli zetu. *(Makofi)*

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi ninaweza kuchangia mawili, matatu kuhusiana na ripoti hii iliyowasilishwa hivi karibuni na Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa).

Kwa hivyo, nitumie nafasi hii kumpongeza Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa), Makamo Mwenyekiti pamoja na wajumbe wote kwa kazi nzuri, ambayo wameifanya katika kipindi chote cha wiki nne cha shughuli za kamati. *(Makofi).*

Mhe. Spika, kamati hii imesheheni mambo mengine ambayo yanayohusiana na ofisi zao wanazozisimamia za Viongozi Wakuu pamoja na taasisi mbali mbali.

Kwa kweli tumeweza kuona changamoto zinazowakabili wenzetu katika utekelezaji wa shughuli zao za kila siku. Lakini tumepata nafasi ya kuona mafanikio ambayo wameweza kuyapata katika kipindi hiki.

Mhe. Spika, nataka nizungumzie maeneo mawili makuu. Eneo la kwanza kuhusu Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais hususani katika eneo la Baraza la Wawakilishi, kama Waswahili walivyosema kwamba sadaka mara nyingi inaaza nyumbani, ndio tunaanza nyumbani. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwenye ripoti ya kamati imezungumzia kuhusu suala la ukosefu wa janareta katika afisi ikiwa ni pamoja na *Echo*. Pamoja na kwamba suala hili tumekuwa tukilizungumza nje ya taratibu, lakini leo tupo kwa mujibu wa taratibu na tunaamini kwamba mazungumzo tutakayoyazungumza leo kuhusiana na suala hili, basi serikali itayatilia maanani. *(Makofi)*

Kwa kweli kukosekana kwa janareta katika chombo kikubwa cha aina hii ni jambo la aibu na kweli wenzetu wanatushangaa sana, kwa sababu tunafika pahala tunaahirisha kikao kwa nusu siku au siku mzima kutokana na matatizo ya kukosekana kwa umeme, hili ni jambo la aibu. *(Makofi)*

Kwa hivyo, serikali yetu imeweza kujenga jengo hili zuri ambalo tunalitumia, lakini tumeshindwa kutafuta janareta kwa ajili ya kuliendeleza na hili ni jambo la aibu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunaona aibu kubwa na kumekuwa na gumzo kubwa linalozungumzwa juu ya chombo kama hili kukosa janareta, kwa ajili ya kuendesha shughuli zake. Lakini tunapata hasara, yaani serikali inapata hasara, kwa sababu pengine muda ambao tungeweza kuutumia kwa ajili ya kuendesha chombo hiki tunautumia kwa shughuli nyengine.

Kwa maana hiyo, Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa bahati mbaya hayupo lakini Waziri wake yupo, basi tunamuomba sana kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba jambo hili alitilie maanani, ili kikao kijacho cha bajeti tuone kwamba janareta linapatikana katika chombo hiki muhimu kwa ajili ya shughuli zetu. *(Makofi)*

Suala jengine katika ofisi hii ni kuhusu *Echo*. Mhe. Spika, kwa kweli tunasumbuka sana Waheshimiwa Wajumbe wako, yaani tunapoteza *energy* kubwa sana katika kukaa na kumsikiliza Mhe. Mjumbe na hili pia nalo linapoteza muda mwingi, kwa sababu swali kila wakati kurejea, yaani tunapoteza muda ambao tungeweza kuutumia kwa shughuli nyengine. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, naiomba serikali kupitia kwako Mhe. Spika, itilie maanani sana suala hili, kwa bahati nzuri Katibu wetu wa Baraza la Wawakilishi alitueleza kwenye kikao cha *Briefing* kwamba kunahitajika shilingi milioni 11 kwa ajili ya kuondosha tatizo hili. *(Makofi)*

Kwa hivyo, tumuombe sana Mhe. Waziri katika Makamo wa Pili wa Rais namuona ananong'ona na Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Lakini nadhani wakati wa kikao cha bajeti suala hili litaondoka. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, kama unavyojua kwamba Kikao cha Bajeti kinachukua muda mrefu, kwa hiyo muda huo mkubwa ambao tutakuwa tunataka kupata nafasi ya kusikiliza bajeti ya serikali vizuri. Kwa mfano, hivi sasa Mhe. Spika mjumbe anaweza kuzungumza humu ndani ya ukumbi hatumfahamu na wala huelewi anazungumza kitu gani, lakini bado tupo na tunaendelea na shughuli zetu.

Kwa hivyo, tunamuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika tatizo hili liondoke, ili wakatii wa Bajeti ya Serikali itakapopitishwa tuwe *free*, kwa sababu hivi sasa hatuko *free*, yaani tumekuwa tunatumia nguvu nyingi kumsikiliza yule Mhe. Mjumbe anayezungumza. *(Makofi)*

Vile vile kamati imezungumzia kwenye Baraza letu juu ya Kitengo cha *Hansard* ambacho kiko katika Baraza letu, Mhe. Spika, naomba kunukuu.

Ukurasa wa 70 maelezo kuhusu Kitengo cha Hansard:-

> "Liliendelea kuimarisha Kitengo cha *Hansard* kwa wafanyakazi wanane (8) wa kitengo hicho kuendelea na mafunzo ya *Computer* na Uandishi wa Habari katika ngazi ya cheti, *diploma* na *degree* ya kwanza".

Mhe. Spika, tunaipongeza Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kuimarisha Kitengo cha *Hansard*. *(Makofi)*

Lakini kitengo hiki cha *Hansard* cha Baraza la Wawakilishi kina umuhimu wa aina yake na kinafanyakazi kubwa. Kwa maana hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba kitengo hiki kinahitaji posho maalum, hawa wafanyakazi wa kitengo hiki wanahitaji *treatment* maalum, kwa sababu wanakuwepo kabla sisi hatujafika na wanaondoka hapa wakati sisi tumeshaondoka. Kwa hivyo, wanatumia muda wao mwingi kwa ajili ya kufanya shughuli zetu hapa. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, nadhani si vyema wafanyakazi wa kitengo hiki tukawaweka sawa na wafanyakazi wengine. Kwa hivyo, kitengo hiki kinahitaji *treatment* maalum kulinga na uzito wa shughuli wanazozifanya, kwa kweli shughuli zao tunazithamini sana na pia tunaamini kwamba baraza hili linathamini sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nafikiri ni vizuri tukawapa moyo, ili waweze kufanya shughuli hizi kwa umakini zaidi na taarifa zetu zikawa *up to date*. Kwa hiyo, naiomba sana afisi hii kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba kitengo hiki kipewe posho maalum kwa ajili ya kufanya shughuli hii. *(Makofi)*

Suala jengine Mhe. Spika, ripoti hii inazungumzia kuhusu agizo lililopewa Afisi ya Mkuu wa Wilaya, naomba kunukuu Mhe. Spika.

> Ukurasa wa 56 maelezo kuhusu agizo kwa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mjini:-
>
> > "Kamati imeiagiza Ofisi hii kwamba kabla ya kusomwa kwa Bajeti ya Serikali ya mwaka 2011/2012, njia iliyofungwa pembezoni mwa Nyumba ya Kulelea Watoto Forodhani iwe imeshafunguliwa".

Kwa kweli hizi ni taarifa njema Mhe. Spika na mimi nakubaliana na wazo lililotolewa na wenzetu, kwa sababu njia ile ambayo imefungwa pale inaleta

usumbufu mkubwa kwa wananchi na wala hakuna sababu ya msingi ya kufungwa kwa njia au barabara ile na tunapata shida.

Kwa mfano, mtu ambaye anatoka Benki ya Watu wa Zanzibar ya zamani au Kamisheni ya Ardhi anataka kwenda maeneo ya Shangani, basi lazima azunguke, wakati zamani njia ile ilikuwa ni *shortcut*, yaani mtu anatoka pale na kupita katika njia ile bila ya usumbufu wowote, kwa bahati mbaya sana njia ile imefungwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwanza Mhe. Waziri atueleze sababu kubwa iliyopelekea njia ile kufungwa, lakini isitoshe atekeleze agizo la kamati kwa niaba ya Baraza. Kwa kweli Baraza ni chombo cha kusimamia wananchi na sisi ndio tunaokaa na wananchi kwamba barabara ile ifunguliwe, ili wananchi waitumie kutokana na kuwa wananchi wanapata usumbufu mkubwa na wala hatujaona sababu ya msingi kufungwa kwa barabara ile.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika wakati atakapokuja kufanya majumuisho basi atueleze sababu pamoja na hili agizo ambalo limetolewa na kamati kwa niaba ya Baraza limeishia wapi au ndio anasubiri wakati wa bajeti hatujui. Kwa kweli hili ni wazo zuri na nalipongeza na hata mimi limekuwa likinisononesha sana, kwa bahati nzuri wenzetu wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa wameliona.

Kutokana na hali hiyo, basi namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika kama ni yeye aliyefunga au serikali basi njia ile ifunguliwe, ili wananchi wetu waweze kupita kwa ufahisi na wala wasipate usumbufu.

Mwisho Mhe. Spika, kuhusu suala ambalo Mhe. Makame Mshimba Mbarouk amelizungumzia. Kwa kweli Mhe. Mjumbe alizungumza jambo ambalo linahitaji kuangalia kwa makini na zipo tuhuma ambazo zimewagusa haidhuru si moja kwa moja, lakini zimewagusa viongozi wakuu ambao wametajwa na alipendekeza kwamba iundwe tume kwa ajili ya jambo hili. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa maoni yangu ili kujisafisha pamoja na kujiweka sawa basi ukubali ombi la Mhe. Mjumbe la kuunda tume kwa ajili ya kuchunguza jambo hili. Vile vile Waheshimiwa Wajumbe wapate nafasi ya kujua juu ya ukweli wa jambo hili, vyenginevyo maelezo yatabakia na tuhuma zitabakia na zitaendelea kuwepo na itakuwa hatujafanya jambo lolote la maana. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe. Spika nakuomba ukubali juu ya wazo la Mhe. Mjumbe la kuundwa tume ya kuchunguza jambo hili, ili tujiweke sawa, kwa sababu naamini tume yako itafanyakazi vizuri na itawasilisha ripoti yake kwako na Waheshimiwa Wajumbe watapata nafasi ya kujua nini kinachoendelea. Kwa

kweli pamezungumzwa masuala ya 10 *percent* pamoja na mambo mengine na hizi ni tuhuma ambazo zinahitaji kutolewa ufafanuzi wa wazi na chombo chako. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magomeni tunaunga mkono Ripoti ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa na ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, mwisho kwa kipindi hiki namuomba Mhe. Hija Hassan Hija.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Ripoti ya Kamati ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa na ninaomba nitumie muda uliobakia, ili kumaliza mchango wangu.

Mhe. Spika, kabla sijaunga mkono au kuchangia ripoti hii nataka nitoe tahadhari moja ifuatayo. Mhe. Spika, sisi ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na tumechaguliwa kwa kuaminiwa, wananchi waliokaa kupiga kura zao majimboni na wale waliotoa maoni yao, basi walituamini kwamba tunaweza. Kwa hivyo, lazima serikali itambue sisi ni wenzao katika kufanyakazi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, juzi ninazo taarifa kwamba Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari iliadhirishwa katika Uwanja wa Mao-Tse-Tung na iliambiwa haina maana yoyote, yaani si kamati na leo Mhe. Makame Mshimba Mbarouk anatueleza kwamba kamati yake ilidharauliwa na hii ni hatari kubwa. Sasa haya yanakuja kwa sababu hatujawa na meno, isipokuwa tunayo meno ya nadharia. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe. Spika mimi kabla sijachangia nasema kwamba, ili wananchi pamoja na watendaji watambue umuhimu wetu basi kamati iundwe twende tukachunguzwe. Sasa ikiwa hakuna dhambi basi sisi tutawasifu kwamba hakuna kosa na kama kuna dhambi, nadhani serikali ikubali kuwa watu wanafanya madhambi, kwa sababu tabia hii ya kuficha kila kitu na hata kama kipo, kwa kweli inavunja moyo na kuna siku wananchi watachoka kutuchagua. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naunga mkono hoja ya Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kwamba kamati iundwe na mtuamini na tukuleteeni ripoti serikali kuwa sisi ndio Wawakilishi. Kwa kweli sisi tupo hapa kwa ajili ya kusimamia mipango ya nchi na wala sio kwa kupiga kelele. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya tanbihi hiyo niliyoitoa naomba niseme kwamba nachangia ripoti hii kwa ufupi na nizipongeze Ofisi hizi Tatu za Viongozi Wakuu wa Nchi. Kwa kweli ni viongozi ambao wanazo sifa zote, yaani wametimia umri wa miaka 40 ambao mtu anafaa kuchaguliwa kuwa Mtume. Kwa hivyo, viongozi hawa wanazo sifa kamili na kwa maana hiyo ni watendaji ambao wameaminiwa, basi lazima wafuate nyayo wa Viongozi Wakuu wa Watatu wa Nchi hii. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nianze mchango wangu kwa Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais katika Tume ya Uchaguzi. Kwa kweli kama kuna mwaka Tume ya Uchaguzi imeweka historia, basi ni siku ya tarehe 01 Novemba, 2010 pale ambapo walitangaza matokeo ya Uchaguzi katika *Hall* la Salama Bwawani mbele ya nyuso za wagombea wote.

Kutokana na hali hiyo, tume hii ilifanya sifa, kwa sababu kila Mgombea Nafasi ya Urais pale alikuwepo na kusikiliza matokeo yake *live* kupitia vyombo vya habari. Sasa kwa mtazamo wangu tume ilifanya jambo la kihistoria.

Vile vile mgombea ambaye alishindwa na kuwa mshindi wa pili basi siku ile alikuwa Maalim Seif Sharif Hamad alitoa tamko la kukubali matokeo. Lakini alisema pamoja na kukubali matokeo tume anaiamini, isipokuwa kuna dosari za kutokuwepo kwa *Secretariat* ya Tume, ambayo ndiyo inayosababisha matatizo madogo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa uungwana mkubwa Mhe. Rais mteule siku ile pale alikiri na kusema kwamba yeye ni Rais atalifanyiakazi juu ya kuunda *Secretariat* ya Tume. Sasa kwa kuwa ni matamko ya Viongozi Wakuu, kwa hiyo naomba nijue Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais wanasimamia vipi suala hili la tamko la Mhe. Rais siku ya tarehe 01 Novemba, 2010. *(Makofi)*

Suala jengine ni kuhusu Afisi ya Baraza la Wawakilishi na ripoti ya kamati imetueleza jinsi Baraza la Wawakilishi lilivyo na Mhe. Salmin Awadh Salmin amezungumza juu ya upatikanaji wa janareta na mimi naunga mkono ni aibu. Kwa mfano, juzi asubuhi magazeti yote pamoja na vyombo vya habari vyengine vinazunguza *issue* ya Baraza la Wawakilishi limeshindwa kuendesha vikao vyake kwa kukosefu wa janareta na hii ni aibu tena ni fedheha. Mhe. Spika, lazima ufumbuzi upatikane, ili tuweze kupata janareta. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, Mhe. Spika sisi hapa tulipo tumepata taarifa hizi kupitia waandishi wa habari, Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum (Mhe. Machano Othman Said) huniuliza huko Wizara ya Habari unayo *share* na wala sina *share* yoyote. Lakini wananchi wetu wanapata taarifa kwa msaada wa vyombo vya habari.

Mhe. Spika, nilipotaka mawasiliano na afisi yetu, basi niliambiwa hapa kipo Kitengo cha Mawasiliano na Habari, yupo mwandishi kutoka TVZ, Sauti ya Tanzania Zanzibar na sehemu nyengine na jumla yao ni watatu.

Kwa hivyo, ushauri wangu Mhe. Spika tuwachukue wenzetu wa TVZ ambao tayari wanamiliki vyombo na tuhamishie ajira zao Baraza la Wawakilishi. Kwa kweli wenzetu hawa wanakaa hapa kuanzia saa 3:00 mpaka 7:00 kwa malipo ambayo hayastahiki. Kwa kweli namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwa busara zake basi azingatie suala hili.

Kwa maana hiyo, kuwahamisha waandishi wa habari hawa kutoka TVZ na kuja hapa Barazani si dhambi na hayo yanafanyika, tuwahamishe ili waturushie taarifa zetu mbali mbali kuliko kuchukua TV nyengine za nje na kuturushia taarifa ambazo si sahihi. Mhe. Spika, naomba kwa busara kubwa, ili kuwaheshimiwa na kuwaenzi wenzetu hawa basi tuwahamishie Baraza la Wawakilishi na kutufanyia kazi zetu.

Vile vile suala jengine ambalo nataka nichangie katika afisi hii ni kuhusu mialiko ya Waheshimiwa Wawakilishi katika Shughuli za Kitaifa. Mhe. Spika, mwaka huu Januari sisi wengi tulikuwa Zanzibar hapa, kwa kweli tulipata tabu je twende katika Sherehe za Mapinduzi au tusiende, kwa sababu tumezoea kila shughuli ya kitaifa kualikwa, kwa bahati mbaya hatukualikwa kwa maana ya barua. Kwa hivyo, tulikuwa na utata kwamba twende au tusiende.

Kwa mfano, hata Mhe. Rais wakati anapotembelea majimboni basi hujiuliza je mimi niende au vipi, kwa sababu huwezi kwenda tu kwa sababu ni mwakilishi na kupata aibu. Sasa nadhani ni vyema tualikwe au tuekewe utaratibu kwamba Rais au Makamo wa Kwanza wa Rais ama Makamo wa Pili wa Rais anapokuja basi muwe mnakwenda moja kwa moja. Kwa hiyo ni vizuri kuekewa utaratibu wa kualikwa au vyenginevyo vipi ushiriki wetu katika Shughuli za Kitaifa za Viongozi wa Wakuu.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye Afisi ya Rais. Kwa kweli hapa naomba nitoe pongezi tu, Rais kwa uamuzi wake wa kuanzisha Kitengo cha Kuratibu Wazanzibari Waliokonje. Mhe. Spika, maamuzi haya ya Rais ni ya busara sana na yameanza kuleta matunda. Kwa mfano, nimezungumza hapa kwamba wapo Wazanzibari waliokuwa nje ya nchi wameanza kurudi na kufanyakazi nchi kwao. Hali hii inatokana na maamuzi ya Mhe. Rais kuunda Kitengo hiki cha Wazanzibari Waliokonje.

Mhe. Spika, mwisho kabisa niende kwa Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais na suala linanigusa sana kuhusu mazingira. Kwa kweli mimi nitamaliza Baraza hili sikubaliani kwamba wananchi peke yao ndio wanaoharibu mazingira.

Kwa mfano, juzi Mhe. Hamza Hassan Juma na bila ya shaka ameliona eneo la Mwambe na alisema jinsi maeneo yetu sisi Pemba yalivyoathirika na hata Unguja. Lakini chanzo kikubwa cha uharibifu huu ni serikali yenyewe. Kwa masikitiko makubwa Mwambe Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais na Waziri wake wa Nchi Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais walikuja na tuliambana katika kufanya ziara na hali waliiona.

Mhe. Spika, hali waliyoiacha pale kwenye eneo la Mbuhoja wameona haitoshi wameelekea eneo jengine la pwani na wanachimba tena kuliko vile na hii ni hatari kubwa. Sasa wananchi ukisema kwamba ndio wanaoharibu mazingira, serikali inafanya nini na wala siamini kwamba kuna mradi wa wa kitaifa usiwe na *component* ya mazingira.

Kwa hivyo, nini fidia ya mazingira yale yaliyoathirika au suala lile la mazingira halitiwi kwenye miradi ya ujenzi wa barabara. Kwa maana hiyo, kama ipo *component* ya mazingira kwa nini wananchi wale hawafidiwi angalau kufukia kwa kifusi au mambo mengine. Mhe. Spika, vyenginevyo eneo la Mwambe bahari inaweza kupanda juu, ingawa siku ile aliyokuwa Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais watendaji walifukia yale mashimo ya bahari, lakini bahari inapanda juu.

Kwa hiyo, namuomba Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba suala hili alisimamie, ili tuweze kupata ufumbuzu kwa ajili ya usalama wa nchi yetu, vyenginevyo serikali itasababisha visiwa hivi kuzama na kutela maafa makubwa.

Mhe. Spika, baada ya hayo naunga mkono Ripoti ya Kamati ya Kusimamia Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa na ninawapongeza sana Mhe. Mwenyekiti pamoja na wajumbe wake. Ahsante sana. *(Makofi)*

(Saa 6:00 mchana Baraza liliahirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti na mimi kunipa nafasi hii ya kuchangia ripoti hii ya kamati ya kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, naomba nianze kwa kuwapongeza viongozi wetu wote

watatu wa juu wa kitaifa kwa kazi nzuri ambayo wanatufanyia. Nashukuru kwamba nchi yetu imepata viongozi watatu watu wazima wote ni watu wazoefu na wanaoheshimika na naamini chini yao nchi yetu itapiga hatua kubwa za kimaendeleo. Wito wetu ni kwamba waendeleze umoja miongoni mwao kwa sababu wao watakuwa ndio wahimili na msingi wa kuendeleza serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliyo katika muundo huu wa umoja wa kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti baada ya pongezi hizo na mimi niseme machache yale ambayo yamezungumzwa katika ripoti hii. La kwanza kabisa nianze katika Ofisi ya Rais upande wa Baraza la Manispaa. Kusema kweli Baraza la Manispaa linaonekana limeoza sio tu katika yale ambayo Mhe. Mshimba aliyataja asubuhi lakini katika hali nzima ya utendaji wake. Baraza la Manispaa linashindwa hata kuweka na kutunza usafi wa mji wetu kila unapopita unakuta taka zimezagaa mitaro haifanyi kazi wala haisafishwi na matokeo yake ni kujengeka kwa hali ya uchafu ambayo inaharibu ile taswira nzuri ambayo nchi yetu na hasa mji wetu ambao imejiwekea. Mji wetu naambiwa kwamba ni urithi wa kimataifa na hasa katika eneo la mji mkongwe kwa sababu hiyo una nidhamu zake. Lakini mtu anapokuja akauangalia hawezi kuamini kwamba mji huu ndio ule wenye ile hadhi ya kihistoria ambao ulipaswa kutunzwa.

Kwa hivyo hili nilikuwa naomba litizamwe kwa ukaribu sana na Wizara inayosimamia Baraza la Manispaa, na zaidi kwa sababu mvua zinakuja na sote tunazijua mvua za masika kuna hatari ya mji wetu kuja kuchafuka kweli kweli na kusabisha mafuriko kwa sababu taka hazizolewi na mitaro inawachwa bila ya kusafishwa, Baraza la Manispaa imekuwa kazi yake ni moja tu ni kama vile mkono wa mamlaka au bodi ya mapato kazi yake ni kukusanya mapato basi hakuna chengine kinachofanyika. Hili ni moja katika mapungufu yake makubwa sana kwamba tunadhani kazi ya Baraza la Manispaa ni kukusanya mapato kuliko kufanya kazi kwa kutumia mapato hayo kwa kuutunza mji na kuuweka katika hali ya kuridhisha.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani kwa kiasi fulani suala hili linachangiwa na ni suala moja ambalo Wizara inapaswa kutupiwa mamcho, ni suala zima la Baraza la Manispaa wenyewe kwa maana ya wale madiwani waliochaguliwa hawaonekani kwamba wao ndio hasa wenye udhibiti wa kuamua nini kifanyike katika Baraza la Manispaa na maeneo yake, badala yake Mkurugenzi ndio anaonekana ana mamlaka yote. Na hili ninasema kwa Baraza la Manispaa lakini inaonekana ndio hali kwa halmashauri za Wilaya takriban zote sasa hii inadumaza ule msingi wenyewe wa kuwa na Baraza la Manispaa na Halmashauri za Miji ambazo madiwani wake wametokana na kuchaguliwa na wananchi wenyewe, kote duniani Mabaraza kama haya wenye maamuzi ni hao madiwani kwa sababu ndio wenye ridhaa za wananchi waliowapigia kura.

Lakini Zanzibar tu tukaoona hata yale mamlaka kufanya maamuzi wanayo wao badala ya kuwa Wakurugenzi wa Manispaa au Halmashauri za miji kwamba wao watekeleze yanayoamuliwa na Manispaa, unakuta wao ndio wamejitwika dhamana ya kufanya maamuzi yote na kufanya wanavyotaka. Sasa ndio matokezeo yake yanakuja yale masuala ambayo Mhe. Mshimba ametueleza nimesikiliza kwa makini lakini suala hili pia limo katika ripoti ya kamati yao ambayo tumepewa pamoja, na mimi nataka kuunga mkono hoja yake kwamba kwa suala hili kwa sababu barabara anayozungumza tumeiona unakuta kweli kuna matangazo ya kampuni nyengine. Sasa kama kuna ushairi huo kwamba kuna mkataba na mkataba ukawa haukuheshimiwa huko ni kuvunja kabisa misingi ya utawala wa sheria kwa nchi yetu, na kunaweza kuitumbukiza serikali mara nyengine kudaiwa mafedha mengi katika kesi zisizokuwa na sababu, kwa sababu tu labda kuna watendaji fulani wanapata manufaa wao wenyewe.

Kwa hivyo na mimi nataka niunge mkono kabisa kwamba Baraza lako Mhe. Mwenyekiti, liunde kamati teule kuchunguza suala hili, haiwezekani tukajenga utaratibu kwamba kuna watendaji wanafanya wanavyotaka hawaheshimu mikono mingine ya dola kama ulivyo mkono huu , au mhimili huu wa Baraza la Wawakilishi wanaitwa kutoa maagizo hayaheshimiwi kama kuna suala pale, kama kuna usafi kamati itasafisha. Lakini kama kuna uchafu kamati ifichue ili Baraza lako hili ambalo la wawakilishi wa wananchi liweze kuchukua hatua zinazofaa na kweli watendji waheshimu vyombo vya nchi vilivyowekwa kusimamia uwajibikaji katika nchi. Kwa hivyo namuomba Mhe. Mwenyekiti kabisa tusije tukazungurushwa zungurushwa hapa. Mhe. Mwenyekiti, tuiombe Ofisi ya Spika, iunde kamati hii ili tupate ukweli wa kile ambacho kimejiri katika suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo kulizungumzwa hapa suala la njia ambayo imefungwa na mimi kwa ufupi niseme naunga mkono kwamba suala la kufungwa njia katika eneo lile la Forodhani kunaleta usumbufu mkubwa sana, badala ya kusaidia kufanya njia moja na kuna kipande ile imefungwa kabisa imepeleka kuwa na usumbufu mkubwa sana, hasa wakati maboti yanaposhusha abiria pale inakuwa mkanganyiko mkubwa sana, nadhani kuna haja suala la njia ile kufunguliwa ili wananchi wote waweze kunufaika kama walivyokuwa wakinufaika hapo kabla.

Niende katika Ofisi ya Makamo wa Kwanza Rais, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kuna haja ya kuitazama kwa makini sana suala hili la uharibifu wa mazingira. Uharibifu wa mazingira umeelezwa mara kadhaa humu ndani jinsi ambavyo unaathiri hali ya visiwa vyetu na mimi nataka kuzungumzia hasa ni kumuomba Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza

wa Rais achukue hatua za kufuatilia yale ambayo yalizungumzwa wakati wa Makamo wa Kwanza wa Rais alipofanya ziara ya kutembelea maeneo mbali mbali ambako kuna uharibifu wa mazingira. Sijui kama ni watendaji walioko katika Wizara hii kwa upande wa mazingira ishindwe kufuatilia au ni haya haya Mabaraza ya Manispaa na Halmashauri za Miji na Wilaya kwamba kuna maagizo yalitolewa yakatekelezwa pale mwanzo lakini baadaye hali imerudi kuwa mbaya sana.

Mhe. Mwenyekiti nataka kutoa mfano mmoja kwasababu unanihusu ni katika eneo la Mji Mkongwe hasa katika maeneo ya bandarini mpaka kuja maeneo tunayoita Rasil Heima pale nyuma ya Bwawani. Palisafishwa lakini sasa hivi uchafu umerudi vile vile ni kama vile tunafanya kazi kwa kuridhisha agizo la kiongozi, lakini baada ya pale watendaji hawaendelei kufuatilia na kuona kwamba hali inakuwa nzuri. Sasa katika hali kama hii tutawachokesha viongozi wetu wa kitaifa, kwamba kila jambo ili lifanyike ni lazima Rais aende au Makamo wa Kwanza wa Rais aende au Makamo wa Pili wa Rais aende akatoe maagizo ndio ifanyike kazi itakuwa hawa watu hawawezi kufanya kazi nyengine za kitaifa muhimu ambazo tumewakabidhi. Kwa hivyo nataka kuona na hili linafuatiliwa ili kuvitunza vizuri vyetu. Mhe. Mwenyekiti kutoka sehemu kunakochimbwa michanga na a mawe, kunakotupwa uchafu kote kwa jumla tunahitaji kuona mazingira yapo katika hali nzuri.

La mwisho Mhe. Mwenyekiti nije Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais nashukuru yale mengine niliyoataka kuzungumzwa yameelezewa kwa hivyo sitoyarejea kuhusu Baraza la Wawakilishi na haja ya kutekelezewa yale mahitaji yake ya msingi yameelezwa hapa kuhusu Tume ya Uchaguzi. Mimi nizungumzia suala moja tu kwamba Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais inashughulikia uratibu wa shughuli za serikali likiwemo suala la Muungano, hili limetajwa kwa ufupi sana karika tipoti mimi nataka kuligusia eneo moja tu ambalo sasa hivi katika nchi yetu limeshika kazi, suala la mjadala wa kutayarisha au kuja kuandika katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania .

Mhe. Mwenyekiti, jana nilisoma katika gazeti la *Citizen* na magazeti mengine yaliandika kwamba tayari Serikali ya Jamhuri ya Muungano imetayarisha Mswada utakaoweka utaratibu wa kuandikwa kwa katiba mpya, utaratibu sio ile katiba yenyewe ile *process* wanaita *constitution renew bees* ambayo inategemewa kuwasilishwa katika kikao kijacho cha mwezi wa April. Humu Mhe. Mwenyekiti, maslahi ya Zanzibar yanaguswa sasa sijui tumejipanga kiasi gani kwa sababu niliposoma yale yaliyoandikwa katika gazeti bahati mbaya sijaupata mswada. Haidhuru nimeuagizia niuone, huoni kwamba huko mwisho maslahi ya Zanzibar yatalindwa. Katika gazeti kunasema katika kuiteua tume ya katiba Rais wa Jamhuri ya Muungano atashirikiana na Rais wa Zanzibar na wajumbe wa tume hiyo watakuwa idadi sawa baina ya Zanzibar na Tanganyika.

Lakini unapokujasoma ule utaratibu unaokuja kufuata baada ya pale ambapo ndio msingi hasa wa maamuzi haki za Zanzibar hazizingatiwi kabisa.

Mwisho unazungumziwa mswada huu kwenye vyombo vya habari vya jana kwamba kutakuwa na kura ya maoni moja kwa Jamhuri nzima ya Muungano ya kuthibitisha katiba hii. Sasa ndio kusema yale tuliyokuwa tukiyazungumza siku zote kwamba katika kutoa maoni kama hayo. Wazanzibari wakipiga kura laki nne na wenzetu Bara wako milioni ishirini hata mkaamua kukataa nyote hamna uwezo ya kuyazuia. Kwa hivyo nilikuwa nataka kusema haya ndio mambo tuliyoyaona. Sisi wengine tuyajadili katika Baraza hili hata tukachukua hatua ya kuleta pendekezo la hoja binafsi, kwamba Baraza hili kama chombo na sauti ya wananchi wa Zanzibar liweke taratibu fulani ambazo zitaiongoza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kudai kwa serikali ya Muungano zizingatiwe ili kupata hati ikija katiba iwe ni kweli katiba ya wananchi inazingatia maslahi, haki, matarajio na matakwa ya pande zote mbili zinazounda muungano huu kwa maana ya nchi mbili zinazounda muungano huu.

Kwa hivyo nilikuwa naomba pia Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais watakapokuja Mhe. Waziri atujibu katika hili turidhike tusiwe tunaambiwa lugha zamambo mazuri kumbe kila kitu mmeshaelewana halafu tukaja tukalalamika baadae, kwa sababu taratibu kama hizi na katika hatua kama hizi hatuziheshimu. Mhe. Mwenyekiti naomba nimalizie hapa lakini nisisitize lile la kuundwa kwa kamati teule ya Baraza ili kuchunguza kadhia ya Baraza la Manispaa. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenekiti, anayefuata ni Mhe. Hamza Hassan Juma, hayupo, wa pili Mhe. Ali Abdalla Ali nae hayupo. Sasa tunaingia Ofisi ambazo zinahusika na Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

Mhe. Waziri Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kupata wasaa huu kuja kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa wajumbe katika michango mbali mbali inayohusu ripoti ya Kamati inayosimamia Ofisi za viongozi wakuu.

Mhe. Mwenyekiti awali ya yote naomba kumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Hamza Hassan Juma pamoja na kamati yake nzima na leo nafikiri *document* ile imewasilishwa vizuri kabisa na Mhe. Mwejuma Faki Mdachi.

Mhe. Mwenyekiti utakubaliana na mimi kwamba wizara yetu ni kubwa na ina mambo mengi lakini hakuna mtu hata mmoja asiyekataa kuelekezwa, asiyekataa kukosolewa kwa hivyo mimi niseme Mhe. Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe sote mimi pamoja na watendaji wenzangu, au

watendaji wangu tumeyapokea kwa moyo mkunjufu kabisa maelekezo yote ambayo tumepewa pamoja na wizara yangu vipi tuwaelekeze yale mambo na tujirekebishe vipi, makosa tumeyaona yapo na utendaji kweli kwenye utendaji siku zote unapotenda ndio unapoona matatizo. Kama hutendi unakaa ofisini tu huyaoni matatizo, lakini hizi kazi za *field* hizi unapotenda ndio unapoyaona matatizo. Kwa hivyo mimi nawapongeza sana waheshimiwa wote waliochangia na waliotuelekeza, vile vile waliotushauri jinsi ya kuendeleza mwenendo wetu.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla alizungumzia masuala ya ukarabati wa Ikulu na mwenendo wa vikosi na pia akatwambia habari za rada, kikosi cha valantia ni mzigo kwa serikali tumesikia, lakini nasema Mhe. Abdalla Juma Abdalla kile kikosi kipo kisheria na kinaendeshwa kwa taratibu ziliopo na tumekipitisha hapa hapa katika baraza letu. Kwa hivyo ningemuomba Mheshimiwa akafahamu tu kwamba kile kikosi kinatusaidia hilo jina tu labda ndio linakushtusha wale ni askari kamili, lakini hawako kambini wengine wako katika mkataba yaani nakusudia wa muda mrefu na wengine wapo nje lakini ikipigwa foleni leo basi wote wameshafika, hata wewe Mheshimiwa unaweza kwenda mafunzo kidogo ukawa askari wa valantia wa akiba.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Salmin Awadh Salmin alitushauri kuhusu ile barabara inayozunguruka Forodhani kule kuzunguruka pale kwenye nyumba ya watoto, unajua pale palifungwa ambapo wakati mmoja ilipofanywa Afisi ya Utawala bora Ofisi mpya ambayo yuko Mhe. Zainabu na Mhe. Haji Omar Kheri ndio wakati ule zilikuwa zinabanana gari sasa wakafunga iwe *one way* sasa walipofunga baadae wakaja wakafungua. Lakini pale hapakufunguliwa kwa hivyo pale kweli kuna matatizo usiku ukipita na hata mchana inakuwa mtu anavizia hasa wanaotoka kule Forodhani maana yake kule ni *one way* hutakiwi utoke Forodhani uje huku.

Lakini wengi kabisa mlikuwa mnatoka huku na wengine posta ya zamani mnakutana kwenye shimo lile. Sasa hilo Mhe. Mwenyekiti nataka kumuhakikisha Mhe. Salmin na waheshimiwa wengine kwamba hilo tutalifanyia kazi pamoja na kurudisha ule mtandao mzima wa *one way traffic* kama ulivyokuwa zamani,. Lakini hayo ni mapendekezo ya sera ya Mji Mkongwe wenyewe kule ambayo tumeagizwa tuyadhibiti magari makubwa na mwenendo kwenye mji mkongwe, nasema ushauri huo tumeupokea tutauzingatia pamoja na sehemu nyengine.

Mhe. Salmin Awadha pia alizungumza suala la Mkuu wa Wilaya kwamba ni agizo hilo tumelipokea na tumelisikia.

Nafikiri kama nilivyosema mengi kwa ujumla yamekusudia kutuelekeza, kutushauri na kutupa muongozo wa kufanya kazi ipasavyo, sasa naomba

nichukue dakika kidogo kuzungumzia suala ambalo Ndugu yangu Mhe. Makame Mshimba Mbarouk ambaye ndiye alilianzisha na waheshimiwa wangine wameliweka na mimi niseme labda kutofahamu tu kidogo hasa chanzo cha tatizo lenyewe.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk amelipata wamemfuata hao watendaji wa kampuni moja hii kampuni iliyowafuata kama alivyosema mwenyewe inaitwa *East Africa Medium* hao ndio waliomfuata na malalamiko kwamba wamenyang'anywa haki yao ya kuweka kwenye mabango hayo. Lakini nataka kumuhakikishia Mhe. Mshimba na waheshimiwa wengine hilo tatizo sio rahisi kama wanavyoliona wao, mimi ni Waziri na muwakilishi kama mwenzake. Yeye kaona tatizo aniite mimi waziri asimwite mtendaji mimi nipo kwa niaba ya kutumikia niite na si kweli kwamba kanita nikakataa barua ninazo hizi hapa kamuandikia moja kwa moja Mkurugenzi wa Manispaa aje kuzungumza nae. Mkurugenzi wa Manispaa hakuja peke yake amekuja na watendaji wake.

Sasa kosa lililotendeka hapo kwa nini asiniite mimi muwakilishi mimi ndio nawajibika kweke muwakilishi wale wadogo kidogo watazungumza maneno utakuja sema Mheshimiwa nimetukanwa na watendaji wako, sasa kuepuka yale nafikri utaratibu mzuri niite mie wala sio barua wala sio miyadi wengine wanafanya hivyo nawandikia barua bahati mbaya leo nina dharura au nitakuja siku nyengine. Lakini nafikiri kosa kabisa Mhe. Mwenyekiti kuwaita watendaji kwenye mambo kama haya na kidogo mambo yenyewe hujayapata kwa undani wake, sasa nataka kusema kwamba hilo jambo unavyoliona

Mhe. Mshimba sio jepesi hivyo nikisema sio jepesi hivyo nakusudia kwamba ni kweli Mhe. Mwenyekiti kuna kosa limetendeka Baraza la Manispaa limefanya kosa tunakubali kabisa, kosa lenyewe wao wamemkodisha mtu barabara kuanzia Mlandege mpaka Maisara, halafu kuanzia Maisara mpaka Air port wewe bwana weka mabango weye sasa yule anayeweka mabango kumbe kidogo kulikuwa na matatizo ya zile taa uweshaji wake alikuwa na matatizo haendi vizuri. Sasa wale baada ya kuvunja mkataba hawakwenda kukaa nae wao wamekwenda kuvunja mkataba wakampa mwengine yule akawekeza mabango yake wakati ameshalipa na ameshafanya gharama chungu nzima, sasa hilo ndio kosa walilolifanya watu wetu wa Manispaa hilo nakubali kweli ndio kosa walilolifanya.

Mhe. Mwenyekiti, huyo ninayemtaja ni *East Africa Medium* lakini kuna kampuni nyengine inaitwa *SISCO* hao ndio wenye mabango wanaowekwa kwenye hizo barabara zetu halafu kuna mwengine anaitwa *ASHTON* ni watatu hawa hao ndio walikamata ukiona hayo mabango yote yaliyowekwa humo mitaani wenyewe ndio wanagombana, unajua ni biashara na wao wanakuwa *sponser* na *ZANTEL na TICO* wanakuwa *sponser* wao waweke yale mabango.

Sasa wenyewe hawa wanagombana kiasi cha kututia kati sisi bahati mbaya wenzetu wa Manispaa waliingia kwenye mtego huo hawakuangalia vipengele vya kisheria huyu hawajamuona kwamba hakutimiza wajibu wake basi tumuondoe kwa taratibu za kisheria, wao wakenda kumuondoa tu bandika lile pale.

Sasa hapa kila mmoja anataka kumshitaki mwenziwe, sio kama anavyosema Mhe. Mshimba kwamba kanyima mmoja tu sasa hili sisi tulioingia wizarani juzi tumelipata wakaja hawa kaanza huyo huyo *East Africa Medium* aliyemsema Mhe. Mshimba mtaliana yule kaja akalalamika, kulalamika akaja na *ASHTON* mwengine akalalamika, akaja na *SISCO Corporation* nae akalalamika nikaona hapa kuna tatizo.

Sasa nilichofanya mimi nikaunda kamati yangu ndani ya Wizara ili kulifanyia utafiti hili suala kwa undani kabisa. Kwanza nilichogundua kampuni zote hizi zimetiliana mkataba 2009/2010 kwa hivyo Mhe. Mwinyi Haji wala sio Salum Kibanzi hiyo *ten percent* sijui tumepata lini mkataba umefungwa mwaka 2010 tarehe 10 November wa huyo *SISCO, ASHTON* umefungwa tarehe 20 October, 2009 wa tatu ambae Mhe. Mshimba anamtetea huyo ni *East Africa Medium* y eye ni mwaka 2009 wote hawa 2009/2010.

Mhe. Mwenyekiti sasa unaponambia kunanuka rushwa, tumekula rushwa hapo nafikiri Mheshimiwa anatuonea tena kwa kutaja jina Waziri na Katibu Mkuu nafikiri hiyo sio sahihi na namuomba ndugu yangu Mhe. Mshimba bora tuombe radhi kwa hilo, kwa kweli sio kibinaadam hiki ni chombo kikubwa unasikika unapomtaja mwenzio *ten passent* ata habari hana nafikri sio jambo jema sana.

Mhe. Mwenyekiti kama nilivyosema mikataba tunayo na baada ya kuona hili tatizo mimi nido nikaitisha hiyo kamati yangu kutafuta tatizo nini, tukagundua tatizo kumbe wenyewe wanapigana vijembe kuna mchezo wa faulu kila mmoja anataka barabara nzuri aicheze yeye, tukagundua hii kampuni ya *East Afrika Mideum* kweli wao kwa barabara hiyo niliyoisema walitia mkataba mwanzo kwa bahati mbaya hakutekeleza tatizo liko hapo tu , hakutekeleza ipasavyo alipaswa asafishe na achomeke yale mambo yao ya kitaalam akasinzia yule kusinzia ndio tulikuwa mji tuwashe kidogo uonekane upesi upesi unawake na unavutia sasa jamaa kidogo hawakwenda kitaratibu wakamwambia kaa benchi wakatia saini mkataba mwengine.

Sasa hilo ndio kosa walilolifanya sasa sisi baada ya kuliona hilo tulitisha kamati naomba nikusomeeni kidogo Naibu Katibu Mkuu wangu Tamisemi ndio nilimpa kazi hiyo, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa akanijibu tarehe 16 March, ananambia kazi hiyo ya uwekeji wa mabango ya matangazo katika taa za barabarani kwa heshima Mhe. Waziri naomba uhusike na mada

iliyotajwa hapo juu aidha naomba urudie maelekezo yako uliyotupa tarehe 21 February 2011 nilipowaagiza kazi hii, wakati tulipokutana ofisini kwako tulipojadili suala hili, pamoja na dokezo hili naomba kuwasilisha taarifa suala zima kama ambavyo utafiti wetu umeonesha wameonyesha utafiti mzima na ripoti ipo Mhe. Mshimba na waheshimiwa wengine yote ipo wazi kabisa tunawea kutoa *photocopy* kila mmoja akaipata. Lakini kama nilivyosema wote wanachezeana mchezo mchafu na kweli huyu karegea kidogo *East Africa Medium* akaingia mtu kwa hivyo wenyewe kwa wenyewe wamebinyiana, sasa nikasema kwamba niitoe kidogo *back ground* sio ionekane kwamba huyu *East Africa Medium* aa? Mwinyi Haji ndio kapata *ten percent* au Katibu Mkuu kamuonea si kweli na wala sio sahihi.

Suala la kutohudhuria vikao kulikuwa na suala jengine kwamba tumealikwa vikao hatukuhudhuria, Mheshimiwa kikao hiki ni kikao kikubwa sana kikao chako kitukufu na Mtu anapolipotosha baraza kwa kuwa tofauti na mwenzake ni kitu kibaya sana, hata siku moja Mhe. Makame Mshimba hajanialika kikao chake. Kwanza mimi siko kwenye kamati yake wala siwajibiki kikamati kwake lakini anaweza kunita kama alivyosema na nikenda, sasa hajafanya hivyo kamuandikia barua Mkurugeni wa Manispaa tarehe 9 March, 2011 wito wa kuhudhuria Kikao cha Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi, Mkurugenzi wa Manispaa alikwenda na Afisa anayeshughulika na mabango ndugu Mwanamvua. Waliitwa sijui Barazani au wapi? Kwa bahati mbaya ilikuwa kule wasikilizwe wao wajieleze upande wa serikali unasemaje au upande wa Baraza la Manispaa nao unasemaje. Lakini haikuwa hivyo Mheshimiwa.

Kwenye kikao hicho alikuwepo pia huyo Muwekezaji East Africa Media (Mtaliana) alikuwepo na msaidizi wake *counter* anaitwa Yussuf. Pale Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha. Mhe. Mshimba alimtukana yule kibibi afsa wangu, yaani kamvua nguo hasa. Matusi ya kumvua nguo mbele ya muwekezaji. Mhe. Mwenyekiti, *where we are going?* Unamchukua mtendaji mbele ya muwekezaji unakwenda kumtukana. *Just because* kwa kuwa anajiona yeye Mwenyekiti. Ndio Mwenyekiti, fuata taratibu, waziri si yupo. Unakwenda kumuumbua mtoto wa kike anafanya yake. Tena bahati mbaya yale yamefanyika wakatii Mkurugenzi wetu alipomwagiwa tindikali. ndio kipindi kile kile. Ndio huyu bibi akawa *subjected* kwenye *harassment* hiyo.

UTARATIBU

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu utaratibu imefika pahali sasa hivi Mhe. Waziri anasema masuala ya uongo tena inaoneshea matusi. Kwa sababu hayo yote unayoeleza hilo suala si kweli na mashahidi wapo, akiwemo mkurugenzi wa Sera na Mipango ya Mawasiliano

na Uchukuzi yupo, Meneja Menyewe wa Zantel yupo na Wahusika Wajumbe wapo na Mwanasheria wa Halmashauri yupo. Naomba Mheshimiwa utekelezaji wako.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, kiutaratibu ni kwamba kwanza Mhe. Mwakilishi alikuwa anatakiwa ataje kifungu ambacho amekitumia. Hajakitaja. Kwahivyo hilo kwanza ni kosa na ilikuwa hayo malalamiko yake yasichukuliwe kwa hivyo.

Pili ni kwamba Mhe. Waziri alipokuwa anaeleza yeye alikuwa anaeleza matokeo yaliyotokea hapo katika Kikao. Mimi nafikiri ni vizuri Mhe. Waziri aendelee kueleza. Kwa sababu yeye anajibu yale masuala ambayo Mhe. Mshimba alielezea. Sasa kama alikuwa anajibu nafikiri kwanza ni vizuri tumuachie yeye Mhe. Waziri kwa mujibu wa utaratibu aeleze. Halafu kama kuna hoja Mhe. Mshimba ndio atanyanyuka ili anukuu kile kifungu ambacho anataka yeye kichukuliwe hatua. Huo ndio utaratibu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Ahsante sana .Nakushukuru, Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria kwa ufafanuzi wako. Lakini pili nakushukuru Mwenyekiti kwa kunipa wasaa wa kuendelea.

Mhe. Mwenyekiti, kinachogomba sijui kama utaratibu wa Baraza kama ndio unavyoelekeza hivyo. Ninachofahamu mimi Masuala ya kiwizara unaitwa Waziri kwenye Kamati unakuja. Haitwi mtendaji. Hata huyo mtendaji kama unamwita sio kwenda kumtukana, kumuumbua. Tena mbele ya muwekezaji, hiyo inauma. Maana yake kenda kamwita kwa Maafisa wangu, na Muwekezaji upande huo hapo na baadhi ya wajumbe wa Kamati, wala sio sote. Kaitisha kamati njooni, akasimama yeye kama Mwenyekiti, wakamtukana wewe umekula rushwa, umenini, umenini.

Nilimwambia yule mtoto wa kike aje hapa, sijui kama yupo Mwanamvua. Mwanamvua kama upo hebu simama wakuone. Bahati mbaya hakuja. Ninachosema nafikiri narudia tena usemi wangu. Kukosolewa ni wajibu na sisi tunafanya kazi tuelekezane, tukosowane, turekebishane, lakini *approach* unatumia utaratibu gani. Hivi kweli wewe Mhe. Mshimba ungekubali mimi niko mbele ya kazi yako nije nikukane, nikuumbue!

Nasema mtu yeyote hakubali kufanyiwa kama hivyo. Ninachosema sasa kama mimi binafsi sioni ubaya wowote kuunda Kamati. Nini ninachosema Mhe. Mwenyekiti, naomba unisikilize vizuri. Sifikiri kama utapata *observation au conclusion* ambazo tumeshazifanya, mtarudia hayo hayo. Kwa hiyo ni *just* kupoteza pesa zetu na kupoteza wakati. Hayo utakayoyapata naamini hakuna kipya kwenye ripoti hii. Wizara tumeshayaona na tunaendelea kuyafanyia kazi.

Naamini tutafika *solution* kama nilivyosema hili suala sio dogo kama anavyoliona Mhe. Mshimba kwa mmoja. Wote hawa kila mmoja anamzunguka mwenzake. Baya zaidi hii arproch.

Kwanza mimi sio Kamati yake mimi Mhe. Hamza ndiye mweye Kamati yake. Lakini sio vibaya, haidhuru mimi Waziri. Ungekuja ukanambia ndugu yangu Mwinyi hebu nimesikia jinsi kadha, kadhaa. Tumecheza pamoja Kwahani huyo, yeye mdogo nimemfundisha mpira. Namjua vizuri. Sasa njoo tuelekezane, kuna tatizo hili na hili, hakuna tatizo. Lakini sasa unavyosema nimemualika kwenye kikao hakuja. Si kweli, hajanialika.

La mwisho baya zaidi kachukua barua kamuandikia Waziri wa Mawasiliano kuhusu kadhia hii. Haidhuru ni kweli mambo ya Zantel ni kwake. Waziri wa Mawasiliano kumshtakia haya mambo yalivyo yote. Sasa haya mambo si yapo kwangu mimi. Nambiye miye, au Mwenyekiti ananiogopa. Mimi sipigani naye, mimi tutashinda kwa hoja tu. Asiniogope Mwenyekiti. Tuzungumze kwa hoja, tushindane mpaka tupate manufaa ya kuendesha nchi yetu. Lakini unaposema unanikweka, waziri mwenye dhamana yupo unamkwepa. Sijui tufahamu vipi.

Nimalizie kwa vile Mhe. Mshimba alikuwa na *very strong allegation* na karudia zaidi ya mara mbili kwamba Waziri kachukua *ten percent* na Katibu Mkuu kachukua *ten percent*. Sasa ninachoomba kwa mujibu wa kifungu cha taratibu za Kanuni cha 59(3) ambacho naomba kukinukuu.

Kifungu cha 59(3) "Mjumbe yeyote anapokuwa akisema Barazani atawajibika kuwa na sababu za msingi kwamba maelezo anayoyatoa ni sahihi na sio mambo ya kubuni au ya kubahatisha. Spika, au Mjumbe mwengine yeyote anaweza kumtaka mjumbe huyo anayesema atoe uthibitisho wa usemi wake unaohusika"

Ninachotaka kusema mwenyekiti, Mhe. Mshimba karudia zaidi ya mara mbili mpaka tatu mbele ya ukumbi hii kwamba Mhe. Waziri na Katibu Mkuu wamechukua rushwa *ten percent*. Mimi naomba auambie ukumbi huu rushwa hiyo kaichukua lini na wapi na kwa misingi gani na kiasi gani, atoe ufafanuzi kidogo. Vyenginevyo Mheshimiwa kama kaona kateleza kwa jazba tunajua mwenzetu huyu. Alikuwa kidogo ana swing, akicheza wakati anasema. Basi atuombe radhi. Vyenginevyo mimi nakiachia kiti chako. Lakini kwa kweli nahisi tumevunjiana heshima tena heshima kama Mwakilishi na Waziri ndani ya Baraza. Mheshimiwa ahsante.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri maelezo ya Waziri yameshamaliza, kama hakuna hoja nyengine tunaendelea na Waziri mwengine.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nilikuwa naomba muongozo wako Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu katika mjadala huu labda niseme kanuni ya 117 katika hizi zilizoandikwa upya kwa za zamani nadhani itakuwa ni 115. Kuna suala la kuundwa kwa Kamati teule kwa hoja ambayo imetolewa na Mjumbe. Sasa katika wajumbe hoja ilitolewa na mjumbe katika mchango wake Mhe. Mshimba na katika wajumbe watano waliochangia hapa wajumbe wanne waliunga mkono hoja hii. Sasa nikuwa nataka kuuliza muongozo wako tu kwamba je, suala hilo litaamuliwa baada ya mjadala wa mawaziri wote kujumuisha na wakati wa kuipitisha hoja au linaamuliwa hivi sasa. Naomba muongozo wako Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, ni sawa kanuni imeungwa mkono, lakini utaratibu hii hoja imevunjwa sehemu za mawaziri watatu kwa hoja moja. Sasa hoja haijamaliza kasema Waziri mmoja, mpaka amalize wa pili na watatu. Halafu wewe ndio pale unauliza kama hoja hii imekubaliwa. Kama hoja haijakubaliwa au kama kuna masuala mengine ndio pale wajumbe wanaponyanyuka na kusema. Sasa hapo ndio tutaamua kama hoja ile iundiwe Kamati au isiundiwe. Ndio utaratibu.

Lakini hapa tupo kati kati ya mazungumzo, hatuwezi tukasitisha kwanza kabla hatujamaliza hoja yenyewe.

Mhe. Waziri Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kwa kuwa leo ni mara yangu kwa kwanza nikizungumza na wewe ukiwa mezani naomba nichukue nafasi hii kukupongeza dhati ni nikwambie hivi ndivyo Baraza lilivyo na ndio aina ya mitihani ambayo kama Spika na Naibu Spika na Wenye Viti inabidi mkabiliane nayo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru sana Mhe. Mwenyekiti, Hamza Hassan Juma na Makamo Mwenyekiti Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi na Wajumbe wote wa Kamati ya Kusimamia Afisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa kazi nzuri na ngumu waliyoifanya na hatimaye kutuwasilishia maoni, mapendekezo ya ushauri wao ambao umekuja kwa mfumo wa ripoti.

Mhe. Mwenyekiti, kuanzishwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Awali uliwatia wasi wasi baadhi ya wananchi na hata baadhi ya Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwamba eti kwa kuwa hakuna kambi ya upinzani iliyo rasmi, basi Baraza litapooza na serikali ingekosa kusimamiwa ipasavyo. Naamini Mhe. Mwenyekiti utakubaliana nami pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote na

wale waliokuwa wana wasi wasi kwamba Baraza la Wawakilishi katika mfumo wa Serikali ya Ummoja wa Kitaifa limekuwa imara zaidi, linaisimamia serikali kweli kweli. Sisi kama serikali tunalifurahia hilo kwa sababu ndio tunajua ufanisi wa yale tunayoyafanya utafanyika. Nachukua fursa hii kwa niaba ya Serikali kuwapongeza *back benchers* wote hongereni sana.

Mhe. Mwenyekiti, majumuisho yangu nimeyafanya katika sehemu mbili. Nitaomba nianze kwa ushauri mbali mbali ambao ulitolewa na Mhe. Makamo Mwenyekiti wakati wanasoma ripoti yao ya Kamati kwa ufupi sana. Katika ushauri ambao tulipewa na Wajumbe wa Kamati nitaanza na Idara ya Watu Wenye Ulemavu.

Tulitakiwa tuhakikishe kwamba sheria ambayo inasimamiwa itakayowafanya ndugu zetu wenye ulemavu wa aina mbali mbali kuweza kufikia majengo hasa yanayotoa huduma za kijamii kwa kuwa na miundombinu ambayo iwawawezesha wao kufikia.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nikuhakikishie Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais mara baada ya kukabidhiwa jukumu hili kwamba ni sehemu ya majukumu yake limeiangalie sheria, sheria Nam.9 ya mwaka 2006 na ikaona ndani yake kuna kifungu Nam.12(1) ambacho hiki kinazungumzia juu ya upatikana na uwezo wa kufikia hudma. Lakini vile vile kifungu cha Nam. 12(2) na Nam. 12(3) ambacho kinawataka wasanifu wa majengo kuzingatia michoro yao hasa wanapochora majengo ambayo yanatoa huduma za kijamii kwa wananchi ili kuhakikisha majengo hayo yanakuwa na miundombinu itakayowezesha ndugu zetu wenye ulemavu kuweza kuyafikia.

Naomba nichukue ushauri huu na niwahakikishie Wajumbe wa Kamati na Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu. Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais italisimamia suala hili ili kuona kwamba sheria inatekelezwa ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine kuhusiana na Idara ya Watu wenye ulemavu ni lile ambalo limeonekana Idara ya watu wenye ulemavu inakosa kutoa ripoti ya pamoja katika suala linalohusu watu wenye ulemavu hasa katika vikao au masuala yanayohusiana na umoja wa Mataifa.

Serikali kwa kuona umuhimu kwamba Tanzania ni moja, lakini ina nchi mbili ambazo kila moja inamatakwa yake. Tuna agizo maalum kutoka kwenye uongozi wa juu, kila wizara na ofisi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iwe karibu sana na ijenge mahusiano ya karibu na ndugu zetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kuhakikisha kwamba fursa zinazopatikana, mikutano ambayo inafanyika ya kimataifa yote tunashiriki na kutoa maoni yetu, ili tuwe

na ripoti ya pamoja katika mikutano hiyo. Naomba niwahakikishie wajumbe wako kwamba ofisi yangu inalifanyia kazi hilo na tatizo hilo litaondoka.

Mhe. Mwenyekiti, eneo jengine ambalo tumepewa ushauri na wajumbe wa kamati hii linahusiana na suala zima la mazingira. Naomba nitanabaishe tu, Waheshimiwa Wawakilishi tufahamu kwamba suala zima la mazingira ni suala mtambuka. Suala ambalo haligusi taasisi moja. Kwahiyo mkubaliane nami kwamba wakati Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais ndio yenye jukumu la uratibu wa kusimamia mazingira ya nchi yetu lakini bado kuna taasisi nyengine nyingi na hata jamii yenyewe ambayo lazima itoe ushirikiano ili kukamilisha uwepo wa mazingira bora ndani ya visiwa vyetu.

Mhe. Mwenyekiti, suala kubwa ambalo limezungumzwa hapa ni suala la athari za kimazingira ambazo husababishwa na miradi. Katika ripoti hii nilivyofahamu Kamati iliangalia miradi ya Serikali ya Ujenzi wa Barabara na jinsi ambavyoharibu mazingira, hasa kwa kuchimba kifusi katika maeneo mbali mbali. Naamini kwa kuwa niliwaona wajumbe wa Kamati wakiwa Pemba walitembelea eneo la Mwambe, naamini hili ndio hasa eneo lililokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kwanza Wajumbe wafahamu kwamba miradi yoyote iwe ya kijamii, iwe ya kibinafsi, iwe ya serikali inahitaji kufanyiwa *(environmental impart assessment)* yaani kuweza kujua miradi hiyo itaweza kusababisha athari gani za kimazingira katika utekelezwaji wake. Ni kweli kumekuwa na tatizo kwa kiasi fulani kwa baadhi ya taasisi za serikali. Katika kipindi cha nyuma kwa wakati ule hasa ikiwa Wizara ya Mawasiliano kutoishirikisha Idara ya Mazingira katika kufanya *environmental impart assessment.* Kitu ambacho kimesababisha kutokuwepo kwa njia za kuweza kukabiliana na athari ambazo zinaachwa baada ya matukio ya kutoa kifusi.

Mhe. Mwenyekiti, mara baada ya kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa na Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Ofisi ya Rais kapewa jukumu la kusimamia mazingira na kujua kwamba kuna tatizo hilo. Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais alifanya ziara katika maeneo mbali mbali ili kuona uharibifu huo na kujaribu kutafuta suluhisho ni kiasi gani tunaweza kukabiliana na uharibifu huo wa mazingira ambao upo katika kiwango kikubwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hapa naomba nimjibu Mhe. Hija Hassan Hija katika eneo lile la Mwambe Mhe. Rais nayeye ambaye kwa bahati nzuri suala la mazingira ni eneo lake. Alitembelea katika eneo hilo sehemu inayoitwa Mbuyu hoja ambako ndiko Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ilipokuwa inachukua kifusi cha kujenga bara bara na kuuwona uharibifu wa mazingira kukiwa na mashimo makubwa sana ambayo yameachwa. Siku ya tarehe 7

mwezi wa Machi, 2011 aliagiza *stop order* kwa Wizara ya Mawasiliano na Miundombinu, kuweza kusimamisha uchukuaji wa kifusi katika eneo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, hizi ni baadhi ya hatua ambazo serikali inapanga kuchukua kuona kwamba uharibifu wa mazingira unazingatiwa na unashughulikiwa kweli kweli. Pamoja na kufunga kuzuia kuchukua kifusi katika eneo hilo la Mwambe, Mbuyuhoja bado kama serikali tunahitaji kifusi katika shughuli zetu za maendeleo hasa za kuenga barabara. Kinachotakiwa kufanyika Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kuweza kuwa karibu sana na Idara ya Mazingira ambayo ipo katika Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais pamoja na Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka. Kwanza kushauriana kwa ajili ya kuangalia eneo muafaka ambapo wanaweza kupata kifusi hicho. Pia kuweza kupokea masharti ya jinsi gani kuweza kuchukua rasilimali hiyo ya mchanga na kuweza kutunza mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, eneo ambalo linatakiwa lichukuliwe kifusi baada ya kufanyiwa ukaguzi kwanza ni lazima liwe umbali wa mita mia mbili (200) kutoka kwenye bahari. Pia uchukuaji wa kifusi huo hautakiwi kwenda chini kuzidi mita mia mbili (200). Hicho ndio kiwango ambacho wataalamu wamekiweka. Baada ya kufungwa kwa maeneo ya Mwambe kwa ajili ya kuchukua kifusi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais cha Idara ya Mzingira Pemba na Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka pamoja na jamii akiwemo Sheha wa Mwambe, walikwenda kufanya utafiti na wakapata eneo jengine jipya ambalo Mhe. Hija amelizungumzia linaloitwa Mbuyu Bangamo au kwa jina jengine linaitwa Pangachumvi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuhakikishie sana Mhe. Hija kwamba uchukuaji wa rasilimali unaofanyika pale unasimamiwa na Idara ya Mazingira na pia unasimamiwa na Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka kuona kwamba unafanyika kwa utaratibu wa kitaalamu unaotakiwa.

Kwa taarifa ya Wajumbe Idara ya Mazingira inafika kukagua maeneo hayo vipi uchukuaji wa rasilimali unaendelea kila baada ya wiki mbili. Wananchi wa maeneo hayo wamepewa taaluma ya kutosha kuona kwamba wanaangalia rasilimali ambayo inachukuliwa na maeneo hayo hayapati uharibifu wa mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati iliendelea kutushauri kwamba kwenye maeneo ambayo kuna mashimo makubwa hasa katika maeneo ya uwandani ambapo kulikuwa na ukataji wa matofali. Pia katika maeneo haya ya Mwambe tukatupe taka ili kufukia mashimo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, ushauri sio mbaya lakini nataka niwafahamishe wajumbe wa Baraza lako tukufu na hasa wajumbe wa Kamati. Utupaji wa taka uliokuwa haujaangalia masharti ya kitaalamu unaweza kutuangamizia ardhi yetu na ikageuka jangwa. Ili taka ziweze kutupwa katika mashimo yale, tuhitaji kwanza tuzibague plastiki ikae mbali, kigae kikae mbali na taka ambazo zinaweza kuchanganyika na odongo mara moja ndio zinaweze kutupwa pale kwa ajili ya kufanya mbolea.

Mhe. Mwenyekiti, kati ya kuzichambua taka zinahitaji ujuzi utaalamu na vyombo ambavyo hivi wasa hatuna. Ushauri huu wa Kamati tunauchukua lakini tayari Idara ya Mazingira Pemba, Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka, Wizara ya Mawasiliano na Miundombinu na wenzetu wenye mradi wa small watafanya utafiti ni jinsi gani wataweza kurejesha hali katika maeneo ambayo mazingira yameharibiwa.

Wito wangu ni kwamba Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wawe karibu ili kuona kwamba kuna msaada unaohitajika katika maeneo yao basi waweze kutusaidia ili kulinda mazingira yetu.

Mhe. Mwenyekiti, eneo jengine ambalo Kamati imetupa ushauri ni kuhusiana na ukataji wa miti ovyo na suala zima la uwepo wa msumeno wa moto ambao unaonekana kuangamiza miti yetu. Hili tumeliona mapema ndani ya Ofisi wa Makamo wa kwanza wa Rais. Ninavyozungumza kama ambavyo nilijibu suala moja hapa juzi. Tayari tuna kanuni ambayo itasimamia matumizi bora ya msumeno wa moto. Tunachotaka kufanya sasa hivi tunawasiliana pia na Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka ili kuona kanuni hizo zinawekwa sawa na zipo kisheria na hazitaathiri utendaji wa shughuli nyengine za kijamii. Katika kupitisha kanuni hizo, wakati wowote tutaweza kuziweka saini ili ziweze kufanya kazi ili kudhibiti matumizi ya msumeno wa moto

Mhe. Mwenyekiti, eneo jengine ambalo kamati imetushauri ni suala zima la kuendeleza elimu ya ukimwi hasa katika kupiga vita unyanyapaa. Nataka nikubaliane na Wajumbe wa Kamati kwamba suala la unyanyapaa kwa wenzetu ambao wameugua maradhi ya ukimwi lipo na ni kwa kiwango kikubwa ndani ya jamii yetu, hasa katika maeneo ambayo sio ya Mjini. Kwa kuliona hili Tume ya Ukimwi Zanzibar imeanza na inaendelea kuandaa programu maalum ambazo zitalenga kuwafikia wananchi katika ngazi ya chini kabisa, ngazi ya shehia ili kuweza kupiga vita unyanyapaa.

Mhe. Mwenyekiti, programu kama hizo tayari zimefanikiwa katika maeneo ya Wete Pemba na vile vile katika eneo la Shehia ya Miembeni na bado Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais inaendelea na juhudi ya kueneza programu hizo

za kupiga vita unyanyapaa, lakini pia na kutoa elimu ya ukimwi katika ngazi ya shehia ili kuweza kuwafikia walengwa kule waliko.

Mhe. Mwenyekiti, eneo jengine ambalo kamati imeliona ni suala zima la udhibiti wa madawa ya kulevya, lakini walichozungumzia hapa zaidi ilikuwa ni kukosekana kwa kituo cha kurekebisha tabia yaani (*Rehabilitation Center*). Mhe. Mwenyekiti, hata mimi bado nilipokuwa *backbencher* suala hili nilikuwa nikilipigia kelele sana kwa sababu sheria za udhibiti wa madawa ya kulevya inahitaji kama atakamatwa kijana ambaye anatumia madawa ya kulevya awekwe ndani miezi sita ikithibitika na baada ya miezi sita apelekwe katika kituo cha kurekebisha tabia. Mhe. Mwenyekiti, kwa sasa hakuna kituo cha kurekebisha tabia ambacho ni cha serikali, eneo tunalo tayari katika eneo la Tunguu tatizo letu ni fedha.

Mhe. Mwenyekiti, kuanzia mwaka 2007 Idara inayoshughulikia Madawa ya Kulevya ilifanya juhudi za kutosha kuweza kuwasiliana na wenzetu wa Shirika wa Maendeleo bila ya mafanikio. Inapokuja kwenye suala la ujenzi ndugu zetu kidogo wanakuwa wagumu sana, na sisi tumeliona hilo na tumesema vijana ni wetu na tunaotaka kubadilisha tabia ni sisi na tatizo tunalo. Kwa hivyo, tumepanga kuweka bajeti wenyewe ya serikali ili tuweze kukabiliana na ujenzi huo ambao kwa kweli tunauhitajia.

Mhe. Mwenyekiti, eneo jengine ambalo ni la ujumla tu limeguswa na kamati ni suala zima la ukosefu wa wafanyakazi wa kutosha katika idara zetu mbali mbali za Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais hususan Idara ya Watu wenye Ulemavu Pemba. Lakini pia na vitendea kazi katika Idara ya Mazingira Pemba na maeneo mengine. Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nikubaliane na Wajumbe wa Kamati na kwanza wakumbuke kwamba Ofisi hii ya Makamo wa Kwanza wa Rais ni mpya ina miezi michache tokea iundwe na kwa bahati mbaya sana imeundwa kati kati ya bajeti ambayo ilikishwakupitishwa.

Kwa hivyo, sisi tumejipanga katika Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kuweza kushughulikia watumishi kuona kwamba Idara zote zinapata watumishi kwa ajili ya kutekeleza majukumu tuliokabidhiwa, vile vile kuweza kuandaa bajeti kwa ajili ya vifaa. Ni imani yangu Mhe. Waziri wa Fedha yupo hapa anatusikia na amekisikia kilio cha kamati kwa hiyo atatuwezesha *inshaallah* katika bajeti ijayo ingawaje simtoi shukurani ametuwezesha kabla ya bajeti kutengeneza mambo mengi ambayo imefanya ofisi angalau ianze kusimama na kuweza kufanya kazi. Kwa hivyo, naomba wajumbe niwashukuru sana kwa ripoti yao ya kamati.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba nijibu yale ambayo mmoja waligusa katika ofisi yangu na kwa kweli hawakuwa wengi. Mhe. Abdalla Juma Abdalla

michango yake naiheshimu sana na kwa kweli suala ambalo amelizungumzia yeye analiita ni uchafuzi wa mazingira, mimi na Ofisi yangu ya Makamo wa Kwanza wa Rais tunaliita ni uharibifu wa mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, nimesimama hapa mara mbili katika kumbukumbu zangu kujaribu kuwaelimisha Waheshimiwa Wajumbe tofauti kati ya uharibifu wa mazingira na uchafuzi wa mazingira. Anachozungumzia Mhe. Abdalla ni uharibifu wa mazingira.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri tujitahidi kuangalia muda zaidi.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, pia amezungumzia sana suala zima la kukatwa kwa mikoko na maji ya chumvi kupanda juu ya ardhi. Mhe. Mwenyekiti, hili tumeliona katika ofisi yetu na tayari kuna *pilot project* katika maeneo mengi kuwezesha wana jamii wenyewe kurejesha ile mikoko iliyokuwepo. Vile vile kwa kushirikiana na miradi ya TASAF kuweza kujenga matuta kwa ajili ya kuzuia maji ya bahari yasije zaidi kuathiri maeneo yetu. Lakini niwaombe basi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kuwa mko sana katika jamii mtoe taaluma yakuwaelimisha wananchi wetu waache kukata mikoko na hata miti ya kawaida ili kuzuia athari hii.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine alilozungumzia ni udhibiti madawa ya kulevya katika viwanja vya ndege na bandari, na jana tu nimejibu suala hapa linalohusiana na hayo nikwamba tufanyia marekebisho makubwa sheria za udhibiti wa madawa ya kulevya ili kuweza kwenda sambamba na kukabiliana na hali hiyo ambayo ipo sasa.

Mhe. Hija Hassan Hija tayari nimeshamjibu kutokana na yale aliyoyazungumza na ninamalizia na ndungu yangu Mhe. Ismail Jussa Ladhu Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Mjimkongwe ambaye naye amenitaka kama waziri kuweza kufuatilia yale ambayo kiongozi wangu mkuu amekuwa anayaagiza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli tunafanya hivyo na tutaendelea kufanya hivyo, lakini kama nilivyotanguliza kusema awali suala zima la usafi wa mazingira ni la Manispaa, kitakachofanya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa kuwa ndio waratibu wa shughuli za mazingira tutaendelea kuwakumbusha na kuwa karibu na manispaa ili kuona kwamba maagizo ambayo yanatolewa na viongozi wetu yanafanyiwa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache sana naomba nikushukuru.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu ili na mimi nipate fursa hii ya kutoa mchango wangu katika Ripoti hii ya Kamati. Kwanza kabisa nichukue fursa hii nimshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati hii ya Viongozi wa Serikali pamoja na makamo wake na wajumbe wote wa kamati hii kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kutusaidia sisi katika serikali kutekeleza wajibu wetu vizuri sana. Tunawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Mwenyekiti, pia nichukue fursa hii niwashukuru sana Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa namna wanavyoshirikiana na serikali, namna wanavyoisaidia serikali ili tuweze kuwatumikia wananchi vizuri zaidi, Waheshimiwa nawashukuruni sana. Aidha, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mwanasheria wetu Mkuu mpya ndugu yangu Mhe. Othman Masoud naamini mzigo aliopewa ana uwezo wa kuutekeleza vizuri sana, namtakia kila la kheri na mafanikio makubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, mengi yanayohusu wizarani kwetu yalikuwa ni ushauri kutoka kwa kamati, ushauri kutoka kwa wajumbe kwa hivyo ninachotaka kusema kwamba, ushauri huu tumeupokea na kuufanyia kazi. Lakini yako maeneo ambayo kwa haraka haraka tu ningependa niyaeleze zaidi. Kwanza kuhusu masuala ya Muungano nataka niwahakikishie Baraza hili tukufu kwamba nia na dhamira ni kuhakikisha kwamba maslahi ya Zanzibar yanalindwa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vikao vya pamoja vinaendelea vizuri yako mambo ambayo tunayazungumza na yameshapata muafaka na yako ambayo tunaendelea kuyazungumza. Dhamira yetu kwa pamoja sasa hivi ni kwamba tuzungumze kindugu, tushindanishe hoja na maamuzi yatakayofikiwa utekelezaji uchukue nafasi yake.

Mhe. Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wajumbe kuhusu masuala ya Katiba mpya nataka kumuhakikishia Mhe. Jussa na wengine wote waliochangia katika eneo hili kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejipanga vizuri kupitia Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wanawasiliana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kuhakikisha kwamba haki za Zanzibar katika utekelezaji mzima wa mchakato wa katiba mpya basi fursa Zanzibar zinapatikana na kwenye uwiano unaolingana. Naamini kabisa Mhe. Makamo wa Pili wa Rais atakapolifunga Baraza hili ataeleza kwa kina juu ya jambo hili.

Mhe. Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wajumbe pia kulikuwa na suala la Idara Inayokabiliana na Maafa hasa Wajumbe walitaka sana suala zima la kutoa elimu kwa umma. Mhe. Mwenyekiti, kazi hiyo imeanza kufanywa na serikali na tumeanza katika ngazi ya shehia na hivi sasa shehia ya 185 tayari zimeanza

kupata mafunzo hayo, na shehia nyengine zilizobaki tutaendelea kufanya juhudi hizo kwani hivi sasa tumeshazungumza na wafadhili na wameonesha nia ya kutusaidia kuendelea na mradi huu wa kuhakikisha kwamba tunatoa elimu kwa umma. Mhe. Mwenyekiti, kubwa katika hili ni kukamilisha mchakato wa sera ili iwe dira ya namna tutakavyoweza kupambana na maaafa.

Mhe. Mwenyekiti, nawahakikishia Waheshimiwa Wajumbe juzi tulifanya semina hii, imo katika mchakato ili ipite katika Baraza la Mapinduzi na baadae ipate baraka za Baraza hili ili utekelezaji uanze. Hata hivyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imo katika mchakato wa kuimarisha hii Idara ya Kukabiliana na Maafa ili iwe na uwezo wa vifaa vitakavyoweza kukabili maafa ya aina yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu kiwanja cha kujengwa idara hii, mazungumzo kati ya serikali na muhusika yanaendelea na fedha za awali zimetolewa na sasa bado shilingi milioni kumi na sita tunalishughulikia jambo hili ili kiwanja kile tuweze kukimiliki na ujenzi uanze wa kujenga Idara hii ya Kukabiliana na Maafa.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la nyumba ya kumbukumbu ya kumuenzi muasisi wa Mapinduzi Mzee Karume nataka niwahakikishie Baraza lako tukufu kwamba kuna mpango katika bajeti inayofuata kuanza ujenzi huo na nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wavute subra wakati tunalishughulikia jambo hili ili shughuli hizo ziweze kuanza. Kuhusu majina ya wanafamilia wanaotakiwa kupelekwa katika Bodi ya Kuenzi Viongozi wa Kitaifa tayari tumewasiliana na wana familia na majina sasa tunayo na mchakato unaendelea ili wana familia majina yao yawe yamepelekwa kule.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu Kiwanda cha Uchapishaji hasa ni kupata eneo jengine. Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba serikali inachukua hatua zinazofaa kwenye eneo hili na hivi sasa imeundwa kamati maalum ya wataalamu ili kuona eneo gani litatusaidia. Kwa bahati nzuri yako majengo ya serikali ambayo huko nyuma yalitumika kama viwanda na sasa hayatumiki tena, kwa hivyo kamati inayatazama majengo hayo na baadae itakuja na mapendekezo ili sasa badala ya kutumia Kiwanda cha Uchapishaji pale Saateni tutumie kwenye eneo jengine ambalo halitoingia maji.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na mitambo serikali tayari imetutaka wizara hii ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kuanza katika mchakato ili bajeti inayokuja tuanze kutenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa mitambo. Hata hivyo, tumeanza kuzungumza na wafadhili mbali mbali na bahati nzuri Serikali ya Oman imeonesha nia ya kutusaidia tayari tumeshawasilisha mahitaji yetu na tamaa ipo ya kupata mitambo hiyo kwa ajili ya uchapishaji. Naamini kadri

tutakavyoweza kuchapisha vizuri ndipo hata lile tatizo letu la kuhusiana na miswada tutaweza kulimaliza na manung'uniko ya Baraza hili kuhusu mambo ya miswada yatamalizika.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo kamati wameliona wanataka tutoe ufafanuzi ni kuhusiana na mfuko maalum wa Baraza la Wawakilishi. Ni kwamba Waheshimiwa Wajumbe tayari warka umeshatayarishwa na umeshapitiwa na Kamati ya Makatibu Wakuu, Makatibu Wakuu wametoa mapendekezo yao na sasa wizarani tunayafanyia kazi ili kuona kukamilisha kazi hiyo na kuwasilisha katika kikao cha Baraza la Mapinduzi ili uweze kuja hapa Barazani kuujadili Mswada wa Sheria ya Kuhusiana na Kuanzishwa Mfuko Maalum wa Baraza la Wawakilishi. Mhe. Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe mvute subra wakati tunalishughulikia jambo hili ili tuweze kuwa na mfuko wetu wa Baraza la Wawakilishi, na Baraza la Wawakilishi liweze kupata uhuru zaidi wa kufanya maamuzi yake.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu genereta sote tunaelewa ugumu wa tatizo la kukosa umeme humu ndani, serikali kwa kushirikiana na Baraza la Wawakilishi kupitia ofisi yangu na Ofisi inayoshughulikia mambo ya fedha tutahakikisha tunapata genereta yetu kabla ya kikao kinachokuja cha bajeti. Vile vile suala la eko Mhe. Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wajumbe wataalamu wameshakuja wameona tatizo lenyewe na sasa tunashirikiana kwa pamoja kulitafutia ufumbuzi na suala kubwa ni la fedha, lakini *inshaallah* hali inavyokwenda tutapata ufumbuzi mzuri tatizo hilo litamalizika katika ukumbi huu.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu mafunzo ya kikazi ya Waheshimiwa Wajumbe ni kwamba hilo ni jambo zuri, jitihada zimeanza Waheshimiwa Wajumbe kupata mafunzo hayo kadri ya hali ya uwezo wa kibajeti utakavyokuwa ndivyo tutakavyoweza kufanya kazi hiyo vizuri zaidi. Lakini hasa mfuko utakapoanzishwa ndio utaotizama jambo hilo na kufanywa kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wajumbe kuhusu maslahi ya Wajumbe tayari vikao vya awali vimekaa kuangalia maslahi stahiki ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu ili Waheshimiwa Wajumbe waweze kuwa na maslahi yaliyo mazuri zaidi kuliko yalivyo sasa. Mhe. Mwenyekiti, hasa kwenye upande wa usafiri na matibabu, jambo hilo limepewa kipaumbele na serikali yatashughulikiwa tunatakiwa tuvute subra wakati mambo haya yakishughulikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na ujenzi wa Ofisi ya Baraza la Wawakilishi Pemba ushauri tumeupokea na tutaufanyia kazi ili tatizo liliopo liweze kuondoka na afisi yetu ile iweze kujengwa vizuri na iweze kutumika.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu magari ya Spika na Naibu Spika ushauri tunaupokea tutaufanyia kazi kadri ya hali itakavyoruhusu sote tunataka tuone Spika wetu na Naibu Spika akipanda gari zuri linalostahiki kutokana na hadhi yake. Mhe. Mwenyekiti, tutajitahidi iwezekanavyo ili jambo hili lipate ufumbuzi. Vile vile kuhusu *binding machine* ushauri tumeupokea nataka nilihakikishie Baraza lako tukufu jambo hili tutalitafutia ufumbuzi na *binding machine* itapatikana.

Hata hivyo, kuhusu mialiko ya Waheshimiwa wa Baraza hili tukufu katika shughuli za kitaifa ni kwamba utaratibu upo wa kuwaalika Waheshimiwa Wawakilishi kupitia Baraza hili la Wawakilishi, lakini kama kuna kasoro yoyote imejitokeza tutachukua hatua kurekebisha kasoro hizo ili tuhakikishe kwamba waheshimiwa wetu wanapata mialiko mapema na waweze kushiriki katika shughuli za kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la elimu ya uraia ushauri tunaupokea ni jambo jema tutaufanyia kazi ili wananchi wetu wapate elimu ya uraia.

Mhe. Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wajumbe kuhusu Tume ya Uchaguzi kwanza kuhusu dosari zinazojitokeza katika uchaguzi, nataka nilihakikishie Baraza lako tukufu kwamba jambo hili linafanyiwa kazi na Tume yetu ya Uchaguzi na mara kazi itakapokamilika itakuja hapa Barazani ili tufanye marekebisho yanayofaa kwa msingi wa kuwa na tume nzuri na kwa msingi wa kufanya shughuli zetu za uchaguzi kwa haki na uhuru zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu kulipia ada za wafanyakazi wa Tume ya Uchaguzi wanapokwenda kwenye masomo yao, hii inategemea sana uwezo wetu wa kibajeti ni jambo jema, nia ya serikali ni kutoa mafunzo kwa watumishi wake wote. Kwa hivyo, jambo hili nalo litapewa kipaumbele. Kuhusu ujenzi wa Makao Makuu ya Tume ya Uchaguzi na ofisi zake Pemba na Unguja mwaka ujao tutaanza mchakato huu, na kwa kuanza baadhi ya majengo hasa baadhi ya Ofisi za Wilaya kwa sababu tunajua umuhimu wa kuwa na Ofisi za Tume za Uchaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na *TASAF III* ushauri tunaupokea kwani mchakato unakwenda vizuri kwa kuweza kufanikiwa na suala la *TASAF III*. Lakini suala la kupunguza kwa asilimia ya miradi, ushauri huu tunaupokea na tutaufanyia kazi tuone uwezekano utakuwaje na tutawaarifu wajumbe kadri ya makubaliano yatakayofikiwa kati yetu na wenzetu.

Waheshimiwa Wajumbe nilikuwa naomba jambo moja ambalo limejitokeza hapa na limezua mjadala sana, kuhusu kamati teule. Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nawanasihi sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu bado jambo hili tuachiwe serikali ili tulifanyie uchunguzi, na taarifa yake

tuiwasilishe rasmi katika Baraza hili tukufu. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja, ahsante sana.

Mhe. Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa (Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi): Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa ruhusa yako naomba niwashukuru tena Wajumbe wa Baraza lako tukufu pamoja na kuwapongeza wale wote waliochangia katika kamati yetu, na niwashukuru wale ambao hawakubahatika kuchangia hivyo nawaomba waungane na wale waliochangia kamati hii.

Mhe. Mwenyekiti, pia naomba niwataje wajumbe waliochangia kamati yetu ni:

1. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
2. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
3. Mhe. Salmini Awadh Salmin
4. Mhe. Hija Hassan Hija na
5. Mhe. Ismail Jussa Ladhu

Mhe. Mwenyekiti, pia naomba kuwashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote kwa majibu yao mazuri na naamini wajumbe wote wameridhika na majibu yao. Mwisho tunaahidi wana kamati inayoongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. Hamza Hassan Juma tutayafanyia kazi na kuyafatilia yale yote ambayo Waheshimiwa Mawaziri wameyaahidi kuyatekeleza, na yale ambayo wameyasahau kwa sababu za ubinadamu tutajitahidi kuwakumbusha na wao wapate kuyatekeleza.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la Waziri na Mjumbe kuunda kamati ninakuachia wewe Mwenyekiti kutoa maamuzi yanayofaa. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na nakupongeza kwa kumudu kiti chako. Ahsante naomba kuwasilisha na naomba kutoa hoja.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana nilitoa hoja hapa katika kifungu hiki cha ukurasa wa 88 kuwa nimeomba Kamati Teule kwenye Baraza lako kwa sababu hapa Mhe. Waziri ameeleza mengi mpaka kufika hadi mengine yaliyokuwemo na yasiyokuwemo, amesema kuwa tumemtukana yule mwanamke. Kwa hivyo, tunaomba iundwe Kamati Teule ndio itakayoeleza yote, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe tunahoja tatu baada ya kwishakupata maelekezo yote hayo. Kwanza inatakiwa Baraza iunde Kamati Teule kuchunguza kadhia ya Baraza la Manispaa. Je, kamati hii undwe au isiundwe. Waheshimiwa Wajumbe hoja ya pili Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kwamba aombe radhi au asibitishe kauli yake. Na hoja ya tatu je,

Baraza litaipokea ripoti hii ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Serikali au laa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba ili tulisaidia Baraza kwanza nirejeshe katika kanuni ili tupate kufanya maamuzi sahihi yatakayozingatia maslahi ya Zanzibar na watu wake ambalo ndilo jambo lilotuleta katika Baraza hili. Mhe. Mwenyekiti, kazi za kamati zimetajwa katika kanuni ya 106 fasili ya 14 iko ukurasa wa 73, nasema itakuwa ni lazima kwa kila Kamati ya Kudumu ya Baraza kuwasilisha ripoti ya shughuli zake mbele ya Baraza na masharti ya kanuni ya 117 yatatumika kuhusu utaratibu wa kuwasilisha ripoti hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kanuni ya 117 inaweka taratibu kuhusu Kamati Teule taarifa zake, lakini pia inasema ita-*apply* kwa kamati za kudumu ambazo tunajadili hapa. Mimi naomba niisome 117 fasili ya tatu inasema.

"Taarifa ya Kamati Teule itawasilishwa kwenye Baraza na Mwenyekiti au Mjumbe mwengine yeyote aliyeidhinishwa na kamati, taarifa hiyo itapigwa chapa au itashughulikiwa vyenginevyo kama Baraza litakavyoelekeza, endapo hoja itatolewa ya kujadili taarifa ya Kamati Teule na majadiliano kufanyika, hoja zinaweza kutolewa kuhusu azimio la kukubali taarifa hiyo pamoja na mabadiliko yake, au bila ya mabadiliko na kuchukua hatua kama itakavyoweza kuamuliwa na Baraza".

Kwa hivyo, la kwanza imezungumzia kuhusu kuipokea ripoti ya kamati nadhani hilo kwa jumla wajumbe hatuna tatizo nalo, lakini katika mjadala huu lilitoka hili la hoja ya Wajumbe waliojadili kutaka paundwe kamati teule. Katika wajumbe watano tulojadili ripoti hii wajumbe wanne tumetoa hoja ya kutaka iundwe Kamati Teule. Kwa hivyo, tukiangalia kanuni ya 50 fasili ya 4 kifungu kidogo (j) ukurasa wa 33 kinaendelea mpaka ukurasa wa 34, naomba niisome kwa kifupi tu.

"Hoja zifuatazo zinaweza kutolewa bila ya taarifa (j) ni hoja ya kuunda Kamati Teule".

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema kwamba nadhani kuna hoja ya kupokea kamati mbali, lakini katika mjadala huu kumejitokeza suala la kuundwa kamati teule ambalo kwa kanuni nilizozisoma nadhani ni sahihi kutohoji wajumbe ambao tunataka kamati iundwe na tukiwa wengi tunataka hivyo, basi kamati hii naomba iundwe.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho nataka kutoa indhari tu ndogo Mhe. Mwenyekiti, kwako vile vile kuhusiana na hayo. Nimeona kumekuja utaratibu mpya hapa,

kwa mujibu wa kanuni hizi nadhani kanuni ya 63 inazungumzia kuhusu utaratibu. Kunapotolewa hoja na wajumbe utaratibu anayetakiwa kuitolea maamuzi ni Spika au aliyekalia kiti cha Spika. Sasa tumeona utaratibu mpya hapa kwamba waziri anachukua madaraka ya Spika na anatuamulia hoja zetu za kanuni. Kwa hivyo, naomba hili lirekebishwe Mhe. Mwenyekiti, uzilinde kauli zako kwa sababu kanuni hizi pia zinataka Spika au aliyekalia kiti cha Spika ndiye atilie nguvu kanuni. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, naomba Mjumbe asome kanuni ya 115(2). Lakini kabla hajasoma kanuni hiyo ile kanuni ambayo aliisema ya 106 iliyosema kwamba itakuwa ni lazima kwanza atwambie kasoma kifungu gani? Kwa sababu hayo yaliyomo aliyoyasoma yeye humu hamna au awe amekosea kifungu, lakini kifungu cha 115(2) kinasema hivi:

> "Kamati teule itapendekezwa kwa njia ya hoja itakayotolewa na mjumbe na kuamuliwa na Baraza"

Baraza ndilo litaamua. Sasa hapa Mhe. Mwenyekiti, sisi tulikuwa tunatoa maelezo, hakuna waziri aliyeamua, hakuna mwenyekiti aliyeamua wala mjumbe aliyeamua, Baraza ndilo litaloamua. Lakini waziri, mwenyekiti na nani wanaruhusiwa kutoa maelezo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana, taarifa yangu ni kuhusu kanuni ya 50(5). Naomba ninunukuu.

Kifungu cha 50(5) kinasema:

> "Endapo wakati wa kikao chochote cha Baraza jambo lolote litatokea ambalo linahusu haki, fursa na kinga za wajumbe au uwezo wa Baraza, basi shughuli zote zinazoendelea zitasimamishwa isipokuwa kama wakati huo Baraza lilitolea uamuzi".

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni hii ya 50(5) mambo yote yasite mpaka lipatikane ufumbuzi suala hili.

Mhe. Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza ningependa kuwashukuru Wajumbe wote waliochangia kwenye ripoti hii ya kamati ambayo imemaliza kujadiliwa hivi sasa. suala ambalo limezungumzwa hapa na yametolewa mapendekezo ya kutaka kuundwa Kamati Teule ya Baraza, ni suala ambalo ndio kwanza limekuja katika Baraza. Serikali bado haijashindwa, tunashukuru kwamba serikali imetanabahishwa kwamba kuna kitu hicho, lakini serikali haijashindwa na wala mimi sijaletewa suala hilo kama kiongozi wa shughuli za serikali. Nimelisikia hapa tatizo hili kwa mara ya kwanza. *(Makofi)*

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema suala hili serikali haijashindwa kulishughulikia na mimi ningeomba Baraza likubali, iliachie suala hili serikali itaunda kamati na itafanya uchunguzi wa kina na Baraza litakuja kupewa taarifa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana na ninamheshimu Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, lakini katika kanuni hizi kwanza hakuna sehemu inayosema kwamba mpaka pale serikali inaposhindwa ndipo Baraza linaweza kuomba hoja ya kuundwa kamati teule. *(Makofi)*

Kwa mujibu wa katiba yetu Mhe. Mwenyekiti, Baraza lina jukumu la kusimamia shughuli za utendaji za serikali na Baraza ni pamoja na kamati zake. Kamati imefanya uchunguzi wake, imeleta hapa tumejadili, wajumbe wameona kuna haja ya kufanya uchunguzi katika kutekeleza kazi zake za Baraza zilizotajwa ndani ya katiba hii, kwamba litasimamia utendaji wa shughuli za serikali kama pana pahala panahitaji pafanyike uchunguzi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kusaidia tena Baraza nasema, Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria alisoma kifungu cha 115(2). Kuna utaratibu ule wa kamati teule ambao unaweza kuletewa hoja na mjumbe. Lakini pia mimi nilisoma kanuni ya 50 fasili ya 4(j) inayosema, katika hoja ambazo zinaweza kutolewa bila ya kutolewa taarifa ni hoja ya kutaka kamati teule iundwe ambavyo ndivyo ilivyoibuka katika mjadala huu. Kama nilivyosema mamlaka haya ni yako Mhe. Mwenyekiti.

Sasa nilikuwa nasema, kwa sababu inaonekana serikali na serikali ni wajibu wake kuanzia Mhe. Makamo wa Pili wa Rais na Mawaziri wake wote ni kazi yao kutetea serikali na ni kazi yetu Wajumbe wa Baraza kuibana na kuihoji serikali ili itekeleze yale ambayo wananchi watafaidika. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kumuheshimu sana Mzee wangu Mhe. Makamo wa Pili wa Rais mimi naomba katika hili atukubalie na kama kuna mvutano huo, basi kanuni ziko wazi tupige kura ili Baraza liamue kuundwa kamati teule au kutoundwa.*(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, sivizuri tena baada ya kiongozi wako kusema na weye ukaelezea maneno ya ziada. Lakini kwa ruhusa yake na kwa heshima yako Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme mawili tu, kama alivyosema na nilivyosisitiza Mhe. Makamo wa Pili wa Rais.

Kadhia hii serikali imeiona, hilo nafikiri niliweka wazi kabisa, kwamba kadhia hii serikali imeiona nime-*admit* kabisa kwamba tatizo lipo. Sasa baada ya

kuona tatizo mimi kama waziri niliunda kamati ndani ya wizara yangu na ikanipa ripoti kamili hii na ninaamini kwa hoja aliyoisema Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na wengine imejibiwa vizuri sana hii Mhe. Mwenyekiti. Naomba nikupe wewe *document* hii uwape wajumbe kama hawakuridhika na maamuzi haya kwa sababu **aliyochepea** Mhe. Makame Mshimba ni *East African Media*, tumekubali kweli. Sio uongo ni kweli na kweli yenyewe sasa sio hapo tu, wenyewe wana vurugu, wenyewe wote hao wana vurugu kwa hivyo kadhia hiyo tumeshaiona na tunaikubali. Sasa sifikiri kama kamati tunakuja ku-*establish* nini tena? Tunakuja kutoa kipi kipya? Hakuna mpya itayotoa zaidi ya hii.

Mimi Mhe. Mwenyekiti, naomba nikupe hii ripoti kama mpaka kesho au Jumatatu uisambaze wasome wote kama hawakuridhika na hii mimi nakubali tuunde kamati, kama hawakuridhika. Lakini sifikiri kama kuna kipya zaidi ya ripoti hii ambayo serikali imechukua mkondo wake na ile *heading* niliisoma kabisa, nilisema Kadhia ya Uwekaji wa Mabango ya Matangazo katika Taa za Barabarani. Mitaa hii yote tumeiona kadhia hii serikali. Kwa hivyo, si kipya kwetu ndani ya wizara, tunalifanyia kazi kutafuta, isipokuwa hawa baadhi ya wawekezaji kama nilivyosema hawatulii wanapita huku na kule wanachonganisha vichwa matokeo yake ndio haya. Huo ndio ukweli kabisa Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, sioni tupoteze muda, Mhe. Waziri keshakubali basi hakuna haja ya kupoteza muda tuunde hiyo kamati teule ndio itakayosema mambo yote. Nilipoeleza hoja zangu nilieleza sehemu nyingi tu, nilisema kuna ubadhirifu wa aina nyingi na nilieleza hapa wazi, ubadhirifu wa kununua gari, ubadhirifu wa kuweka viongozi kinyume na utaratibu au *qualification* zinazotakiwa, maeneo mengi tu nimeeleza. Kwa hivyo, tume teule itakayoundwa itaeleza yote wazi. Leo umepata kuona wapi mtu akajichunguza kwa nyumba yake? Nyumba yake mwenyewe akajichunguze umepata kuona wapi, mimi nitasema kweli choo kibovu wakati choo changu kizima, nitasema choo changu kizima wakati kibovu, mtu ndani ya nyumba yake hawezi kujichunguza, kamati teule i-*stick* pale pale tunaomba iteuliwe.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe baada ya kwisha kupata maelekezo ambayo yametoka pande mbali mbali na wajumbe kuchangia katika hili, nahisi sasa tuelekee kwenye maamuzi ya wajumbe ili tuweze kupata ufumbuzi wa tatizo ambalo linatukabili. Tutaanza na suala la kwanza ambalo tunasema je, Baraza liunde kamati teule kuchunguza kadhia ya Baraza la Manispaa au isiundwe?

(Kura ya Kuundwa Kamati Teule)

Tutaomba wale wajumbe ambao wanakubaliana na hoja hii wanyooshe mikono. Wanaokataa kuundwa kwa kamati hiyo,

Utaratibu

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, kwa utaratibu wa kanuni naomba kura zihesabiwe tena.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri unataka zihesabiwe zote zilizokubali na zilizokataa au upande mmoja tu?

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, zote tuanze tena, kwa sababu sijaridhika na ni haki yangu kama ni mjumbe.

Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe wanaokubali kuundwa kamati teule wanyooshe mikono juu, hesabu tena, imepita ee? Tunaomba ahesabu, tumia ya pili yake.

Katibu: Mhe. Mwenyekiti, kanuni inasema kura tuhesabu kwa mikono, lakini kama unatokea utata taratibu za kanuni zinaturuhusu tuite majina. Kwa hivyo, Mjumbe mmoja mmoja aseme kura yake.

Katibu: Mhe. Ali Abdalla Ali, hayupo. Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa.

Mhe. Mwenyekiti, Ndio mimi hapa kwenye kiti.

Katibu: Hapana, ni kwamba kifungu cha katiba kinasema ‘mtu anayeongoza kikao ikiwa ni Spika, atakuwa na kura ya uamuzi, kama si spika atakuwa na kura zote mbili ya uamuzi na kura ya kawaida. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, kura yako inatakiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Nimekubali isiundwe kamati teule. *(Kicheko)*

Katibu: Mhe. Mwenyekiti, naomba kusoma kifungu cha 83(2) cha katiba. “Jambo lolote litakalopelekwa kwa uamuzi katika Baraza la Wawakilishi, mtu atakayekuwa anaongoza kikao cha Baraza la Wawakilishi ikiwa ni Spika atakuwa na kura ya uamuzi na sio kura ya asili, ikiwa sie Spika, atakuwa na kura ya uamuzi pamoja na kura ya asili”. Kwa hivyo, swali lililotolewa ni kwamba, wale wanaokubali kuundwa kamati teule waseme ndio, wasiokubali waseme hapana. Kwa hivyo, Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa kura yako.

Mhe. Mwenyekiti: Hapana.

Katibu: Mhe. Mgeni Hassan Juma, hapana; Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, hapana; Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, hapana; Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, hapana; Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora, hapana; Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, hapana; Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais, hapana; Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, hapana; Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, hapana; Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, hapana; Mhe. Waziri wa Afya, hapana; Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, hapana; Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo; Mhe. Waziri wa Ardhi, Makazi, Maji na Nishati, hapana; Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili, hayupo; Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, hapana; Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi, hapana; Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika; Mhe. Suleiman Othman Nyanga, hayupo.

Wengine ni Mhe. Haji Faki Shaali, hapana, Mhe. Machano Othman Said, hapana; Mhe. Issa Haji Ussi, hapana; Mhe. Zahra Ali Hamad, hapana; Mhe. Dr. Sira Ubwa Mwamboya, hapana, Mhe. Bihindi Hamad Khamis, hapana; Mhe. Haji Mwadini Makame, hapana; Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi, hapana; Mhe. Othman Masoud Othman, hapana; Mhe. Abdalla Juma Abdalla, ndio; Mhe. Abdalla Moh'd Ali, ndio; Mhe. Abdi Mosi Kombo, hayupo; Mhe. Ali Salum Haji, ndio; Mhe. Amina Iddi Mabrouk, Mhe. Asaa Othman Hamad, ndio; Mhe. Asha Abdu Haji, Mhe. Asha Bakari Makame, hapana; Mhe. Ashura Shari Ali, Mhe. Bikame Yussuf Hamad, hapana; Mhe. Farida Amour Moh'd, hapana; Mhe. Fatma Mbarouk Said, hapana; Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Kwa kuwa waziri katika maelezo yake amesema hana wasi wasi na kuunda kamati, na mimi kwa kuwa ndiye mwenyekiti wa ile kamati, mimi sina tatizo na kuunda kamati.

Katibu: Tunataka kauli moja ndio au hapana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Sina tatizo na kuundwa kamati wacha iundwe.

Katibu: Mhe. Hamza Hassan hapa tunapiga kura hatutaki maelezo, tunachotaka ni ndio au hapana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: nasema iundwe.

Katibu: Mhe. Hassan Hamad Omar, Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe. Ismail Jussa Ladhu, ndio; Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mhe. Kazija Khamis Kona, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, ndio; Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando),

hapana; Mhe. Mlinde Mbrouk Juma, Mhe. Mohammed Haji Khalid, ndio; Mhe. Mohammed Mbwana Hamad, ndio; Mhe. Mohammed Said Mohammed, Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak, Mhe. Mussa Ali Hassan, hapana; Mhe. Mussa Khamis Silima, hapana; Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa, hapana; Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, Mhe. Nassor Salim Ali, hapana; Mhe. Omar Ali Shehe, ndio; Mhe. Panya Ali Abdalla, hapana; Mhe. Rashid Seif Suleiman, ndio; Mhe. Raya Suleiman Hamad, hapana; Mhe. Rufai Said Rufai, hapana; Mhe. Saleh Nassor Juma, Mhe. Salim Abdalla Hamad, ndio; Mhe. Salma Mohammed Ali, Salma Mussa Bilal, Mhe. Salmin Awadh Salmin, hapana; Mhe. Salum Amour Mtondoo, ndio; Mhe. Shadya Moh'd Suleiman, ndio; Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, hayupo; Mhe. Shawana Buheti Hassan, hapana; Mhe. Subeit Khamis Faki, ndio; Mhe. Suleiman Hemed Khamis, ndio; Mhe. Ussi Jecha Simai, Mhe. Viwe Khamis Abdalla, hapana; na Mhe. Wanu Khafidh Ameir, hapana.

(Uhesabuji wa Kura)

Katibu: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, katika kura zilizopigwa kura zilizosema ndio zilikuwa ni 20 na kura zilizosema hapana ni 39.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe baada ya kupatikana kwa matokeo ya kura za wajumbe wote, upande uliosema kwamba kamati teule iundwe ilikubaliwa na wajumbe 20 na upande ambao ulitaka kamati teule isiundwe umepata wajumbe 39. kwa hivyo, upande wa wale ambao wametaka kamati isiundwe wameshinda.

Kwa maeelekezo haya inaonekana mpaka hoja ya tatu imejibika vile vile. Hoja iliyosalia ni ya pili sasa, ambapo tuna taarifa kwamba Mhe. Makame Mshimba Mbarouk aombe radhi au athibitishe kauli yake.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwanza pole kwa kazi ngumu ndio mambo ya Baraza. Lakini mimi nadhani hoja kama ulivyosema zilikuwa tatu, kuna hoja ya kuunga mkono ripoti ya kamati nafikiri ilikuwa haina wasi wasi, hoja ya Mhe. Makame Mshimba kuundwa kamati teule, ndio imeshapigiwa kura, hoja tatu Mheshimiwa alitaka aombwe radhi.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, tunaposema kwamba Mhe. Makame Mshimba Mbarouk aombe radhi, ina maana Mhe. Mshimba radhi ile tayari alitaka iundwe kamati ili kuthibitisha. Hiyo kamati ambayo ingeundwa ndio ingetegemea aje aombe radhi au asiombe radhi. Lakini hivi sasa Mhe. Mshimba akiambiwa aombe radhi, aombe radhi kwa kitu gani kama hoja zake alizozitaka za msingi tayari zimekataliwa.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani kwa busara Mhe. Waziri mwanzo alitamka alipokuwa akifanya majumuisho yake akasema mimi sina tatizo na kuundwa kamati. Lakini pia itakapokuwa kamati imetakiwa isiundwe ina maana unapoleta suala la kuomba radhi Mhe. Mshimba yeye kuna maelezo aliyasema ana ushahidi nao na Mheshimiwa vile vile atakuwa na ushahidi nayo. Ina maana hapa tukitaka Mhe. Mshimba aombe radhi ina maana kamati itabidi lazima iundwe, vyenginevyo Mhe. Waziri na yeye tumuombe a-*withdraw* ili haya masuala yawe yamemaliza.

Kwa sababu leo tunaziba hili lakini kesho tunafunua jengine kwenye bajeti. Mimi kama Mwenyekiti wa Kamati sitopenda kuja kumuona Waziri wangu anasumbuliwa kwa mambo kama haya. Kwa hiyo, mimi kama Mwenyekiti wa Kamati namuomba Waziri suala hili ali-*withdraw* ili tumalize hii kazi yetu kwa salama.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, namheshimu sana Mwenyekiti wangu wa Kamati na busara anazotumia. Mimi sina tatizo lakini nasema *hansard* huko ndio iliyomnukuu Mhe. Makame Mshimba Mbarouk. *Hansard* ipo asubuhi hapa mara tatu Waziri na Katibu Mkuu wamekula *10 percent*. Sasa ile *hansard* nafikiri mtu akaifuta ni yeye. *Hansard* imeganda kule na itabaki ile *forever*. Sasa ana ushahidi gani, kama hana ushahidi basi a-*withdraw* yeye tu, tukitaka tumuombe radhi hapana neno, a-*withrdraw* ile *hansard* iliyonasa kule kwamba *10 percent* Waziri na Katibu Mkuu tumekula.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, mimi nimechaguliwa na wananchi. Waswahili wamesema "Nzi kufa kwenye kidonda si haramu". Nilichokieleza nina uhakika nacho na nikasema mimi sina dhana potofu ya *10 percent*, ndio nikataka iundwe kamati ili lile suala lieleweke. Namheshimu sana Waziri wangu niko pamoja na yeye katika utendaji wa kazi zetu lakini tusilee ubovu.

Mimi nasema kwa mantiki bwana, nimesema katika *document* ameeleza maneno mengi jamani, mngekaa mngeunda kamati nyinyi viongozi nyote mngelia hapa na mngeona mambo yote kwa hakika. Lakini kwa kuwa tunalindana sina tatizo. Sitoomba radhi mimi nasema.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, haya masuala yaliyopo sasa kwa mujibu wa kanuni ni baina ya mjumbe na mjumbe. Kanuni zetu zinasema kwamba hatakiwi mtu aseme yaliyokuwa sio. Pale ambapo mjumbe mmoja ndio aliyeambiwa kwamba sio ana wajibu wa kutaka ama mjumbe yule aliyesema athibitishe, akiwa hana uthibitisho basi aombe radhi ndio utaratibu wa kanuni.

Sasa kwa kuwa kanuni inasema hivyo, mimi nafikiri pengine Mhe. Waziri labda ningelichukua nafasi hii ya kusema kwamba kwa sababu hili suala limeshafika hatua ambayo tumeshakubaliana kwa baadhi ya sehemu labda na yeye atafakari. Hiyo *hansard* hivi sasa imeshaonesha kwamba Mhe. Waziri anakataa, ingawa ni mheshimiwa lakini Mhe. Waziri anakataa. Kwa hivyo, kuna *hansard* mbili sasa ya kusema na kukataliwa. Lakini nimuachie Mhe. Waziri kwa maamuzi yake ya mwisho.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, lazima tuive kiutendaji, tuive kama wawakilishi na tuive kwenye *element* ya kuheshimiana. Hichi ni chombo kikubwa sana, tusizungumze kwa jazba, kitu uwe na uhakika na ujue unayemwambia ni mwakilishi mwenzio anawakilisha jimbo kama wewe. Niko katika uwaziri miaka 10 sasa *Alhamdulillah* namshukuru Mwenyezi Mungu. Sasa unapom-*pin point* mwenzako kwa kitu kama hichi, kidogo inauma sana Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hiyo, naomba sana ndugu yangu kwa nia safi kabisa mimi nimekusamehe. Nawashukuru wote waliosema kwamba hakuna haja tunafanya kazi pamoja na tutalisafisha hili kwa manufaa ya nchi yetu. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe wanaounga mkono hoja ya kamati teule wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

KAMATI YA MIFUGO, UTALII, UWEZESHAJI NA HABARI

Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari (Mhe. Asha Bakari Makame): Mhe. Mwenyekiti, kabla sijawasilisha nataka nichukue nafasi hii nikupongeze kwa dhati kabisa kwa jinsi unavyoendesha kikao chetu hichi cha Baraza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, Bwana wa viumbe vyote, kwa kutujaalia uhai, afya njema na taufiki ya kuweza kukutana hapa leo hii kwa madhumuni ya kujadili mambo mbali mbali yenye maslahi mema na ustawi mzuri kwa nchi yetu na watu wake.

Mhe. Mwenyekiti, napenda nimpongeze Mhe. Spika kwa kuchaguliwa kwa mara nyengine tena kushika wadhifa huo muhimu wa uongozi wa Baraza hili

tukufu la kutunga sheria. Tunaamini uchaguzi wake umezingatia mchango wake mkubwa katika kuendeleza Baraza hili katika awamu zilizopita. Aidha, kwa niaba ya kamati yangu nawapongeza wale wote walioteuliwa kushika nyadhifa mbali mbali za uongozi wa taifa hili na tunawaombea Mwenyezi Mungu awazidishie uwezo, upeo, busara na hekima katika uongozi wao.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza lako tukufu lina majukumu makubwa ya Kitaifa yakiwemo yale yaliyoelezwa katika kifungu cha 88 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984, ambapo kifungu cha 88 (a) kinaeleza yafuatayo:-

”Baraza la Wawakilishi litakuwa na kazi ya kutunga sheria pale ambapo utekelezaji wa jambo unahitaji kuwepo kwa sheria hiyo”. Hivyo, ni wazi kuwa Baraza hili ni muhimili muhimu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutokana na majukumu hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kama mnavyofahamu Kamati yetu imeundwa kwa mujibu wa kifungu cha 104 (h) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi - Zanzibar, toleo la mwaka 2011. Majukumu na kazi za Kamati hii yameainishwa katika kanuni ya 113 ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi ambapo pamoja na mambo mengine Kamati ina majukumu ya msingi yafuatayo:

a) Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye Ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia.

b) Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara husika kwa kadri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji Bajeti na Hotuba nyengine za Mawaziri walizotoa Barazani.

c) Kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Kitaifa na miradi ya wananchi ya Wizara husika.

d) Kuchunguza na kufuatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha.

e) Kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka.

f) Kushughulikia Miswada ya Sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika.

g) Kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufuatilia utekelezaji wa ahadi hizo.

h) Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari imepewa majukumu ya kusimamia Wizara tatu zifuatazo:

- Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo
- Wizara ya Mifugo na Uvuvi
- Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu ina Wajumbe saba na makatibu wawili. Naomba niwatambulishe Wajumbe wa Kamati kwa majina kama ifuatavyo:

1.	Mhe. Asha Bakari Makame	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Mohammed Said Mohamed		M/ Mwenyekiti
3.	Mhe. Assaa Othman Hamad	-	Mjumbe
4.	Mhe. Salim Abdalla Hamad	-	Mjumbe
5.	Mhe. Abdi Mosi Kombo	-	Mjumbe
6.	Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Mjumbe
7.	Mhe. Kazija Khamis Kona	-	Mjumbe
8.	Ndg. Asma Ali Kassim	-	Katibu
9.	Ndg. Abdu Maulid Haji	-	Katibu

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka huu wa fedha 2010/2011, Kamati yetu ilifanya kazi kwa muda wa wiki nne kati ya Unguja na Pemba. Kuanzia tarehe 31/1/2011 hadi tarehe 11/2/2011 huko Pemba na kumalizia kazi zake kwa upande wa Unguja kuanzia tarehe 28/2/2011 hadi tarehe 11/3/2011.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu kimsingi imeridhika na utendaji wa Wizara zote 3 ilizozitembelea. Kamati inawapongeza kwa dhati watendaji wa Wizara zote kwa juhudi kubwa wanayoichukua kutekeleza majukumu yao licha ya mazingira magumu wanayokabiliana nayo.

Kwa kuendelea naomba sasa niwasilishe mbele ya Baraza lako Tukufu, muhtasari wa taarifa ya utekelezaji wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka huu wa fedha 2010/2011 kwa kuchambua Wizara moja moja, huku nikigusia utekelezaji, changamoto na maoni ya Kamati.

WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, UTALII NA MICHEZO

Mhe. Mwenyekiti, natumai sote tunaelewa na kufahamu kwa kina umuhimu uliopo kwa Wizara hii na vitengo vyake huku tukitilia maanani kuwa kupata habari ni haki ya msingi kwa kila Mtanzania. Hivyo, Wizara hii inabeba jukumu zito la Kitaifa la kuwa ni mdomo na kiungo muhimu kwa mawasiliano kati ya Serikali na watu wake.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inatoa pongezi za dhati kwa Wizara kwa kulifanyia matengenezo makubwa jengo la Makao Makuu ya Wizara lililopo Mnazi Mmoja ambapo jumla ya shilingi milioni 70 zilitumika. Jengo hilo linawapa fursa watendaji wa Wizara kutekeleza majukumu yao ipasavyo, kwani Kamati imewashuhudia wakiendelea vyema na ujenzi wa Taifa. Hata hivyo, Kamati imesikitishwa na hali ya jengo la Wizara hii huko Pemba kwani liko katika hali mbaya na ya hatari kwa wafanyakazi na wananchi wengine wanaofuata huduma afisini hapo.

Mhe. Mwenyekiti, katika kada ya michezo, Kamati yetu imesikitishwa mno na hali mbaya za viwanja vyetu vyote vya michezo. Kwa kweli, viwanja hivi vinahitaji kuangaliwa kwa jicho la huruma.

Kwa kuanzia na Uwanja wa Amaan, Kamati iliarifiwa kuwa uwanja huo umefungwa kwa muda kutokana na tatizo la kuharibika *tartan* baada ya kutumika kwa ajili ya Sherehe za Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. Aidha, nyasi za uwanja huo nazo zimekufa kutokana na kuoteshwa kwenye udongo ambao rutuba yake imemalizika. Hivyo, Kamati inaishauri Wizara itafute mbinu mbadala za kuziendeleza nyasi hizo, kwani ni aina bora ya nyasi zinazodumu kwa muda mrefu.

Kwa upande wa Uwanja wa Mau, Kamati ilijionea uchakavu wa uwanja huo ambao kwa sasa uko chini ya dhamana ya *ZFA*. Hivyo, Kamati imeitaka Wizara kuurejesha uwanja huu kwenye udhibiti wake ili kuuendeleza na kufikia hadhi inayostahiki.

Mhe. Mwenyekiti, Uwanja wa Gombani Pemba umekosa matunzo yanayostahiki kwani Kamati ilitegemea kuukuta katika hali nzuri baada ya kupokea taarifa kwamba umefanyiwa matengenezo. Tunaishauri Wizara

kuchukua jitihada za hali ya juu kurekebisha kasoro zilizopo katika uwanja huu ambao ni uwanja pekee unaotegemewa kwa Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, utalii ni sekta inayokua kwa kasi visiwani Zanzibar na inahitaji kuenziwa kwa ajili ya kukuza uchumi wetu. Katika usimamizi wake ni dhahiri kuwa tunahitaji taasisi imara ambazo zitabuni njia madhubuti za kupambana na vyombo vyengine vya nje ya nchi ili kuwavutia watalii wengi zaidi kutembelea nchi yetu. Kwa mantiki hiyo basi, Kamati inaiomba Serikali kulipa heshima na haki Shirika la Utalii liendeshe shughuli zake kibiashara, ili liweze kupunguza mzigo kwa Serikali kwa kujiendesha lenyewe na kuchangia katika pato la Taifa.

Aidha, Kamisheni ya Utalii nayo inahitaji kuwa na akaunti yake yenyewe badala ya kutegemea kasma inayotoka Wizara ya Fedha ambayo husababisha usumbufu mkubwa wanapohitaji kufanya matumizi.

Mhe. Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kuwa katika kuimarisha sekta ya utalii nchini, Wizara ina mchango mkubwa kwa kushirikiana na taasisi nyengine kama Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Kamati yetu imepata fursa ya kutembelea Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume na kushuhudia jinsi wageni (watalii) walivyofurika uwanjani hapo na kulazimika kukaa chini huku wengi wao wakijipepea kutokana na upungufu mkubwa wa vipooza hewa *(AC).* Huo ni udhaifu mkubwa ambao unaweza kusababisha kupungua kwa idadi ya watalii wanaoingia nchini hasa wale wa daraja la kwanza ambao ni watu wanaohitaji matunzo ya hali ya juu.

Mhe. Mwenyekiti, elimu ndio msingi imara wa kusimamisha lengo lolote la kimaendeleo katika karne hii ya sayansi na teknolojia. Katika kufanikisha maendeleo ya utalii nchini, Wizara inawajibika kukifanyia matengenezo ya hali ya juu chuo cha utalii kwa kukijengea majengo ya kisasa yanayokwenda sambamba na taaluma inayotolewa chuoni hapo. Mafunzo kwa njia ya vitendo nayo pia yana umuhimu wake kwa wanafunzi wa chuo hicho na hivyo Kamati imeshauri kupatiwa vifaa vya mafunzo kwa njia ya vitendo *(practical)* wanafunzi wa chuo hicho ili kuwafanya wawe bora zaidi kwenye soko la ajira.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu imetembelea Hoteli ya Bwawani na kujionea hali halisi ya uchakavu wa baadhi ya maeneo. Kwa kweli, hoteli hii iko katika hali ya kusikitisha mno kwamba ni hoteli kubwa inayotegemewa na Serikali na hadi hivi sasa haina utambulisho wa kisheria *(legal status).* Hali hii imetokana na kuhamishwa hoteli hiyo kutoka katika Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na kupelekwa kwenye Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Kutokana na hali hii, hoteli haiwezi kupata fursa ya mkopo kutoka benki kwa ajili ya kujiimarisha zaidi. Kwa hivyo, Kamati inaiomba Wizara

ifuatilie kwa kina suala la kupatikana kwa utambulisho wa kisheria wa hoteli ili tuweze kupata tija iliyokusudiwa.

Aidha, Kamati imebaini udhaifu mkubwa kwenye mikataba ya ukodishwaji wa Hoteli ya Bwawani kwani hoteli imekodishwa kwa bei ndogo mno ukilinganisha na hadhi yake na zabuni nyengine za bei ya juu zilizokuwepo. Hivyo, Kamati inalishauri Baraza lako tukufu kufanya kila linalowezekana kuiwezesha kufanya kazi muda wa ziada ili kupata fursa ya kulifuatilia kwa kina tatizo hili kwa maslahi ya Taifa letu na wananchi wake.

Zaidi ya hayo, changamoto nyengine ya hoteli ya Bwawani ni ile ya wafanyakazi wa hoteli hii kutokujua hatma ya ajira zao. Wafanyakazi hao walieleza malalamiko yao juu ya mazingira yasiyoridhisha wanayokabiliana nayo katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku. Kamati imegundua kuwa wafanyakazi hao huajiriwa kwa muda mfupi mfupi kati ya miezi 3 na 6 kinyume na sheria za kazi zinavyoagiza. Hivyo, Kamati imeiagiza Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika kulifuatilia kwa karibu zaidi suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, utamaduni ndio kitambulisho cha wazi cha utaifa wa jamii yoyote ile. Kwa hapa Zanzibar, utamaduni wetu umeanza kupotea kutokana na sababu mbali mbali zikiwemo athari za utandawazi. Kwa kuzingatia hili, Kamati imeiagiza Idara ya Utamaduni kuandaa Sera na Sheria ya kulinda utamaduni wetu.

Kwa madhumuni makubwa ya kuwalinda watoto na majanga yanayoweza kuwapata yakiwemo yale ya kutumbukia katika mambo maovu na kuharibu mustakabali mzima wa maisha yao. Kamati imeitaka Wizara kuzuia *(disco toto)* kwenye kumbi zote ambazo zinauzwa pombe.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imeiomba Idara ya Makumbusho kulifanyia matengenezo jengo lake lililopo Forodhani *(People's Palace)* kwani limebainika kuwa ni chakavu na limepoteza haiba yake ya awali. Aidha, Idara imetakiwa kununua samani zinazoendana na zile za asili za jengo hilo, ili matengenezo hayo yasiathiri matumizi ya jengo hilo kama ni makumbusho.

Mhe. Mwenyekiti, kwa nia njema kabisa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeanzisha Shirika la Utangazaji na hadi sasa Shirika hilo limo kwenye safari ngumu ya kuelekea kwenye matumizi ya teknolojia ya *digital* kwani lina upungufu mkubwa wa vifaa vya redio na televisheni. Hali hii imesababishwa na kutokuwepo fungu maalum kwenye Bajeti kwa ajili ya Shirika hilo changa ambalo linahitaji kujiendesha.

Aidha, katika utengenezaji wa Gazeti la Serikali la Zanzibar Leo vifaa vya kisasa vinahitajika ukiwemo mtambo wa kuchapia gazeti hilo ambalo kwa sasa linachapishwa huko Tanzania Bara na kugharimu fedha nyingi. Mtambo huo unakadiriwa kugharimu jumla ya shilingi milioni 70 na unategemewa kuongeza ufanisi wa gazeti hilo ikiwa ni pamoja na kutolewa kwa wakati.

Halikadhalika, maslahi yasiyoridhisha kwa watendaji wa Shirika hilo yamewafanya baadhi yao kutafuta sehemu nyengine za kufanyia kazi nje ya Zanzibar. Hali hii inalirudisha nyuma shirika, kwani utendaji bora huchangiwa na kuwepo kwa watendaji wenye uzoefu na ujuzi wa kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imejionea changamoto kubwa ya Wizara hii kwa upande wa Pemba kuwa ni kushindwa kuwapatia wananchi wa Pemba matangazo ya televisheni kwa muda wa miaka mingi. Hali hii kwa kiasi kikubwa imesababishwa na uchakavu wa vifaa na kupelekea wananchi hao kuangalia televisheni nyengine za nje ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imeitaka Bodi ya Sensa iwajibike kuzuia uingizwaji wa filamu zote ambazo haziendani sambamba na maadili ya Mzanzibari, kwani vijana wengi wameshatumbukia katika kuiga maadili yanayokwenda kinyume na silka na utamaduni wa Mzanzibari. Zoezi hilo linaweza kusaidia kuwalinda vijana wetu na wimbi kubwa la mporomoko wa maadili.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imeitaka Idara ya Magofu na Mambo ya Kale kuchukua juhudi za makusudi kuhakikisha inatoa matangazo ya ndani na nje, ili kuhakikisha idadi ya wageni wanaokuja kutembelea katika maeneo ya kihistoria wanaongezeka, ili kuongezeka kwa mapato ya serikali na kuinuka kiuchumi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imeitaka Wizara iandae mipango madhubuti ya kupewa kipaumbele Kiwanja cha Gombani, ili iwe ni chachu ya kukuza mapato yatokanayo na kiwanja hicho. Pamoja na kuhakikisha matumizi bora ya fedha hizo, inaonekana kiwanja hicho kufikia hadhi yake inayostahiki.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

Mhe. Mwenyekiti, Sekta ya Mifugo na ile ya uvuvi ni tegemeo la idadi kubwa ya watu hususan wale wanaoishi katika ukanda wa pwani vikiwemo visiwa vya Unguja na Pemba. Kwa msingi huo basi, Serikali imeamua kuunda Wizara maalum itakayoshughulikia maendeleo ya mifugo na uvuvi kwa maslahi ya Taifa hili.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu ilifanya ziara kwenye Wizara ya Mifugo na Uvuvi na kujionea miradi mbali mbali ya wananchi kama ifuatavyo:

- **KAMATI YA UVUVI - MTAMBWE KUSINI (Mitambuuni)**

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilipata fursa ya kukagua Kamati ya Uvuvi ya Mtambwe- Kusini na kuikuta ikiwa na migogoro kadhaa. Kubwa zaidi ni ule mgogoro wa uendeshaji wa boti ya uvuvi iliyotolewa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia mradi wa *MACEMP*. Kamati ilielezwa kuwa, boti hiyo iko mikononi mwa Sheha na wananchi waliobakia hawafaidiki nayo kwa njia yoyote kwa zaidi ya mwaka mmoja sasa. Hatimaye, Kamati iliamua kwamba chombo hicho kikabidhiwe kwa Kamati ya Uvuvi na faida ya muda wote aliokitumia chombo hicho Sheha ielezwe bayana na kugawiwa kwa wanakamati wote. Pia, Kamati yetu iliiagiza Kamati ya Uvuvi ya Mtambwe Kusini kufanya uchaguzi chini ya usimamizi wa Idara ya Uvuvi, ili boti hiyo itakapokabidhiwa iwe chini ya usimamizi utakaoridhiwa na pande zote.

- **MRADI WA UVUVI- MTAMBWE KUSINI (Makongeni)**

Mhe. Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa, Kamati ilipokea taarifa za kutoendelea vyema kwa mradi huu ambapo wanakikundi walieleza wasi wasi wao kuwa ni watu wachache tu kati yao ndio wanaofaidika na mapato ya mradi huo. Kutokana na matatizo hayo, baadhi ya wanakikundi waliamua kukitia moto chombo hicho na hadi sasa kimo kwenye matengenezo makubwa. Kamati ilishauri kuwa kwa vile boti kwa sasa imo kwenye matengenezo, mashine na nyavu vikodishwe kwa ajili ya kupata fedha angalau za kuendeshea kikundi hicho. Aidha, kumbukumbu zote za mahesabu ziwekwe vyema ili kuwafanya wanakikundi wawe na imani na uongozi wa mradi huo kwa nia ya kujiendeleza zaidi.

- **KIKUNDI CHA UVUVI (TWENDE NA WAKATI) - MTAMBWE KASKAZINI**

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu ilishuhudia kikundi hichi kikiwa na mafanikio kiasi na ilishauri mambo yafuatayo yafanyike ili kukiimarisha zaidi.

Kwanza, kikundi kiweke kumbukumbu za fedha kwa uangalifu mkubwa na akaunti ifunguliwe ili fedha hizo ziwe salama zaidi.

Wanakikundi wapange mikakati mizuri ili waweze kununua mashine ndogo ya boti itakayotumia mafuta kidogo na kuwaongezea tija.

Kutatua tatizo la ukosefu wa soko la kudumu la samaki na bei zisizoridhisha, wanakikundi wameshauriwa kupeleka samaki wao katika maeneo yenye upungufu wa samaki hao.

- **KIKUNDI CHA UVUVI (TUSHIKAMANE) – MTAMBWE KASKAZINI**

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imejionea matatizo ya kutokuwa na ushirikiano kati ya wanakikundi wa Tushikamane ambayo yamekwamisha maendeleo ya kikundi hicho na kuagiza mambo yafuatayo:

Wafanye uchaguzi wa viongozi wa kikundi hicho, kwa kushirikiana na Idara ya Uvuvi ambapo kabla ya uchaguzi huo, vifaa vyote vya kikundi vikabidhiwe kwa sheha na baadaye sheha avikabidhi kwa Mwenyekiti mpya atakae chaguliwa.

Wanakikundi waache kuchanganya itikadi zao za kisiasa kwenye miradi ya maendeleo kwani watagawanyika na kushindwa kufanya kazi zao kwa pamoja.

- **KARANTINI YA MIFUGO – GANDO**

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilipokea taarifa kwamba, eneo kwa ajili ya uanzishwaji wa karantini ya mifugo tayari limeamuliwa, ikiwa ni utekelezaji wa ahadi ya Wizara katika mkutano wa bajeti uliopita. Aidha, Kamati imepata fursa ya kulitembelea eneo hilo lililopo Gando-nzi wengi na kubaini kuwa hatua za uanzishwaji wake zitahitaji fedha nyingi na utaalamu wa kutosha. Hivyo, Kamati imeishauri Wizara kuandaa mpango wa muda mrefu wa utekelezaji wa mradi huu hatua kwa hatua na kutafuta fedha kutoka kwa washirika mbalimbali wa maendeleo badala ya kusubiri fedha kutoka Serikalini kwani kasma ya Wizara pekee haikidhi kuliendeleza eneo hilo.

- **UFUGAJI WA SAMAKI – CHOZI**

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu mchanga umeanzishwa mwezi Januari 2011 na Kamati imewashuhudia wanakijiji wa Chozi wakiwa katika Harakati za awali za uchimbaji wa mabwawa ya kufugia samaki.

Lakusikitisha ni kwamba, wanakijiji hawa wanatumia nguvu zao nyingi, bila ya kuwa na uhakika juu ya mradi wenyewe kwani wakati Kamati ilipowatembelea bado hakujafanyika utafiti wowote wa kitaalamu kuhusu athari za kimazingira kwa mradi wanaouanzisha. Kutokana na hali hiyo, Kamati imeishauri Wizara kufanya tafiti za kina kwa miradi ya wananchi, kabla ya kuanza miradi

yenyewe ili kuelekeza nguvu zao kwa pamoja kwenye miradi yenye manufaa zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa upande wa Uguja, Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ilifanya ziara katika Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi kwa kupokea taarifa na kutembelea miradi mbali mbali kama ifuatavyo:

- **SHAMBA LA MALISHO YA MIFUGO – KIZIMBANI**

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu imelitembelea Shamba hili lenye ukubwa wa ekari 18, lililo chini ya usimamizi wa Wizara na kubaini kuwa halina hatimiliki na hivyo kurahisisha uvamizi wa wananchi kwa ajili ya matumizi mengine yakiwemo ya kuwapatia malisho wanyama wao. Kamati imeishauri Wizara kuyatafutia hatimiliki mashamba yake yote haraka iwezekanavyo ili kuyalinda yasivamiwe kwa matumizi mengine.

- **CHINJIO LA KISAKASAKA**

Mhe. Mwenyekiti, kamati iliarifiwa kwamba Sera na Sheria ya mifugo haviendi sambamba na wakati tulionao, kwani katika chinjio kuu la Kisakasaka, kiwango cha shilingi 300/- hutozwa kwa kuwekwa karantini ng'ombe kwa siku moja, ada ya kuchinja ng'ombe mmoja ni shilingi 800/-, ambapo mbuzi huchinjwa kwa shilingi 400/- tu. Viwango hivi ni vidogo mno kwa maisha ya sasa na haviwiani na gharama halisi za uendeshaji wa chinjio hilo. Hivyo, Kamati imeshauri kufanywa marekebisho ya Sheria hiyo ili kupata fedha angalau za kuliendesha chinjio na kulifanyia usafi unaohitajika ili kuhakikisha ulinzi wa afya ya jamii yetu.

Aidha, kamati imeelezwa kuwa, senyenge iliyozungushiwa eneo la nje ya chinjio hilo huharibika mara kwa mara kutokana na kuwa karibu na bahari. Pia, Kamati iliishuhudia nyumba ya wafanyakazi iliyopo katika eneo hilo ikiwa katika hali mbaya mno na hivyo kuishauri Wizara kuijenga upya nyumba hiyo badala ya mpango wake wa sasa wa kutaka kuifanyia matengenezo.

Katika chinjio hilo, Kamati imearifiwa kuwepo kwa wafanyakazi 13 tu ambao hulazimika kufanya kazi ya ziada kwani takriban ng'ombe 20 huchinjwa kwa kila siku. Kutokana na hali hiyo, Kamati imependekeza kuongezwa kwa wafanyakazi kituoni hapo ili kuongeza ufanisi wa kazi zao.

Halikadhalika, Kamati imejionea tatizo la uvamizi wa eneo la Wizara katika shamba la Kisakasaka ambapo baadhi ya wananchi wameanzisha makazi na kupanda miti ya kudumu katika eneo hilo, kwa madai ya kuwa eneo hilo ni mali yao. Kwa hivyo, Kamati inaiomba serikali kuisaidia Wizara kulitatua

tatizo hili kwa kulipatia hatimiliki eneo hili pamoja na kuwachukulia hatua kali wavamizi hao ili iwe fundisho kwa wananchi wengine wenye tabia kama hiyo.

- **MWANGAZA WALEMAVU – NYAMANZI**

Mhe. Mwenyekiti, ni kikundi cha ufugaji kinachojishughulisha na ufugaji wa ng'ombe wa kisasa. Kamati imeshuhudia mafanikio yaliyopatikana kwenye kikundi hichi cha walemavu kwani tangu kuanzishwa kwake rasmi mwezi Mei 2010, wameweza kuunga maji, kununua gari la ng'ombe na zaidi ya yote wameanza kugawana mitamba kwa wanakikundi mmoja mmoja.

Pamoja na mafanikio makubwa waliyoyapata, wanakikundi hao wanakabiliwa na changamoto kama:

Fedha za kikundi ziko mikononi mwa mshika fedha, Kamati imeagiza kikundi hicho kufungua akaunti yake benki kwa uhifadhi bora wa fedha hizo.Wizara imetakiwa kuweka daktari maalumu kwa kila kanda na kuwapatia usafiri wa uhakika madaktari hao ili kuwawezesha kuwapandishia ng'ombe kwa wakati muwafaka.

- **KIKUNDI CHA KUENDELEZA UTALII – FUMBA**

Mhe. Mwenyekiti, kikundi hichi kimefadhiliwa na MACEMP/TASAF na kinajishughulisha na kusafirisha watalii hadi kwenye visiwa vidogo vidogo vya bahari ya Fumba. Katika utendaji wao wa kila siku, wanakikundi wameieleza Kamati kwamba wanakabiliwa na changamoto zifuatazo:

Hadi hivi sasa kikundi kimeshindwa kupata usajili kutoka Idara ya vyama vya ushirika
Kikundi hakina akaunti ya benki na jumla ya shilingi 1,800,000/- za kikundi ziko mikononi mwa mshika fedha.

Kuna uharibifu mkubwa wa matumbawe kwenye visiwa vidogo vidogo wanavyopelekwa watalii hali ambayo inahitaji kudhibitiwa kwa haraka. Kutokana na matatizo waliyonayo wanakikundi hicho, Kamati imeshauri yafuatayo:

Wanakikundi wafanye mawasiliano ya moja kwa moja na hoteli wanazofikia wageni, ili waweze kupata wageni wengi zaidi na kwa bei yenye maslahi mazuri, badala ya hali ya sasa ambayo inawapa fursa mapapasi kujinufaisha wao binafsi kwa kupitia migongo yao.
Kikundi kifanye haraka iwezekanavyo kufungua akaunti benki ili kuwa na uhifadhi zaidi wa fedha zao.

- **MKUTANO NA WAVUVI – MATEMWE KIGOMANI**

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilipata fursa ya kusikiliza maoni ya wavuvi wa Shehia za Matemwe, Pwani mchangani, Nungwi na Kijini ambao waliieleza Kamati juu ya mgogoro wao wa muda mrefu kuhusu mradi wa ukodishwaji wa kisiwa cha Mnemba (MIMKA). Mradi huu umeelezwa kuwa na faida ndogo sana kwa wananchi kwani mnamo mwaka 2004, wanakijiji walipatiwa jumla ya shilingi 1,000,000/- kwa kila shehia kati ya shehia zote nne zilizotajwa hapo juu na baadaye fedha hazikupatikana tena. Wananchi hao waliiomba Kamati kuwatafutia ufumbuzi wa mgogoro huo. Nayo Kamati kwa upande wake imeitaka Wizara iwasilishe taarifa kamili ya mgogoro huu ili kujuwa jinsi gani ifuate taratibu za kuutatua mgogoro huo.

- **MAABARA YA MIFUGO – MARUHUBI**

Mhe. Mwenyekiti, kamati imearifiwa kwamba maabara ya ufuatiliaji wa mwenendo wa maradhi, iliyopo Maruhubi imeshindwa kufanya kazi kwa miaka mitano sasa kutokana na ukosefu wa *KIT*.

Aidha, maabara inakabiliwa na upungufu wa watendaji wenye fani maalumu kama vile wataalamu wa uchunguzi wa minyoo "*parastology"*. Vile vile, uhaba wa mashine za uchunguzi wa maradhi ya mimea na mifugo pamoja na uchakavu wa zile zilizopo unakwamisha shughuli za kila siku za maabara.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu imejionea maendeleo ya mradi wa kupandisha ng'ombe kwa njia ya sindano (*artificial insemination*), ambayo umeanzishwa mwaka 2009, na unaendelea na uzalishaji wa mbegu bora za ng'ombe na kuzisambaza nchi nzima baada ya kupatikana kwa nyenzo muhimu ya *"liquid nitrogen"* ambayo ilikosekana kwa muda mrefu na kuzorotesha uzalishaji. Kamati imeishauri Wizara kufikiria mpango wa kuuza mbegu hizo za ng'ombe wa kisasa baada ya kutosheleza mahitaji ya lazima kwa wafugaji wazalendo ili kupata fedha kwa kuuendeleza mradi huu.

Mhe. Mwenyekiti, maendeleo ya wananchi wa visiwa hivi ni jambo linalotiliwa maanani sana na Wizara hii. Kamati imearifiwa kuwa, Wizara inaendelea na utafiti wa mwani bora wa aina ya "*Cottonii"* kwenye kina kirefu cha bahari ya Fundo na Uvinje, chini ya wataalamu kutoka Taasisi ya Sayansi ya Baharini (*IMS*). Kukamilika kwa utafiti huu kutawasaidia wakulima wa mwani kujua ni maeneo gani yanayofaa zaidi kwa kulima mwani wa aina hii ambao ndio wenye tija zaidi.

WIZARA YA KAZI, UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI NA USHIRIKA

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika ni Wizara mpya katika Serikali ya Mapinduzi Zanzíbar ya awamu ya saba, yenye muundo wa umoja wa Kitaifa. Wizara hii imeundwa rasmi Novemba 2010, ikiwa na jukumu Kubwa la kusimamia shughuli zote za kuongeza ajira kwa vijana na kuinua hali zao na taifa kwa ujumla. Kimuundo, Wizara ina Idara saba, Kamisheni moja na Afisi kuu Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imearifiwa kwamba programu ya pamoja ya mashirika ya umoja wa mataifa JP 5 iliyoanza mwaka 2008 iliendelea kutekelezwa, kwa nia ya kupunguza umasikini kwa kuongeza ajira, kutoa mafunzo kwa wajasiri amali, kuweka mfumo wa hifadhi ya jamii kwa wote na kutekeleza kwa vitendo sheria za kazi. Vile vile, Wizara ilisimamia ziara ya watendaji wa ILO na wabunge kutoka Norway kwa wajasiriamali walionufaika na misaada ya shirika la kazi duniani kupitia programu hiyo ya UN JP 5.

Mhe. Mwenyekiti, Katika harakati za kuwawezesha wananchi kiuchumi na kuwatoa katika janga la umasikini uliokithiri, Wizara inaendelea kuratibu mfuko wa uwezeshaji wa wananchi kiuchumi (JK na AK). Shughuli kuu za utendaji wa mfuko huu zinatekelezwa na Kamati za Uratibu za Wilaya, Shehia na Benki ya watu wa Zanzibar. Pamoja na hayo, Kamati imeishauri Wizara ipewe mamalaka zaidi katika kusimamia mfuko huu badala ya Benki ambayo inaonekana kuuendesha zaidi mfuko kibiashara kwa kujiongezea faida zaidi kupitia kiwango cha riba ambacho wananchi wengi hawakimudu.
Aidha, Kamati imewatembelea waliopata mkopo wa JK na AK na kubaini mambo yafuatayo:

- **WALIOFAIDIKA NA MFUKO WA AK NA JK- MICHEWENI**

Kamati ilikutana na wananchi waliopata mkopo wa AK na JK wa Wilaya ya Micheweni

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwenyekiti wa kamati, naona tumuombe Mhe. Waziri Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais, ili tutenge kando kanuni tuweze kuongeza muda na kuweza kumalizia ripoti yako. Mhe. Waziri karibu.

HOJA YA KUONGEZA MUDA

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa muda ulio mbele yetu hautoshi kumaliza shughuli zilizo mbele yetu.

Kwa hivyo, naliomba Baraza lako liridhie kutengua kando kanuni ili tuweze kuongeza muda na kuweza kumaliza shughuli zilizokuwa mbele yetu. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji waliokubali hoja ya Mhe. Waziri wanyooshe mkono juu. Waliokataa. Waliokubali wameshinda. Tuendelee.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mhe. Mwenyekiti anaendelea na hotuba yake ya kamati baada ya kuongezwa muda)

Mhe. Asha Bakar Makame (Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari):

- **WALIOFAIDIKA NA MFUKO WA AK NA JK- MICHEWENI**

Kamati ilikutana na wananchi waliopata mkopo wa AK na JK wa Wilaya ya Micheweni na kubaini kwamba, wananchi hao hawaelewi utaratibu mzima wa mikopo wa Serikali na hivyo kuiagiza Wizara kuwafanyia utaratibu maalumu wa ziada wa kuwaelimisha wananchi hao.

Zaidi ya hayo, Kamati ilielezwa kwamba, gharama za uendeshaji wa mkopo, riba pamoja na nauli ya kutoka Micheweni kwenda Wete zote hubebwa na Wananchi hao na hivyo kutopata faida iliyokusudiwa ya mkopo huu. Kamati imeshauri Wizara kuwaandalia mpango wa ufuatiliaji wa mikopo kiwilaya na kufikiria suala zima la kupunguza kiwango cha riba ili kupunguza gharama hizo na kuwakwamua wananchi hao kwenye matatizo ya kiuchumi waliyonayo.

- **TUJUWANE *SACOSS*- KONDE**

Mhe. Mwenyekiti, wakati kamati yetu ilipoitembelea *SACOSS* hii ya Wanawake watupu, iliwakuta wakiendelea na shughuli zao kwenye jengo la kukodi ambalo linawagharimu jumla ya shilingi 480,000/- kwa mwaka na kuwashauri kuanzisha ujenzi wa jengo la Afisi yao ya kudumu, ambapo Kamati iliahidi kuwaunga mkono baada ya kuona nguvu zao. Aidha, Kamati iliarifiwa kwamba mashine yao ya kutengenezea chaki ni mbovu.

- **MIKOPO JK/AK KWA WATU BINAFSI- OLE**

Kamati ilipata fursa ya kumtembelea ndugu Hamdu Yussuf ambaye amepatiwa jumla ya shilingi 3,000,000/- kwa kuendeleza mradi wake wa gereji, na kubaini kuwa pamoja na marejesho mazuri anayoyafanya, bado anakabiliwa na matatizo ya kukosa jengo la kutosha kufanyia kazi zake na zana za kisasa kadhalika hajapata. Pia, Kamati imepokea ombi la kupunguzwa kwa mzigo mzito wa riba kutoka kwa bwana huyu na kuitaka Wizara kulifanyia kazi ombi hilo.

Wakati Kamati ilipomtembelea ndugu Thiney ambaye pia alipatiwa milioni 3,000,000/- kwa ajili ya mradi wa kuzalisha chumvi, hali ilikuwa ni tufauti mno kwani ulipaji wake ulikuwa unasuasua kutokana na kukosa soko kwa chumvi aliyokwisha izalisha. Hivyo, Wizara imeshauriwa kuwasaidia wananchi wanaopatiwa mikopo katika suala zima la kutafuta masoko ya bidhaa zao ili waweze kulipa vizuri mikopo hiyo. Vile vile, Wizara imetakiwa kumchukulia hatua kali za kisheria yeyote ambaye atathibitika kutolipa fedha hizi kwa uvivu na kutowajibika ipasavyo katika kazi yake.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ilipata fursa ya kutembelea Harakati *SACOSS*, ushirika wa jambo nia, ushirika wa Kibokoni *SACOSS* na Mwanzo mgumu *SACOSS* ya Mkanyageni kwa upande wa Pemba. Kuanzia tarehe 9/3/2011 hadi tarehe 11/3/2011, Kamati yetu iliikagua Wizara hii kwa upande wa Unguja na kuzitembelea *SACOSS* mbali mbali kama ifuatavyo:

- **ZIMWA *SACOSS*- Chukwani**

Ni *SACOSS* inayobeba dhana ya Utaifa kwani ina jumla ya matawi manne Unguja na Pemba. *SACOSS* hii imepatiwa jumla ya shilingi milioni 30 kutoka mfuko wa AK/JK na hadi kufikia Januari 2011, wanadaiwa shilingi milioni 19. Ulipaji wao ni mdogo sana na hawana será wala masharti yoyote yanayotolewa wakati wa utoaji wa mikopo hiyo kwa wanachama wake. Hivyo, Kamati imeitaka Wizara kushirikiana bega kwa bega na *SACOSS* hiyo katika kupanga na kutekeleza mikakati ya kurejesha fedha hizo ili zitolewe kwa wanachama wengine.

- ***SACOSS* ya Shehia ya Mombasa**

Mhe. Mwenyekiti, kamati iliitembelea *SACOSS* hii ambayo imepata jumla ya milioni 120,800,000/- kati ya fedha zote za Mkoa wa Mjini Magharibi ambazo ni milioni 400. Aidha, Kamati iliarifiwa kwaba *SACOSS* hii ni ya mfano kwa Unguja kwani imefanikiwa kulipa vizuri mkopo wake ambapo imebainika

kwamba mashirikiano yaliyopo baina ya Wananchi, Sheha na Mratibu wa uwezeshaji wa Wilaya ndiyo siri ya mafanikio yao.

Mhe. Mwenyekiti, wizara ilieleza kwamba imefanikiwa kusajili vyama 95 vya ushirika Unguja na Pemba, ambayo ni sawa na asilimia 63 ya malengo iliyojiwekea. Aidha, Kamati yetu ilipata fursa ya kutembelea vikundi mbalimbali vya ushirika na kushuhudia mafanikio na matatizo waliyonayo kama ifuatavyo:

1. MUWAPE *SACOSS*

Ni SACOSS ya Wilaya nzima ya Wete ambayo asilimia 90 ya wanachama wake ni Wanawake. Wanakikundi wamefanikiwa kuandaa mpango ambao unakaribia kukamilika wa kuanzisha *SACOSS* bank lakini wanakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa utaalamu wa uendeshaji wa miradi yao. Pia, kikundi kinaendesha shughuli zake kwenye jengo la kukodi ambalo linawagharimu fedha nyingi. Hivyo, Kamati imeitaka Wizara kuwapatia mafunzo yanayohitajika hasa kwa uendeshaji bora wa SACOSS hii, na kuwaandalia mpango wa kupata jengo la Afisi ili kupunguza gharama.

2. KIKUNDI CHA UKULIMA WA MBOGA MBOGA- LIMBANI

Kamati imekagua kikundi hichi na kujionea mafanikio makubwa yaliyopatikana kwenye ukulima wa mboga mboga kwa njia ya umwagiliaji (*drip irrigation*), ufugaji wa ng'ombe, mbuzi na bata. Changamoto kubwa ya kikundi ni kukosa umiliki wa eneo wanaloendeshea harakati zao. Hivyo, Kamati imeitaka Wizara kulipima eneo hilo na kuwaombea serikalini ili wakabidhiwe kwa ajili ya shughuli zao kwani ni eneo la serikali lililokosa matumizi kwa muda mrefu.

Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe fursa hii kuwapongeza wana kamati wangu wote kwa mashirikiano makubwa ambayo walishirikiana na mimi kwa kutembelea sehemu mbali Mbale.

HITIMISHO

Mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu inatoa shukurani za dhati kwa usikilizaji mzuri wa Waheshimiwa Wajumbe, wakati wote wa uwasilishaji wa hotuba hii na tunatoa wito kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzíbar, kuyatekeleza kwa vitendo yale yote yaliyoagizwa na kushauriwa na Kamati ili kuongeza ufanisi wa wizara zetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kwa vile muda umekwisha na kazi yetu leo ilikuwa ni kubwa mno. Sasa tumefikia pahala kwamba tunaliahirisha Baraza hili mpaka siku ya Jumatatu, saa 3:00 asubuhi.

(Saa 1:47 usiku Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 04/04/2011 siku ya Jumatatu saa 3:00 za asubuhi)